

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Pili – Tarehe 3 Novemba, 2021

(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa Tano na leo ni Kikao cha Pili, jana kilikuwa Kikao cha Kwanza. Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa yanayokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MHE. AMINA IDDI MABROUK K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Amina Amour. Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Swali la kwanza linakwenda Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya Mbunge wa Meatu.

Na.16

Barabara za *TARURA* Kupandishwa Hadhi

MHE. LEAH J. KOMANYA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipandisha hadhi barabara za *TARURA* zinazochochea ukuaji wa uchumi kwenda *TANROADS* ili zipatiwe fedha za kutosha za kufanya matengenezo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, TAMISEMI hapo hapo ulipo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kupandisha hadhi barabara ni la kisheria kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa. Barabara ambayo inakidhi vigezo kutoka daraja la barabara ya wilaya kwenda daraja la barabara ya mkoa inatakiwa ijadiliwe kwenye kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa husika. Ikionekana inakidhi vigezo ndio Bodi hiyo kupitia Mwenyekiti wake itamshauri Waziri mwenye dhamana na barabara kuwa barabara husika imekidhi vigezo vyta kuwa na hadhi ya

Barabara ya Mkoa na hivyo ipandishwe daraja na kuwa Barabara ya Mkoa chini ya *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uwezo wa *TARURA* hususani uwezo wa rasilimali fedha, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo, itaendelea kuiwezesha *TARURA* kwa kuiongezea fedha na kuijengea uwezo ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na weledi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hiyo, katika mwaka wa fedha 2021/2022 zimetengwa shilingi bilioni 966.90 ikilinganishwa na shilingi bilioni 275.03 zilizotengwa mwaka wa 2020/2021 kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya barabara na madaraja zinazosimamiwa na *TARURA*.

SPIKA: Mheshimiwa Leah Komanya, nilikuona.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nashukuru majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa barabara ya Mwanuzi hadi Mwabuzo, kilometra 42 imekuwa ni barabara muhimu kutokana na wafanyabiashara wanaotoka Wilaya ya Meatu na Maswa kwenda Igunga kufanya biashara na hata magari ya kusafirisha pamba. Kikao cha DCC kilipeleka maombi Mkoani na RCC walishapeleka Wizarani. Je, Serikali haioni haja ya kuipandisha barabara hiyo kuwa ya *TANROADS?* (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kipande cha Mwabuzo – Igunga, kilometra 36 kimekuwa ni cha muhimu kutokana na biashara inayofanyika hadi mabasi saba yanapita katika barabara hiyo na wakati wa masika yanalazimika kuitia Shinyanga mpaka Igunga, kilometra 300. Je, Serikali haioni haja ya kuifungua barabara hiyo kutoka Mwabuzo kilometra 36 hadi daraja la Manonga kilometra 36? (*Makof!*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, nimekuona Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba nitoe maelezo ya maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jeremiah ambayo yameulizwa kwenye Ofisi ya Rais, TAMISEMI kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hii ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja walipeleka maoni yao katika ngazi ya wilaya kama utaratibu ulivyo, yamefika kwenye ngazi ya mkoa wakajadili kwenye *RCC* yao na sisi Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tumeshatuma watalaaam wetu katika eneo hilo, ma-*engineer* wameenda wametafuta tafuta taarifa mbalimbali. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge avute Subira, watalaaamu wetu walete majibu yale, halafu kama itakidhi vigezo barabara hiyo itapandishwa hadhi na kuhudumiwa na *TANROADS*ili iweze kutengenezwa na ipitike wakati wote.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; barabara yake ya pili ambayo ameizungumza, tumeipokea kwa uzito tutaifanyia kazi, tuombe ushirikiano ili barabara hiyo iweze kufanyiwa matengenezo ya kudumu na wananchi wa eneo hilo waendelee kupata huduma muhimu kwa njia ya barabara. Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Deo Mwanyika.

MHE. DEODATUS P. MWANYIKA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza. Barabara ya Mtila - Lugenge mpaka Usalule ni barabara ya muhimu sana nani barabara inayounga wilaya tatu ikiunga pamoja na Hospitali kubwa ya Mkoa wa Njombe. Je, Serikali haionti kwamba ni muhimu sana hii barabara na yenyeWE ikaingizwa katika mpango wa *TANROADS* kwa sababu mchakato umeshaanza na umekwama mahali Fulani? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swalii hilo, bado tupo kwa Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwanyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hoja hii Mheshimiwa Mbunge amefikisha ofisini katika Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Kama alivyosema mwenyewe kwamba mchakato unaendelea, naomba *a-speed up process* hiyo na sisi tutatoa ushirikiano, itakapokidhi vigezo tutaipokea kama *TANROADS*, tutaitengeneza na wananchi wake watapata huduma muhimu katika eneo hilo. Ahsante.

SPIKA: Turudi tena Meatu, Mheshimiwa Luhaga Mpina.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Kwa kuwa barabara ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Meatu Mheshimiwa Leah Komanya ni barabara ambayo pia inaungana na barabara ya kutoka pale Mwabuzo ikaenda Kabondo, Itinje, Mwandwitinje mpaka Mwaukoli na inaunganisha na zote hii inatoka Bariadi nyngine inatoka Meatu zinaenda zote Mkoa wa Tabora na Wilaya ya Igunga.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu mapendekezo haya yote tuliyaapeleka kwa pamoja kama ambavyo Naibu Waziri wa Ujenzi amejibu, sasa anaweza kunihakikishia kwamba haya maombi yote yanafanyiwa kazi kwa pamoja na muda mfupi ujenzi utaanza wa barabara hizi sasa kuwa za mkoa na baadaye ujenzi kuanza mara ili kuondoa changamoto zilizopo kwa sasa kutokana na *TARURA* kushindwa kumudu kukidhi mahitaji yake?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mpina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie Bunge lako Tukufu kumwagiza Meneja wa Mkoa wa Simiyu, Shinyanga na Mwanza na maeneo yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameshaleta mapendekezo kwenye maeneo haya, wafanye kazi ya tathmini haraka iwezekanavyo, wawasilishe majibu Wizarani na sisi kama Serikali tuweze kuchukua hatua ili maeneo hayo yaweze kutengenezwa kwa haraka na wananchi wote waweze kupata huduma ya barabara. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea, bado tupo TAMISEMI Waheshimiwa, kwa sababu ya muda Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe uliza swali lako sasa.

Na. 17

**Uhaba wa Watumishi na Vitendea kazi Halmashauri
ya Wilaya ya Manyoni**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA K.n.y. MHE. AYSHAROSE N.
MATTEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Watumishi pamoja na vitendea kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni?

SPIKA: Ahsante sana Dkt. Chaya, majibu la swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Dkt. Dungange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu: -**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa watumishi, mwezi Julai, 2021, Serikali ilipeleka watumishi 28 wakiwemo watumishi 19 wa

Sekta ya Afya na watumishi tisa wa Sekta ya Elimu. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, imepanga kuajiri jumla ya watumishi 477 ili kupunguza changamoto ya upungufu wa watumishi. Pamoja na jitihada hizo, Serikali itaendelea kufanya msawazo wa watumishi katika Halmashauri zote ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kwa kadri ya mahitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vitendea kazi, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni imetenga na kuidhinishiwa bajeti ya shilingi milioni 705.85 kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo samani za ofisi pamoja na magari manne kwa gharama ya shilingi milioni 430.00. Mpaka sasa, Halmashauri ipo katika hatua za mwisho za ununuzi wa magari mawili ya awali kwa gharama ya shilingi milioni 220.00 yatakayosaidia kupunguza changamoto ya upungufu wa magari. Kwa ujumla, Serikali itaendelea kununua vitendea kazi kwa ajili ya halmashauri hiyo kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Chaya, swali la nyongeza.

MHE. DKT. PIUS S. CHAYA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; katika Jimbo la Manyoni Mashariki hususan Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, tuna upungufu mkubwa sana wa Watendaji wa Vijiji na tayari tulishapeleka maombi ya kupata kibali cha kuajiri Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Kata. Je, ni lini Serikali itatupatia kibali sasa cha kuwaajiri Watendaji wa Vijiji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika Jimbo la Manyoni Mashariki tuna kilimo kikubwa sana cha korosho kwa kutumia *block farming*. Je, Serikali haionti sasa kuna umuhimu wa kusaidia kupeleka wataalam wa kilimo ili kuchochea uwekezaji huo? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili Dkt. Dugange, nimekuona.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya Mbunge wa Manyoni Mashariki, lakini pia Mheshimiwa Massare Mbunge wa Manyoni Magharibi na Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe kwa kazi kubwa sana wanazozifanya kwa pamoja, kuhakikisha wananchi wa Manyoni na Singida kwa ujumla wanapata miradi ya maendeleo kwa ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tuna changamoto ya upungufu ya Watendaji wa Vijiji na Kata katika halmashauri zetu zilizo nyingi. Serikali inaitambua changamoto hii na tathimini na mpango mkakati unaendelea kuandaliwa, hatua nzuri ili tuone namna gani tunakwenda kujaza nafasi za Watendaji wa Vijiji na Kata katika maeneo yetu ili waweze kusimamia kwa ufanisi zaidi shughuli za maendeleo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kulifanya kazi hilo na litapatiwa ufumbuzi kwa awamu na kwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunahitaji wataalam wa kilimo lakini pia wa kada mbalimbali. Nalo pia linafanyiwa kazi na kwa kadri ya uwezo wa Serikali na upatikanaji wa wataalam hao tutaendelea kuajiri ili wakafanye kazi hizo. Nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na swali linalofuata la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua Mbunge wa Kilindi.

Na. 18

Hitaji la Gari la Wagonjwa Kilindi

MHE. OMARI M. KIGUA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Gari la Wagonjwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tupo kwako Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Dkt. Festo John Dugange, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Jimbo la Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali kupitia fedha za Mkopo wa Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) imetenga shilingi bilioni 46.94 kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa 253, ambapo magari 195 yenye thamani ya shilingi bilioni 35.1 yatanunuliwa kwa ajili ya halmashauri zote 184, ambapo kupitia magari hayo Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi itapatiwa gari moja la wagonjwa. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Kilindi.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Binafsi nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa uamuzi wa busara sana sana wa kununua magari katika halmashauri zote za Tanzania yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; ni ukweli usiopingika kwamba huduma ya *ambulance* ni muhimu sana katika kuwahudumia wananchi wa Tanzania. Hata hivyo, huko nyuma imejitokeza changamoto kwamba huduma ya magari haya ya *ambulance* yanapelekwa sehemu moja mawili, matatu wakati sehemu nyingine hakuna magari kabisa. Sasa nini mpango wa Serikali katika kuepuka hili siku za usoni? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; Serikali imefanya jambo jema sana, inaenda kujenga vituo vya afya kwenye tarafa takribani nchi nzima. Je, nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba tarafa zote hizo pia zinapata magari ya wagonjwa kwa maana ya *ambulance*? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Dkt. Dugange, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza nipokee shukrani nyingi ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitoa kwa Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na ni kweli Dhahiri, shahiri inaonyesha kazi kubwa sana ambayo Serikali yetu ya Awamu ya Sita inaifanya katika kuboresha huduma za afya katika nchi yetu kwa kasi kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumekuwa tunapeleka magari ya wagonjwa katika halmashauri mbalimbali, lakini kuna vigezo ambavyo vimekuwa vikizingatiwa wakati tunapeleka magari na ndiyo maana kumekuwa na utofauti kidogo wa idadi ya magari yanayopelekwa kwenye halmashauri moja ikilinganishwa na magari yanayopelekwa kwenye halmashauri nyingine. Moja ya vigezo ni pamoja na idadi ya wananchi, wingi wa vituo vya afya, lakini pia idadi ya matukio ya magonjwa mlipuko, lakini na ajali za barabaranii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaratibu huu ni wa kisera tutaendelea kufanya hivyo, lakini jambo la msingi ni kuhakikisha halmashauri zetu zote zinapata magari ya wagonjwa angalau kutimiza majukumu hayo bila kujali wingi wa wagonjwa na kadhalika, kwa maana ya kuhakikisha kwamba huduma zinapatikana vizuri. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge jambo hili tunalizingatia na mipango yetu ni kuendelea kuboresha.

Mheshimiwa Spika, la pili, katika ujenzi wa vituo vya afya katika kila tarafa; tunahitaji kuwa na vituo vya afya

vyenye magari ya wagonjwa na magari haya yataendelea kuwekwa kwenye mipango na kufikishwa kwenye vituo vya afya vinavyojengwa katika tarafa zetu kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Pia kama nilivyotoa taarifa hapa, tuna magari mengi ya wagonjwa yanakwenda kununuliwa mwaka huu wa fedha na hivyo tutaendelea kuboresha utaratibu huo kufikisha magari hayo. Nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa tuokoe muda, tuelekee Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, swali la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

Na. 19

Muundo wa Maafisa

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itabadilisha Muundo wa Utumishi wa Maafisa Utumishi/Utawala na Walimu ili waweze kuanza na Daraja E kama ilivyo Kada ya Sheria na nyaginezo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri Utumishi na Utawala Bora Mheshimiwa Deogratius John Ndejembji, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinkyo Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya Kada mbalimbali inayotumika sasa katika Utumishi wa Umma iliandaliwa kwa kuzingatia matokeo ya zoezi la Tathmini ya Kazi iliyofanyika kuanzia mwaka 1998 hadi 2000. Aidha, Miundo husika ilianza kutekelezwa mwezi Julai, 2003.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya zoezi la tathmini ya kazi ilioainisha uzito wa majukumu ya kada mbalimbali katika utumishi wa umma na yallyotumika kama msingi wa kupanga vianza mshahara kwa watumishi wa umma wa kada mbalimbali wakiwemo Maafisa Utumishi na Utawala ambao wanaanza na ngazi ya mishahara ya *TGS D*, walimu Daraja C yaani walimu wenyewe shahada ambao wanaanza na ngazi ya mshahara *TGTS D* na Maafisa Sheria ambao wanaanza na ngazi ya mshahara ya *TGS E*.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 hadi 2017 Serikali iliendesha zoezi lingine la tathmini ya Kazi katika Utumishi wa Umma ambalo lililenga kubaini uzito wa majukumu kwa kada mbalimbali. Katika kuoanisha na kuwianisha viwango vyta mishahara vyta watumishi katika Utumishi wa Umma, Serikali itatumia matokeo ya mapendekezo ya zoezi hilo kupanga vianzia mshahara vyta kada mbalimbali ikiwa ni pamoja na Maafisa Utumishi na Utawala na Walimu kwa kuzingatia uwezo wa kibajeti. Naomba kuwasilisha.

SPIKA: Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza naipongeza Serikali kwa nia hiyo njema ya kutamani kuboresha stahiki za watumishi, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa sasa tathmini imeshafanyika tangu mwaka 2015/2017 ya kufanya marekebisho ya muundo na mishahara ya watumishi: Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza jambo hili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kumekuwa na ucheleweshaji mkubwa sana wa mafao ya watumishi wanapostahili: Ni nini kauli thabiti ya Serikali kuwahakikishia watumishi wanapostahili watapata stahiki zao/mafao yao kwa wakati? (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Deo Ndejembii, majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nitoe pongezi zangu kwa Mbunge wa Hai, Mheshimiwa Saashisha kwa kuwa anaafuatilia sana masuala ya kiutumishi hasa yale ya watumishi katika jimbo lake na yale ambayo yanahusu wastaifu wanaotoka katika Wilaya ile ya Hai na jimboni kwake.

Mheshimiwa Spika, sasa nikienda kwenye kujibu swalı lake la kwanza, Serikali tayari ilishaanza mpango wa kuweza kufanya kazi ile tathmini iliyofanyika 2015/2017. Tayari kuna kada ambazo zilishafanyiwa kazi ambapo kwa zoezi liliyofanyika mwaka 2015, kada ya Wahasibu, *Internal Auditors* na hawa washika fedha; kada hizo zilikuwa zinatofautiana sana katika ngazi ya mshahara, lakini ukiangalia elimu wanayosoma, ilikuwa ni moja. Kwa hiyo, tayari Serikali imeanza kufanya mpango huo.

Mheshimiwa Spika, vile vile mwaka 2017 ilifanyika tathmini ya Watumishi wa Umma wote, kuangalia ulinganifu ikiwemo kwenye ma-engineer ukiangalia katika wanasheria na kadhalika. Sasa katika utekelezaji kama unavyofahamu Serikali itatekeleza pale tu kwa uwezo wa kibajeti katika kulipa mishahara. Kama tunavyoona jitihada zinazofanyika na Serikali za kuboresha uchumi wetu chini wa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan, uchumi wetu ukiboreka, basi tutafanya kazi na kuboresha maslahi ya watumishi wetu.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swalı lake la pili, Watumishi wa Umma inatakiwa inapofika mienzi sita kabla ya kustaafu, tayari waanze na kujiardaa na nyaraka mbalimbali. Sasa changamoto imekuwa ikijitokeza unakuta mtu ajira yake ya kwanza alianzia Halmashauri ya Kongwa ,lakini anapokuja kustaafu, anastaaafia Ukerewe, tatizo linakuwa kwenye *documentation*. Halafu mtu anakuja kukumbushwa suala hili la Maafisa Utumishi limebaki mwezi

mmoja, anapoanza kufuatilia barua yake ya ajira, iko Kongwa. Sijui alipata uhamisho kwenda Songea; akatoka akaenda kustaafia Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utakuta changamoto kwenye *documentation* na mtu huyu hana nauli, ndiyo maana mafao yanachelewa, lakini tayari tumeanzisha mfumo wa *HCMIS* ambao utahakikisha taarifa zote za mtumishi zipo na zinaanza *notification* walau miezi sita kabla.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali tunafanyia kazi mfumo huu, nawaasa Maafisa Utumishi wote nchi nzima kuhakikisha wanaangalia *records* za watumishi wao wanaokaribia kustaafu wawape taarifa walau mienzi sita kabla, ili isije ikafika nauli imekwisha, anakaribia kustaafu kesho, ndiyo anakumbushwa aanze kutafuta taarifa zake. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Getere nimekuona.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Hili suala la wastaafu kwa kweli ni kero kubwa katika nchi yetu. Nashukuru majibu ya Serikali, lakini niseme tu Serikali inatakiwa kujitahidi kwenye jambo hili, kwa sababu wastaafu waliomaliza *ku-document document* zao ambao wapo kwenye maeneo, wanaolia, wanaokwenda kwenye maofisi, wana miezi sita, miaka tano, miaka minne, ni wengi kuliko ilivyo kawaida.

Kwa hiyo, Serikali itafute mfuko thabiti wa kuzingatia mambo haya ili watu waweze kupata fedha zao. Watu wanakuwa wanadai fedha, kwa nini mtu ameitumikia nchi, halafu anakuwa anadai fedha.

Mheshimiwa Spika, naiomba tu Serikali itengeneze jambo hili liwe nzuri zaidi.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri na Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma. Naomba niliambie Bunge lako Tukufu, Serikali ya Awamu ya Sita na hasa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma baada ya kuingia na kugundua kwamba wakati mwingine ucheleweshaji wa mafao hayo ya wastaifu yanatokana na haya malimbikizo ya michango. Michango mingi ambayo inatakiwa ipelekwe na waajiri, imekuwa ikicheleweshwa kupelekwa kwa mazingira ya aina moja ama nytingine. Serikali imekuwa na suluhu hiyo ya kutengeneza mfumo ambao utawasaidia wafanyakazi wote kutambua ni lini wanastaifu na haki zao zikoje?

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha sasa na upande wa plili wa mifuko, tumewaagiza na wameshatikeleza. Kwa mfano, Mfuko wa *PSSSF* wameshatengeneza mfumo ambao unaitwa *PSSSF Kiganjani*. Mfumo huo sasa umeshasambazwa na unaendelea kusambazwa kwa wanachama wote. Wanachama ambao wanakaribia kustaifu, wamekuwa sasa wakiwezeshwa kuzitambua haki zao kupitia kwenye mfumo na kuanza kuwasiliana na ofisi zote kabla ya muda kustaifu ili kupunguza hiyo kadhia ambayo imekuwa ikiendelea.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo tumewahagiza Mfuko wa *PSSSF* na mifuko mingine, kabla ya muda wa kustaifu, wastaifu wote watarajiwa tumeanzisha sasa vikao maalumu mfuko kukutana na wastaifu watarajiwa kuwatambua na kuandaa mafao yao mapema na hivyo kadiri tunavyokwenda kadhia hii itakuja kuondoka na tunapenda wastaifu waweze kupata mafao yao kwa muda unaotakiwa. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu yanatia moyo sana haya. Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri wakati anajibu, amesema moja ya changamoto ya kuchelewa

kulipwa kwa wastaaifu ni pamoja na waajiri kuchelewa kupeleka michango. Wakati jana nimeomba mwongozo, nimepokea *message* 165, wengine hawajalipwa kuanzia mwaka 2012; lakini kwenye Bunge la Bajeti Mheshimiwa Waziri aliji-*commit* kwamba atafanya ziara kwenye vyombo vyote vyta habari kuhakikisha wanapeleka michango ili Waandishi wa Habari na watu wengine binafsi walipwe kwa wakati. Sasa nataka niulize, ni lini ataanza hiyo ziara ili Waandishi wa Habari michango yao ipelekwe ili na wenyewe wawe na uhakika, baada ya kumaliza kazi zao wapate stahiki zao? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, masuala haya ya haki ya wafanyakazi ni masuala yanayotakiwa kuangaliwa kwa utaratibu mzuri sana. Masuala haya hayafanani tu labda na maamuzi ya mtu, kuamua kukaa hapa, ukae na nani na ufanye nini? Hapana, ni lazima kuyatengenezea utaratibu madhubuti.

Mheshimiwa Spika, naomba kumwambia Mheshimiwa Mbunge, tumeshaanza hiyo kazi. Kazi ya kwanza tulioifanya ni kupata ushirikiano kutoka kwa Waandishi wa Habari, kutambua vyombo ambavyo vimekithiri kwa kutokulipa mishahara na mafao ya Waandishi wa Habari. Kazi hiyo, tumeshaitekeleza na baada ya hapo sasa ndipo tutakwenda kuanza ziara ya kukutana na vyombo hivyo. Huwezi kuanza tu kukutana nao kabla hujapata taarifa.

Kwa hiyo, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge Serikali inafanya kwa utaratibu, inatengeneza mikakati kusudi utaratibu huo ukianza kuchukuliwa hatua, hatua hizo ziwe zimezingatiwa kwa mujibu wa sheria na utaratibu. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, tunashukuru. Waheshimiwa kwa sababu ya muda, naomba tuendelee.

Waheshimiwa Wabunge, mtu anayestaafu leo kwa miaka 60 maana yake amezaliwa mwaka 1961; na kama alianza kazi ana miaka 20, maana yake ni *around* mwaka 1970 hivi au 1971 ndiyo alianza kazi. Anapostaafu tu anaenda kufuatilia mafao, anaambiwa sasa kalete kwanza barua yako ya ajira, na barua ya kuthibitishwa kazi mwaka 1972 na sijui kitu gani; Sasa ninyi mmeniajiri miaka yote, tangu 1970; wengi wenu hapa hata mwaka 1970 mlikuwa hamjazaliwa. Leo ndiyo mnaniuliza karatasi za mwaka 1970 na ninyi ndiyo waajiri wangu Serikali miaka yote! (*Makofî*)

Kwa hiyo, yako maeneo ya kuangalia kidogo kwa upande wa mwajiri pia. Yaani pasiwepo na visababu. Ndiyo watu wengi wanakosa haki zao kwa sababu hiyo, kwamba aliajiriwa Muleba, sasa anamaliza kazi yake Tandahimba. Anaanza kuambiwa Muleba mwaka 1970 ulipoajiriwa, kalete karatasi Muleba, hawezi. Wengi sana wanakuwa... (*Makofî*)

Tunaendelea na Wizara ya Maji, swali linaulizwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako.

Na. 20

Mradi wa Maji Vijiji vya Ikelu - Nyamande - Mahongole

MHE. DEO K. SANGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji katika Vijiji vya Ikelu, Ibatu, Mtulingala, Nyamande, Usetule Mahongole Wilayani Makambako?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, nimekuona Mheshimiwa Winfred Mahundi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji vya Ikelu, Ibatu, Mtulingala, Nyamande, Usetule na Mahongole. Utekelezaji wa mradi wa maji katika Kijiji cha Ikelu umefikia asilimia 98 na umeanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi wa kijiji husika. Kazi zilizobaki ni ulazaji wa bomba umbali wa kilometra 29.8, ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa lita 25,000 na ufungaji wa pampu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Desemba, 2021.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa maji katika Kijiji cha Ibatu umefikia asilimia 56 ambapo kazi zilizobaki ni ukamilishaji wa ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 100,000, ufungaji wa pampu ya kusukuma maji pamoja na uunganishaji wa umeme. Mradi huo umepangwa kukamilika mwezi Machi, 2022. Aidha, utekelezaji wa miradi katika Viji vya Mtulingala - Nyamande - Mbugani na Usetule – Mahongole kwa pamoja umefikia asilimia 67 na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Machi, 2022.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa utekelezaji wa miradi hiyo kutaboresha huduma ya upatikanaji wa maji na kunufaisha wananchi wapatao 18,000 wa vijiji hivyo.

SPIKA: Mheshimiwa Deo Sanga, umeridhika na majibu hayo?

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali. Pamoja na majibu mazuri ya wananchi wa vijiji hivi ambavyo vimetajwa, nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza: Pamoja na Naibu Waziri kutamka hapa kwamba vijiji hivi vitapata maji mwakani na kingine cha Ikelu kina asilimia 98: Tatizo ambalo lipo aniambie hapa, Wakandarasi hawa wamesimama, hawaendelei kwa sababu hawajalipwa fedha; ni lini watalipwa fedha ili waweze kukamilisha miradi hii? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili: nazungumza kwa uchungu, Pamoja na kwamba Wizara ya Maji wanafanya kazi nzuri sana na Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Awamu ya Sita, kazi yake ni nzuri sana. Kuna jambo ambalo nataka nizungumzie hapa unisaidie katika miji 28 ambayo ilikuwa ipate maji kupitia fedha za mkopo nafuu kutoka India, limezungumzwa kwa muda mrefu, mojawapo ni Makambako nayo ipo kwenye miradi hiyo... (*Makofii*)

SPIKA: Sasa swali Mheshimiwa.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, sasa swali. Katika Mji wa Makambako ambao unategemea mradi huu mkubwa, una Kata tisa. Unapitiwa na Kata tisa. Wananchi hawa tumekuwa tukiwaambia kwa muda mrefu: Ni lini Mkandarasi atakwenda kuanza kutengeneza mradi huu? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Maji, Mheshimiwa Eng. Maryprisca Winfred Mahundi, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Kasenyenda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba kusema Wakandarasi tayari malipo yanaendelea na malipo tunalipa kwa awamu kadri ambavyo tunapata fedha. Ninaamini hata Wakandarasi wa Makambako nao kwa mgao wa mwezi huu wa Kumi ambao tunaugawa mwezi huu wa Kumi na Moja, nao wataingizwa katika malipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na miji 28, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wetu Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, amefatilia kwa karibu sana suala hili na tayari wakandarasi wapo; na wenzetu kutoka Benki ya *Exim* kutoka India wamefika Tanzania, hapa Dodoma juzi na jana pia tulikuwa na kikao nao. Hivi ninavyoongea kikao kinaendelea ndio maana Mheshimiwa Waziri hapa hayupo. Kwa hiyo,

niseme tupo mwishoni kabisa kuona kwamba *story* za suala hili la miji 28 sasa linafikia ukingoni. Tumshukuru sana Mheshimiwa Rais ameweza kusimamia kwa karibu suala hili mpaka linaelekea ukingoni. Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Kwa hiyo, officially sasa ni miji 28 eeh! Ahsante sana. Mheshimiwa Aida, bado tupo Wizara ya Maji.

Na. 21

Changamoto ya Maji - Nkasi Kaskazini

MHE. AIDA J. KHENANI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza changamoto ya maji katika Jimbo la Nkasi Kaskazini?

SPIKA: Bado tupo kwako Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika Wilaya ya Nkasi ni wastani wa asilimia 52.2. Katika kutatua changamoto ya huduma ya majisafi na salama katika Jimbo la Nkasi Kaskazini, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi minne ambayo ni Kirando, Namanyere, Mataala na Katongolo. Miradi hii imepangiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Desemba, 2021.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuanzia mwezi Januari, 2022 Serikali itaanza utekelezaji wa miradi ya maji katika Vijiji vya Korongwe, Lyazumbi, Masolo, Mpata, Isale na Kakoma na utekelezaji wa miradi hiyo umepangwa kukamilika mwezi Oktoba, 2022. Kukamilika kwa miradi hiyo, kutawanufaisha wananchi wapatao takribani 97,000.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mji wa Namanyere, Serikali inaendelea na uboreshaji wa huduma ya majisafi na salama kwa kutumia chanzo cha maji cha Bwawa la Mfili. Ujenzi wa mradi huo unahusisha kazi za ujenzi wa chanzo, ufungaji wa pampu mbili zenyenye uwezo wa kusukuma lita 80,000 za maji kwa saa, ulazaji wa bomba kuu kilometa 3.9, ulazaji wa bomba la kusambaza maji kilometa 6.4, ujenzi wa tanki la lita 500,000. Ujenzi wa mradi huo umepangwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Desemba, 2021.

Mheshimiwa Spika, aidha, kupitia mradi wa Maziwa Makuu wa kutumia Ziwa Tanganyika, Serikali imekamilisha usanifu wa kina na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Tanganyika. Kupitia mradi huo, vijiji 32 vya Halmashauri ya Nkasi vinatarajwa kunufaika.

SPIKA: Kwa majibu hayo mazuri, Mheshimiwa Aida bado una swali la nyongeza? Haya nakuruhusu.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi, nami niulize maswali mawili ya nyongeza. Kabla sjaauliza, tunafungwa sana na Sheria ya Takwimu, lakini naomba Bunge lako Tukufu, sheria hii isiwe ni kichaka cha kutoa takwimu za uongo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri anasema upatikanaji wa maji ni asilimia 52, wakati nafika hapa Meneja ananijibu ni asilimia 27. Sijui nani mkweli kati ya hizo taarifa? Nakosa maneno ya kusema kwa sababu ya Sheria ya Takwimu kwa sababu mtaniambia nimefanya *research* kupitia nini?

Mheshimiwa Spika, na mimi naomba kusema kwa sababu kwa miradi hiyo...

SPIKA: Hapa Bungeni unaruhusiwa, wewe sema tu, mradi usidanganye tu.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, Wana-Nkasi wanasikia, akisema asilimia 52, wakati Kata zenyewe uhakika wa kupata maji hazizidi mbili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kuna miradi miwili ambayo ni miradi kichefukichefu; Mradi wa Isale na Mradi wa Namanyere ambaao una zaidi wa miaka mitatu; na miradi hiyo hata ikikamilika haiwezi kabisa kutatua changamoto ya maji Jimbo la Nkasi Kaskazini: Serikali haioni sasa kuna haja ya kuchukua Maji Ziwa Tanganyika ambayo ni kilometra 64 tu kuweza kumaliza changamoto ya maji? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili: Kwa kuwa Serikali imepata huo mkopo ambaao imegawa kwenye Wizara za Kisekta ikiwepo Wizara ya Maji, napenda kujua, Jimbo la Nkasi Kaskazini tunapata kiasi gani ili angalau ikapunguze makali ya changamoto za maji? (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Aida, ile miradi miwili ndiyo ile Mheshimiwa Ally Keissy alikuwa analalamikia sana? Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aida Joseph Khenani kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Dada yangu, Mheshimiwa Aida, kwa ufuatiliaji wa suala hili la miradi hii ya maji na nipayende kukuhakikishia Mheshimiwa Aida kwamba miradi hii ambayo umeiita kichefuchefu tayari Wizara tumeipa nguvu na tutaisimamia kwa karibu sana kuona kwamba inakamilika. Kwa sababu lengo la Mheshimiwa Rais ni kumtua ndoo Mama kichwani nasi kama Wizara ya Maji ni wanufaika wakubwa wa fedha kutoka Serikali Kuu, hivyo, nikutoe hofu, nikuhakikishie tutasimamia na miradi hii itakamilika kama ambavyo miradi mingine mingi zaidi ya 200 ilivyoweza kukamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kuhusu fedha za *Covid*. Katika Jimbo la Nkasi Kaskazini pia wamekuwa wanufaika wa hizi fedha ambazo Mheshimiwa Rais ameweza kuzipigania. Tumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa sababu wananchi wa Nkasi Kaskazini na wao wametengewa milioni 500 kwa lengo la kufanya mradi wa Mpata.

Mheshimiwa Spika, lengo la hizi fedha ni kufanya mradi utakaokamilika ndani ya miezi sita, miezi tisa, uweze kutoa maji na wananchi wanufaika. Hivyo, tumeweza kuweka mradi mfupi ambao ndani ya shilingi milioni 500 utakamilika na wananchi watanufaika moja kwa moja. Kwa miradi hiyo ya Namanyere tayari ipo ina bajeti, kama Namanyere ina bilioni 1.5. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge nitaendelea kukupa ushirikiano kama ambavyo tumekuwa tukiwasiliana. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Kamishna Halima Mdee, uliza swali lako.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani sasa hivi tunavyozungumza ambayo inahudumiwa na mitambo ya Ruvu Chini, nazungumzia Bagamoyo, nakuja Jimbo langu la Kawe pale, nakwenda Kinondoni, Temeke, kuna uhaba mkubwa sana wa maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasema kwa sababu kuna upungufu wa maji, yaani kina cha maji kimepungua. Sasa ninataka Serikali iniambie, kwa sababu kupungua kwa maji kwa vyovyote vile kuna uhusiano na mabadiliko ya tabianchi, dunia nzima sasa hivi inazungumzia *climate change*. Leo nimemsikiliza Rais anasema anataka Serikali mtenga fedha za *climate change*.

Mheshimiwa Spika, nataka nipate majibu sahihi ili tatizo hili lisiwe la kudumu, kuna mkakati gani wa muda mfupi na muda mrefu kuweza kukabiliana na upungufu huu wa maji

ili wananchi wa maeneo husika waepukane na kero hii? Hasa kwa kuzingatia miradi husika tumejenga kwa fedha za mikopo za mabilioni ya shilingi ambayo Taifa linalipa sasa hivi. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Halima Mdee kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli mitambo yetu ya Ruvu Chini hapa katikati ilipata hitilafu ya kupata maji kwa upungufu lakini kama Wizara tuna mabonde tisa ambayo yanafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa sana kuona kwamba tunadhibiti tatizo hili. Tatizo hili ni kwamba matumizi ya shughuli za kibinadamu kwa sehemu kubwa ndiyo yameathiri.

Mheshimiwa Spika, huwa tunatoa vibali kwa wenzetu kufanya umwagiliaji maeneo karibu na vyanzo vyetu vya maji lakini vina muda. Muda ambao unapaswa kutumika ni muda ule wenye *high season*, maji yanakuwa mengi na muda huu wa kiangazi vile vibali huwa vina-expire. Sasa wale wamwagiliaji wamekuwa wakiendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa hivi kama Wizara tayari tumeweke *task force* kuhakikisha hakuna atakayetumia maji yale kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji na shughuli nyingine yoyote isipokuwa kuelekeza maji katika mitambo yetu kwa ajili ya kuchakata kwenda kwenye matumizi ya kibinadamu.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine wa Wizara yetu ni kuona tutaendelea kutoa elimu ya kutosha, matumizi sahihi ya maji katika maeneo yote yenye mito tiririka ili vyanzo vyetu vya maji visiweze kuathirika kama ulivyosema. Tayari tumeshatumia fedha nyingi kujenga miundombinu ambayo Serikali inatarajia wananchi waweze kupata maji ya kutosha, safi na salama wakati wote. (*Makof!*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi; Mheshimiwa Mbunge wa Ulyankulu, Mheshimiwa Rehema Migilla.

Na. 22

**Ujenzi wa Barabara ya Ulyankulu – Uyui – Tabora
kwa Kiwango cha Lami**

MHE. REHEMA J. MIGILLA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Ulyankulu – Uyui hadi Tabora Manispaa kwa kiwango cha lami ikizingatiwa kuwa barabara hii ni muhimu kwa uchumi wa Wilaya hizo tatu?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara ya Ulyankulu – Uyui –Tabora yenyeye urefu wa kilometra 77 kwa wananchi wa Wilaya za Kaliua, Uyui na Manispaa ya Tabora ambapo kwa sasa inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na hatimae kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiendelea na juhudzi za kutafuta fedha ili kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami, Wizara yangu kupitia *TANROADS* inaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii ili iweze kupitika majira yote ya mwaka ambapo katika Mwaka wa Fedha 2021/22 kiasi cha shilingi billioni moja na milioni mia tano kimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Rehema.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu hayo ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, suala la barabara hii limekuwa sasa kama ni hadithi. Hata watangulizi wangu wamekuwa wakipigia kelele sana barabara hii lakini pamoja na umuhimu wake bado Serikali inatuletea hadithi ya kwamba inatafuta bajeti. Wananchi wamechoka na hii hadithi, wanataka wajue je, ni lini barabara hii sasa itawekwa kwa kiwango cha lami?

Swali la pili; kwa kuwa Serikali bado inaendelea kutafuta bajeti kwa hii barabara lakini barabara hii ni muhimu sana, inapitisha mizigo kutoka sehemu mbalimbali na inapitisha abiria na mambo mengine. Lakini barabara hii mpaka leo inatumika kama uchochoro kwa baadhi ya magari ambayo yanakwepa kupima uzito sehemu nyingine. Sasa je, Serikali ipo tayari kutujengea mzani ili barabara hii iweze kuwa katika ubora wake ule ule?

SPIKA: Hivi Tabora barabara za lami nyingi mlizonazo mnataka zote ziwe za lami jamani Wanyamwezi ninyi? Majibu ya swali hiyo Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rehema Migilla kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza siyo kweli kwamba hizi ni hadithi nimesema tu kwamba kwa niaba ya Serikali tunaendelea kutafuta fedha tufanye upembuzi yakinifu na usanifu wa kina tuweze kujua tunahitaji upana wa lami kiasi gani na uzito wa mizigo unaoweza kupita katika eneo hilo, madaraja, ili tupate makisio ya bajeti ili tuweze kutafuta fedha. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira katika wakati huo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ameomba mizani. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa wazo hili limepokelewa na litafanyiwa kazi na watapata majibu kwa wakati muafaka. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, na kwa niaba yake namuona Mheshimiwa Abdallah Chikota.

Na. 23

**Ujenzi wa Mnara wa Mawasiliano wa
Halotel – Chilangala Newala**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA K.n.y. MHE. MAIMUNA S.
MTANDA** aliuliza: -

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya ujenzi wa mnara wa mawasiliano wa *Halotel* katika Kata ya Chilangala ambapo mkataba ulisainiwa mwaka 2020 lakini mpaka Septemba, 2021 mradi huo haujaanza?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa *Eng. Andrea Kundo tafadhali.*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA
TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, Mbunge wa Newala Vijiji, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) katika zabuni ya awamu ya nne ya kufikisha mawasiliano maeneo ya vijiji, iliingia mkataba wa kufikisha huduma ya mawasiliano ya simu katika Kata 114 ikiwemo Kata ya Chilangala na Kampuni ya *Halotel*

(Viettel) mnamo tarehe 24 Januari 2020. Utekelezaji wa mkataba huo ilitakiwa kukamilika ndani ya miezi tisa yaani tarehe 23 Oktoba 2020. Lakini kutokana na changamoto ya UVIKO-19 utekelezaji wa mradi huo ulichelewa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi huo ulipelekea watoa huduma wengine kuboresha huduma za mawasiliano katika kata hiyo ambapo Kata ya Chilangala ina mawasiliano ya Mtandao wa Tigo ambao wana minara miwili katika Vijiji vya Chilangala na Namdimba. Hivyo basi, Serikali haitojenga mnara huo katika Kata ya Chilangala, na hivyo kuzielekeza fedha hizo katika maeneo mengine yenye changamoto zaidi za mawasiliano. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Chikota nimekuona.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza:

Mheshimiwa Spika, changamoto ya mawasiliano iliyopo Kata ya Chilangala inafanana na Kata za Kitaya, Mnongodi na Namtumbuka ambazo zipo mpakani na Msumbiji na ambako kama utakuwa unafahamu sasa hivi kuna changamoto ya kiusalama kule. Naomba mpango mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba Kata hizi kwa sasa zinakuwa na mawasiliano ya uhakika ili isaidie katika...

SPIKA: Zipo kwenye Wilaya gani hizi Kata.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Spika, zipo Wilaya za Mtwara Vijijini na Tandahimba ambazo zinapakana na jirani zetu wa Msumbiji. Kwa hiyo naomba mpango wa haraka wa Serikali wa kuhakikisha kwamba Kata hizi zote zinapata mawasiliano ya uhakika.

Swali langu la pili ni kwamba minara ambayo inajengwa vijijini sasa hivi ni kwa ajili ya mawasiliano ya sauti tu, kwa ajili ya *voice*, lakini kuna mahitaji makubwa ya *internet*

sasa hivi vijijini na hata llani yetu ya Chama Cha Mapinduzi inasema tunataka kuboresha upatikanaji wa *internet* vijijini. Sasa Serikali ina mpango gani wa kuboresha au ku-*upgrade* minara hii ili iweze kuhakikisha kwamba hata *data* zinapatikana vijijini?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Mhandisi Andrea Kundo.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitumie fursa hii kuwapongeza sana Wabunge wote wa Mtwara kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakitupatia tunapofika katika maeneo yao ya kazi. Maeneo haya ya Kitaya pamoja na maeneo mengine ya Lulindi, Tandahimba pamoja na Newala tulishafika na kupitia fedha ambayo Serikali ilipitishiwa hapa Bungeni tayari kuna miradi ambayo imepangwa kwenda kutekelezwa kupitia miradi ya mipakani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi kabisa, kwa sababu dhamira ya Serikali ni ileile ya kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanapata mawasiliano. Maeneo ya mipakani tunayaangalia kwa umuhimu wake kwa sababu ni masuala ya kiusalama.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile katika Kata ya Kitaya, Mbunge anafahamu, mimi na ye ye tulikwenda mpaka katika Kata ya Kitaya ambapo kuna mradi wetu ambao umeshakamilika na tayari umeshawashwa na huduma ya mawasiliano tayari imeshafika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala la uhitaji wa *internet* kwanza kabisa mpaka sasa Serikali inaboresha miundombinu ya Mkongo wa Taifa. Kwa upande wa Kusini mpaka sasa ukitoka pale Mangaka kwenda Mtambaswala takribani kilometra 72, tunajenga mkongo wa Taifa siku za hivi

karibuni mradi huo utakamilika. Hivyo basi, hata ile miradi sasa ambayo itakuwa inahitaji *data* maana yake ni kwamba Serikali imeshaelekeza watoa huduma wote wahakikishe miradi yote ambayo itajengwa kuanzia sasa iwe inatoa huduma ya *3G* na *4G* na kuendelea. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Bado tuko Wizara hiyo ya Habari, Mheshimiwa Mbunge wa Tumbatu, Mheshimiwa Juma Othman Hija.

Na. 24

Kuboresha Usikivu wa Redio ya Taifa (TBC) – Nchini

MHE. JUMA OTHMAN HIJA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha usikivu wa Radio ya Taifa (TBC) katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Zanzibar?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Habari.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiboresha usikivu wa *TBC* kwa kutenga fedha katika bajeti ya maendeleo kila mwaka ili kuyafikia maeneo yasiyo na usikivu wa *TBC* kwa nchi nzima yakiwemo maeneo ya Zanzibar. Miradi iliyotekelawa na *TBC* ni pamoja na kufunga mitambo ya kurushia matangazo ya redio katika Visiwa vya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, aidha, miradi ya upanuzi wa usikivu wa *TBC* inaendelea kutekelezwa katika Mikoa mipyaa ya

Songwe, Njombe na Simiyu. Vilevile upanuzi huo unaendelea kwa upande wa Visiwa vya Unguja na Pemba. Miradi hiyo inatarajiwaka kukamilika ifikapo Machi, 2022.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuiwezesha *TBC* ili maeneo yote nchini ambayo hayana usikivu yakamilike ifikapo mwaka 2025 kama ilivyoainishwa katika llani ya uchaguzi ya CCM (2020 – 2025) lbara ya 125 (f). Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Tumbatu nacho kisiwa pia. Mheshimiwa Mbunge wa Tumbatu, Mheshimiwa Hija.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri na ya kuridhisha ya Serikali, nina swali fupi la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza wigo wa usikivu nchini, *TBC* haioni kwamba kuna haja ya kuwasiliana na redio za kijamii ili kuziwezesha kujunga na *TBC* Taifa wakati wa matokeo makubwa kama vile taarifa ya habari na mengineyo? Ahsante. (*Makof*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juma Othman Hija kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba Shirika la Utangazaji *TBC* linafanya mahusiano mazuri na Shirika la Utangazaji la Zanzibar. Baada ya kukamilisha katika miradi yetu ya awali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, tuna mpango wa kuja kushirikisha na redio zingine ili pale ambapo Shirika la Utangazaji Tanzania linapokuwa na changamoto ya miundombinu basi iweze kushirikisha redio nyingine ambazo zitakuwa zinasaidiana. (*Makof*)

SPIKA: Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini.

Na. 25

Uzalishaji katika Kiwanda cha Viuadudu Kibaha

MHE. SYLVESTRY F. KOKA aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha kinazalisha *bio-larvicides* za kuangamiza viluilui vya mbu kama ilivyokusudiwa?

SPIKA: Majibu ya Serikali, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Exhaud Silaoneka.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Sylvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kiwanda cha viuadudu Kibaha, Tanzania *Biotech Products Limited* ni mali ya Serikali kwa asilimia 100. Kiwanda hiki kinao uwezo wa kuzalisha lita milioni sita za viuadudu vya kibaolojia (*bio-larvicides*) kwa mwaka vinavyotumika kuua viluilui wa mbu waenezao Malaria na aina nyinezo.

Mheshimiwa Spika, kiwanda kinaendelea kuzalisha viuadudu vya kibaolojia ambapo tangu kiwanda kilipoanza uzalishaji mwaka 2017 hadi mwezi Agosti, 2021 kimeweza kuzalisha jumla ya lita 700,286.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali kupitia Shirika letu la Maendeleo ya Taifa (*NDC*) ni kuhakikisha kiwanda hiki kinazalisha kwa ukamilifu wake (*full installed capacity*) kwa kutafuta masoko zaidi ya viuadudu ya ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Koka, swali la nyongeza.

MHE. SYLVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu. Kiwanda hiki cha kipekee Afrika na ambacho kina uwezo wa kuzalisha viuadudu vinavyoua masalia ya mbu na kuangamiza Ugonjwa wa Malaria katika nchi yetu na nchi mbalimbali Barani Afrika, kama ulivyomsikia Mheshimiwa Waziri ni miaka mitano toka kimeanzishwa lakini hakijazalisha hata asilimia mbili ya uwezo wake wa kuzalisha dawa hizo licha ya kuwa na uwezo vilevile wa kuzalisha mbolea pamoja na *vaccine* kwa ajili ya wanyama.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha, ukienda kwenye kiwanda hicho sasa hivi ni kama mahame, hakifanyi kazi. Wafanyakazi wa kiwanda hiki walikaa hadi miezi mitano hawajalipwa mishahara, hata mafao yao hayajawasilishwa katika mashirika yetu ya hifadhi ya Jamii hadi leo ninavyozungumza.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama, alifika pale kujiona *saga* hili katika kiwanda hiki cha Serikali. Serikali imejikita kuagiza madawa kwa gharama kubwa kutibu malaria badala ya kusaidia kiwanda hiki kununua hizi katika kila Mkoa na Wilaya ili kuangamiza mbu. Tumejikita kutibu malaria badala ya kuzuia malaria na uwezo tunao, hili ni jambo la aibu!

SPIKA: Mheshimiwa Koka sasa swali!

MHE. SILYVESTRY F. KOKA: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza ni lini Serikali kuititia Wizara ya Afya wataagiza dawa hizi, kiwanda kifanye kazi ili tuangamize malaria katika nchi yetu? (*Makofi*)

Swali la pili; ni lini wafanyakazi hawa wanaopigwa danadana wengine wameajiriwa *NDC* na wengine wameajiriwa na kiwanda watakuwa wakilipwa mishahara yao na makato yao kufikishwa sehemu husika?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Hapa ndipo Bunge huwa linagawanyika, maana majibu ya Waziri tofauti, *observation* za Mbunge tofauti kabisa. Mheshimiwa Naibu Waziri ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Kibaha Mjini, Slyvestry F. Koka kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme wazi kuwa si kweli kwamba kiwanda kile ni magofu kama alivyosema. Kiwanda kile kinafanya kazi na...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, mahame.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, magofu au mahame, kinafanya kazi...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: ... ambapo sasa hivi...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Basi sasa Waheshimiwa Wabunge, swalii hili tulivuke kwa sababu ninayo maombi ya Kamati yangu ya Viwanda na Biashara tayari mezani ya kutembelea kiwanda hiki. Kwa hiyo, Waziri na Kamati yangu watakwenda huko, wakitoka huko watatuletea lipi ni lipi. Ahsante sana. (*Makof/ Kicheko*)

Lakini, *Observation* moja ni kwamba, Mheshimiwa Ummy hayupo, Mheshimiwa Dugange mpo hapa, aah yupo kumbe. Moja ya sababu ambazo nilikuwa nimeelezwa mapema ni kwamba TAMISEMI kuititia halmashauri zote walikuwa wamewekeana mkataba huko mwanzo wa kununua hizi dawa za viua mbu hizi. Sasa halmashauri hazinunui zile dawa, kwa hiyo nao wanasabisha *incapacitation* ya kiwanda. Kwa hiyo, Kamati itafanya kazi

halafu tutaona namna gani ya kusaidia kiwanda hiki Muhimu. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, tunaelekeea Katiba na Sheria, Mheshimiwa Husna!

Na. 26

Mpango wa Kumsaidia Mjane Katika Masuala ya Mirathi

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO aliuliza:

Wanawake na Watoto wanapata shida Baba wa familia anapofariki; pamoja na Sheria ya Mirathi;

Je Serikali ina mpango gani zaidi wa kumsaidia mjane katika masuala ya mirathi.

SPIKA: Majibu ya Serikali, Mheshimiwa Naibu Waziri Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi anavyofuatilia na kusemea kwa nguvu kuhusu dhuluma wanazofanyiwa wanawake na watoto mara baada ya baba wa familia kufariki.

Mheshimiwa Spika, sheria zinazohusiana na mirathi, zinatamka wazi kuwa wanufaika wa mirathi ni mke wa marehemu, watoto wa marehemu na wazazi wa marehemu. Vilevile inaelekeza kuwa msimamizi wa mirathi si mrithi wa mali za marehemu labda atokane na makundi tuliyoyataja hapo juu. Uteuzi wa msimamizi wa mirathi hufanywa na kikao cha familia na baadaye kuthibitishwa na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kwa vitendo vyaa dhuluma, udhalilishaji wa familia ya marehemu akiwemo mke

na watoto, Serikali imeanza kupitia upya Sheria ya Usimamizi wa Mirathi hiyo katika kubaini mapungufu ili iweze kurekeblishwa. Kwa kuwa mchakato huo uhusisha taasisi za dini, mchakato umeanza wa kukutana nao na pia kukutana na viongozi wa makabila mbalimbali ili kupitia mila zao ambazo nyingi ni za udhalilishaji.

Mheshimiwa Spika, ikibainika kutokea vitendo vyatuhuluma kwa wanafamilia waliopoteza baba wa familia inaelekezwa kwenda Mahakamani kutafuta haki zao. Nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge kutoa ushirikiano wa familia hizo ambazo nyingi hazina uelewa mkubwa wa masuala ya kisheria kufikia ili huduma hii na waweze kupata haki zao. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Husna Sekiboko.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Spika nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nishukuru kwa majibu hayo lakini naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa msimamizi wa miradhi kwa mujibu wa sheria ya sasa anachaguliwa kwenye kikao cha familia ya marehemu ambacho katika kikao hicho mjane anakuwa ni mgeni, wengi wanakuwa ni ndugu wa marehemu, na hivyo anakosa kauli ya kuweza kuchagua au kupitisha mrithi au msimamizi wa mirathi hali inayopelekea familia kwa maana ya mjane na watoto kutaabika pale ambapo aliyechaguliwa kujimilikisha mali hizo. Je, ni lini sasa Serikali inatuletea marekebishi ya sheria hii ili tuweze kuondoa changamoto hizi?

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na sheria ambayo inakwenda kurekebishiwa, je, Wizara inachukua hatua gani za dharula ili kuondoa hizi changamoto kwa sababu tunajua mchakato wa kurekebisha sheria inaweza kuchukua muda kidogo? (*Makof*)

SPIKA: Swali hili muhimu sana sana sana, muhimu sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, nipende kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Husna kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa inatokea wakati wa vikao vile vya familia za marehemu wajane hawa wamekuwa hawahusishwi kwa asilimia 100 katika kufika muafaka wa kupata yule Msimamizi wa Mirathi. Lakini kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi, ni kwamba msimamizi wa mirathi, si mrithi wa mali za marehemu. Na kwa bahati mbaya sana, kwa kuwa sheria hii ya mirathi ina sura tatu yaani kuna sheria ambayo inaruhusu mfumo wa kidini katika kugawa mali, kuna kimila na kuna sheria ile ya Serikali; kumekuwa na mkanganyika mkubwa na ndiyo maana Serikali sasa kwa makusudi kabisa tumeamua kuzipitia hizi taratibu zinazosimamia mgao wa mirathi ili kuondoa huu mkanganyiko ambao kwa sasa unakabili familia nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, lakini ni hatua gani za dharula ambazo tunazichukua, kwa sasa tunaendelea kila tunapopata nafasi ya kwenda katika maeneo mbalimbali ya nchi kuelekeza na kutoa elimu kwa wahusika wote. Kwamba ni muhimu wakatambua kuwa wasimamizi wa mirathi si warithi wa mali za marehemu, labda atokane na wale wanaotajwa kwenye orodha ya mirathi, na ye ye anaingia kwenye ule mgao wa kawaida wa mali za marehemu. Lakini vinginevyo tumekuwa na tafsiri ambayo asili yake inatokana na mfumo wa kikabilna mila na desturi zao; yaani mtu akishaambiwa ye ye ni msimamizi wa mirathi anajimilikisha haki zote za usimamizi wa mirathi na kuanza kutumia mali za marehemu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwaomba na Waheshimiwa Wabunge po pote mtakapokwenda kuendelea kuelimisha, wakati sheria inakuja kuendelea kuelimisha juu ya nafasi ya msimamizi wa mirathi. Na

inapobainika, kwamba, msimamizi wa mirathi ametumia kula mali ya marehemu kinyume cha utaratibu afikishwe kwenye vyombo vyaa sheria na hatua zichukue mkondo wake. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Hili ni tatizo kubwa. Mheshimiwa Neema nilikuona, haraka haraka.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, kwa kuwa matatizo na changamoto ambazo wanapitia wanawake kwenye masuala haya ya kifamilia yamezidi kukithiri, na tarehe 6 Oktoba, 2021 Mheshimiwa Rais alilikazia hili, na hata Jaji Mkuu alielezea umuhimu wa kuwa na Mahakama ya Familia. Ningependa kuiuliza Serikali kuititia Wizara ya Katiba na Sheria. Je, ni lini ambapo itakuja na Mahakama ya Familia ili masuala yote haya ya mirathi matunzo na kadhalika yaweze kuangaliwa kwa utaratibu na haki iweze kutolewa? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Katiba na Sheria, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa mapendekezo mbalimbali yalitolewa kwa ajili ya kuanzisha Mahakama ya Familia, na bado tunaendelea kufanya kazi, kwa sababu ni taasisi ambayo inahitaji kuwa kwenye muundo sasa wa utendaji kama zilivyo Mahakama nyingine. Kwa hiyo, ni imani yangu kwa kuwa tunakwenda sasa katika kurekebisha sheria yenye na muundo wake tunadhani tutakapokuwa tunakuja tutakuja na sura sasa ya kuwa na mahakama hii ambayo itashughulikia masuala ya mirathi. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Tunaomba Serikali mliangalie jambo la Sheria hii ya Mirathi ili ikiwezekana nayo tuweze kuitendea haki, maana ni taabu. Yupo mama mmoja mume wake ni mmoja wa matajiri wakubwa hapa Dodoma alifariki mwaka mmoja miwili iliyopita, lakini mke wake anaauza uji kwenye stendi za mabasi hapa, kwa sababu alikuwa na watoto wadogo kwa hiyo hivyo vikao vyaa familia wamejali hao wengine,

wamegawana na wanafanya ubabe. Yaani *you can't believe*. Kwa hiyo ni sheria peke ambayo inaweza ikasaidia akina mama wa namna hii.

Anaangalia mali waliyochuma na mume wake hivi hivi, yaani *she is nowhere* kabisa, inatia huruma kwelikweli unaweza ukatoa machozi kabisa.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Jumanne Abdalla Sagini, Mbunge wa Butiama tafadhalii.

Na. 27

**Ujenzi wa Chuo Kikuu cha Teknolojia na Kilimo cha
Mwalimu Nyerere -Butiama**

MHE. JUMANNE A. SAGINI aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza rasmi ujenzi wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Teknolojia na Kilimo, Butiama.

SPIKA: Majibu wa swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri nimkuona elimu, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini Mbunge wa Butiama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza mchakato wa kukijenga Chuo Kikuu cha Teknolojia ya Kilimo cha Mwalimu Nyerere, Kampasi ya Butiama. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imetenga Dola za Kimarekani Millioni 44.5, sawa na Shilingi za Kitanzania Bilioni 103 kupitia mradi wa Mageuzi ya Kiuchumi kwa ajili ya Elimu ya Juu uitwao *Higher Education for Economic Transformation-HEET*. Mradi wa HEET

unatekelezwa kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikishirikiana na Benki ya Dunia kuanzia mwaka huu 2021 mwezi Septemba.

Mheshimiwa Spika, yapo baadhi ya maandalizi muhimu yaliyokamilika ambayo ni pamoja na: kupatikana kwa hati miliki ya eneo lenye ukubwa wa ekari 573.5; uandaaji wa mpango kabambe (*master plan*); tathmini ya athari ya mazingira (*Environmental and Social Impact Assessment*); na usanifu wa majengo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa taratibu zinazofuata ni kumtafuta mshauri mwelekezi, na atakapopatikana atafanya kazi ya mapitio ya michoro na kuandaa hadidu za rejea na makabrasha ya zabuni ili kutangaza na kumpata mkandarasi. Michakato hiyo itakapokamilika ujenzi huo utaanza rasmi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Jumanne Sagini nilikuona.

MHE. JUMANNE A. SAGINI Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, kwa kweli yanaleta matumaini. Hofu yangu ni moja tu, kwamba hizi lugha za mchakato, mchakato wakati mwingine unaweza ikachukua muda mrefu. Wakati nachangia hotuba ya bajeti ya Wizara hii, waliniyahidi kwamba mwaka wa fedha utakapoanza utaanza harakati za ujenzi. Lakini hadi leo wanazungumzia mchakato, sasa hebu atuhakikishie hii michakato ya *ku-procure* huyo *consultant* ili afanye *review* ya hizi *design* zitakamilika lini na ujenzi uweze kuanza? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Mbunge wa Butiama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika kama nilivyoeleza kwenye jawabu la msingi kwamba taratibu zote sasa zimekamilika; na upatikanaji huu wa fedha kama nilivyozungumza kwamba umeanza mwezi wa Septemba. Tunatarajia kama mambo yote yatakwenda vizuri mpaka kufika mwezi wa Februari shughuli za ujenzi katika eneo hili inawezekana zikawa zimeanza rasmi. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana, bado tupo elimu, Mheshimiwa Mbunge wa Singida Mjini, Mheshimiwa Mussa Sima.

Na. 28

Somo la Kilimo Kuwa la Lazima

MHE. MUSSA R. SIMA aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kulifanya somo la kilimo kuwa la lazima kuanzia ngazi ya elimu msingi mpaka chuo kikuu kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi.

SPIKA: Majibu ya swali hilo bado tupo kwako, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu na mchango mkubwa wa Kilimo katika maendeleo ya familia na taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, somo la kilimo linafundishwa katika ngazi zote za elimu hapa nchini. Kwa mfano, katika ngazi ya mtaala wa ngazi ya elimu ya msingi maarifa na stadi za kilimo zinafundishwa katika somo la stadi za kazi. Kwa upande wa

Sekondari, somo la kilimo ni somo chaguzi na linasomwa na wanafunzi kuanzia kidato cha Kwanza hadi cha Sita.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia inahuisha miongozo ya eimu ya kujitegemea kuanzia shule za msingi hadi vyuo vya ualimu. Miongozo hiyo imelenga kuziwezesha shule na vyuo vya ualimu kuanzisha na kusimamia kwa ufanisi miradi ya uzalishaji mali ikiwemo shughuli za kilimo na biashara. Elimu hiyo itamsaidia mwanafunzi kujifunza kwa vitendo stadi mbalimbala za maisha ikiwa ni pamoja na kilimo kwa lengo la kuwajengea misingi imara ya kujitegemea na kujajiri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa Wizara kuitia Taasisi ya Elimu Tanzania inafanya mapitio ya mitaala ya ngazi zote za elimu msingi, suala hili litajadiliwa na kufanyiwa maamuzi stahiki. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Sima nimekuona, Mbunge wa Singida Mjini.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Taifa letu la Tanzania linatambulika kabisa kwamba kilimo ni uti wa mgogo, na tangu uhuru tunatambulika kwamba taifa hili ni taifa la wakulima na wafanyakazi. Serikali imesema somo hili linafundishwa kwenye somo la maarifa ya jamii na stadi za kazi. Kimsingi ni mada wala si somo la kilimo ni mada zinafundishwa huko.

Mheshimiwa Spika, swali langu, swali langu, ni lini sasa...

SPIKA: Anayeuliza maswali haya ni mwalimu jamani enhee Endelea Mheshimiwa.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Spika, swali langu, ni lini sasa Serikali itaweka kipaumbele kuhakikisha kwamba somo hili la kilimo linafundishwa na linakuwa la lazima, kwa maana *compulsory* dhidi ya masomo mengine kama *general*

study, develop and study ambayo kimsingi tija yake ni ndogo ukilinganisha na tija hii ya somo la kilimo? Serikali inasema ukienda sekondari unachagua maana yake ni option, sasa una opt nini ilhali kwenye msingi hujatengeneza somo?

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali, ikubaliane na mawazo haya kuhakikisha kwamba inalianzisha somo hili la kilimo kuanzia ngazi ya msingi mpaka chuo kikuu?

Mheshimiwa Spika, lakini swalilangu la pili, Serikali imeanza mchakato wa mabadiliko ya mtaala wa elimu, na nichukue fursa hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Samia Suluhu alipoamua kwa dhati na kusema kuna haja kufanya mabadiliko ya mtaala wa elimu. Sasa swalilangu hapa, ni lini Serikali itatuletea mchakato huu hapa Bungeni ili sisi tukachakata na kuhakakisha kwamba tunakuwa mstari wa mbele kuhakikisha elimu yetu hii tunaiwekea msingi ulio bora ili watoto wetu waweze kujajiri na kuajiriwa kupitia na ujuzi huo? Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Prof. Ndalichako, Waziri wa Elimu, majibu tafadhali.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, Ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kujibu muhimu kabisa la mwalimu mwenzangu, Mwalimu Sima. Kwa kweli maswali aliyouliza ni ya msingi. Tunatambua kwamba asilimia kubwa ya wananchi wetu ni wakulima. Kwa sasa hivi, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri wangu, somo la kilimo liko kwenye sekondari kama *options* na kwa upande wa shule za msingi tunafanya stadi za kazi; na tunafanya mapitio ya mitaala.

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu umetuwekea semina, lakini kabla hujatutangazie ile *briefing* mimi nilikuwa nimepanga tarehe 6 Novemba, 2021 nifanye semina, ingawa nilikuwa sikupanga kwa Bunge lote lakini nilikuwa nimepanga nifanye na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, niwapitishe mpaka sasa hivi Serikali

imefikia wapi kwenye mapitio ya mitaala, wadau wanasesma kitu gani na uchaguzi wa Wizara ni nini kutokana na maoni ya wadau na mwelekeo wa Serikali kutokana na maoni ya wadau ni nini, ili sasa Waheshimiwa Wabunge wapate nafasi ya kuweza kuweka maoni yao wakati tayari maoni ya wananchi wao tumeshayaweka Pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, labda niahidi tu kwamba hili nitalifanya kazi kiutawala kuangalia kwamba tarehe 6 ambayo nilikuwa nafikiria kuwa na semina na Waheshimiwa Wabunge tayari Mheshimiwa Wangu Spika kiongozi wetu umeishaichukua hiyo tarehe kwa hiyo tutaangalia utaratibu. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana. Tutawasiliana na Waziri wa Nchi kuhusu jambo lako muhimu hilo totalitafutia *slot* mahali katika kipindi hiki cha Bunge, ili Kamati hiyo iweze kupata hli dozi. Tutawasiliana na Waziri wa Nchi na tutaelewana tu kuhusu muda. Tutawasiliana baadaye kuhusu pendekezo la Mheshimiwa Waziri wa Elimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Nusrat nilikuona.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusiana na hatua mbalimbali ambazo, tayari wameshaanza kuzichukua kwa kuona umuhimu wa kufanya mapitio ya mitaala yetu ya elimu.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nikufahamu kwa sababu kimsingi wameshafanya makongamano kadhaa ya wadau na marafiki wa elimu kwa ajili ya kukusanya maoni. Lakini wamepitia elimu ya awali, msingi na sekondari kimsingi vyuo na vyuo vikuu bado. Kwa hiyo, niulize sasa Wizara ama Serikali ina mpango gani wa kutuletea pia kufanya mapitio ya kozi ambazo zinatolewa kwenye vyuo vyetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, kuna maoni ya watanzania wametoa mbalimbali kuna masuala ya kilimo, kuna masuala ya ujasiriamali pamoja na stadi za kimaisha

na mambo mengine mengi yote yamejadiliwa. Lakini vyuo na vyuo vikuu ambavyo ndio kimsingi vinatoa watu ambaa ndio watenda kazi kwenye nchi. Ni lini sasa Serikali italeta kufanya marekebisho pia ya mtaala na masuala ya kozi ambazo zinatolewa kwenye vyuo hivyo. Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Alaa! Kumbe mnashughulika na... sisi tulifikiri elimu kwa ujumla kumbe Mheshimiwa Profesa, mko na kipande kidogo tu cha *primary* na sekondari pekeyake? Majibu tafadhalii Mheshimiwa Profesa. (*Makofii*)

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nitoe ufafanuzi na kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Hanje. Utaratibu wa vyuo vya katilini na vyuo vya elimu ya juu wana taratibu zao za kuanzisha mitaala.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika vyuo vikuu seneti ndio chombo kikuu ambacho kina mamlaka ya kuangalia mitaala katika vyuo vikuu na vyuo vya katilini vina nyanja tofauti, vyuo vya kilimo viko chini ya Wizara ya Kilimo, vyuo vya utalii viko chini ya Wizara ya Utalii, vyuo vya afya viko chini ya Wizara ya Afya na wote wana taratibu zao. Wizara husika ndio zinakuwa na mabaraza kwa mfano Wizara ya Afya, Baraza la Madaktari ndio linaangalia mitaala ya madaktari, Baraza la Wauguzi linaangalia mitaala ya manesi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kiasi fulani hili jambo labda nilipokee kama Serikali tuangalie namna ya kuliratibu. Kwa sababu, kwa sasa hivi sio vyuo vyote vya katilini vinasimamiwa moja kwa moja na Wizara ya Elimu na wala Wizara haihusiki moja kwa moja na kuidhinisha mitaala. Ila imekasimisha mamlaka kwa seneti za vyuo vikuu pamoja na vyombo ambavyo vimewekwa, kwa mujibu wa sheria katika vyuo husika kushughulika na mitaala.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu tuangalie namna gani labda kwa kuongezea kabla sijamalizia. Ni kwamba nako pia tumeelekeza wafanye mapitio ya mitaala na katika huu Mradi wa *Higher Education* tuna fedha ambazo

tumetenga, kwa ajili ya kufanya mapitio makubwa na ndio maana mradi unaitwa mageuzi ya kiuchumi na yanajikita katika kuimarisha uchumi wa viwanda. Kwa hiyo, mapitio ya mitaala yanafanyika kwa hiyo tutaangalia utaratibu mzuri wa kuratibu tupate mapitio yanayofanyika. Ili tuweze kuja kutoa taarifa kwenye chombo muhimu, ambacho ndio kinasimamia sheria na kusimamia utendaji wa shughuli za Serikali. Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Profesa kusema ukweli tumekuwa *disappointed*. Kwa sababu, wewe ndio Waziri wa Elimu na watanzania wanalamikia mfumo wa elimu ulivyo. Wanataka tujadiliane mfumo uweje sasa kama kuna wengine tena seneti ndio wenyе mamlaka, sisi tunataka elimu ya Tanzania. Tuitazame tuone, na wewe ndio mtu wetu sisi Waziri wa Elimu. Kwa hiyo, hao sijui iko Wizara gani, Wizara gani sisi kama wananchi haituhusu. Sisi tunachotaka tuchangle tuseme tunataka nini kwenye elimu. (*Makofi*)

Halafu ninyi wataalam sasa ndio mtajua kama hili la seneti mtaagiza kwenye seneti, yaani lile la ndani ya Serikali lile halina shida ni la kwenu, lakini namna ya kupata maoni ya watanzania wanatakaje mambo yao yakae katika upande wa elimu na wanasema hivyo kwa sababu, hizo seneti zimeshashindwa vinginevyo pasingekuwa na malalamiko. (*Makofi*)

Kwa hiyo, sio mbaya kwamba tumeanza na hizi *primary* na nini lakini iko haja ya kufungua mjadala wa elimu kwa ujumla wake. Ndivyo ninavyosoma na ndio maana Wabunge wamekuwa wakisema tushirikishwe hatujasema tushirikishwe *primary* na sekondari peke yake hapana. (*Makofi*)

Tushirikishwe mfumo wa elimu katika nchi yetu ilivyo. Kwa hiyo, kaliangalieni vizuri. Tena elimu ile ya chuo kikuu na nini ndio watu wanalamikia kweli kweli kuliko hata ya huko chini. Ahsante sana, basi mliangalie vizuri ndani ya Serikali namna gani ya kushirikishana ili tuweze kuvuka. Mheshimiwa Rais Mkapa wakati wake alisisitiza sana hili, Mheshimiwa

Jakaya Kikwete amesitisitiza sana hili na watu wengi sana wamezungumza habari hii tujadiliane kuhusu elimu yetu. Sasa wasibakie wengine waseme sisi seneti ndio tuna mamlaka, elimu yote ile tupate nafasi ya kuzungumza. (*Makofi*)

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Nkasi Kusini leo watu wa Nkasi ni maswali tu leo.

Na. 29

Ukosefu wa Masoko ya Samaki Ukanda wa Ziwa Tanganyika

MHE. VINCENT P. MBOGO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga masoko ya samaki katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika hususani Kata ya Kala Mpasa, Wampambe, Kizimbi na Naninde ili wavuvi wapate maeneo ya kuuzia samaki badala ya kulazimika kwenda kuuza nchi za jirani za Zambia, Congo na Burundi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Abdalah Hamis Ulega, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kujenga miundombinu ya uvuvi katika maeneo mbalimbali ikiwemo katika mwambao wa Ziwa Tanganyika. Miundombinu ya Mialo na Masoko ni muhimu katika kuhakikisha kuwa na mazao bora na salama, kupunguza upotevu wa mazao na kusaidia ukusanyaji wa taarifa na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu huu, ujenzi wa masoko unahitaji rasilimali ikiwemo ardhi na fedha.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali ipo tayari kujenga Soko, katika Wilaya ya Nkasi kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi kuandaa eneo katika Wilaya ya Nkasi, ili kuwezesha hatua za ujenzi wa soko kuanza pindi fedha itakapopatikana. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mbogo una swali la nyongeza?

MHE. VINCENT P. MBOGO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Uchumi wa *blue unafanana* na mazingira mazuri kabisa sawa sawa na Ziwa Tanganyika. Je, Serikali ina mpango gani kama inavyofanya kwenye mazingira ya Bahari ya Hindi rasilimali zinavyopatikana baharini, vivyo hivyo na rasilimali zinapatikana Ziwa Tanganyika. Ni lini Serikali mnakuja na mkakati maalum swali namba moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali namba mbili dagaa Ziwa Tanganyika ni zao la kipekee ambalo ndio linasababisha uchumi wa Mikoa mitatu Kigoma, Rukwa na Tanganyika. Serikali ina mpango gani na zao hili na pia kwa sababu linavuliwa ndani ya Mikoa mitatu, libadilishwe jina sio dagaa wa Kigoma waitwe dagaa wa Ziwa Tanganyika ili kuweza kutangaza Ziwa Tanganyika? Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvusi, Mheshimiwa Abdalah Ulega, dagaa wa Ziwa Tanganyika sio dagaa wa Kigoma. Majibu unasemaje Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua kwanza fursa hii, kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbogo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza naomba kwa namna ya kipekee nimpongeze ye ye na Wabunge wote wa Mkoa wa Kigoma, Katavi na Rukwa kwa kuona umuhimu wa Ziwa Tanganyika na mazao yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Rais Samia Suluhu Hassan, moja ya mkakati ni hili la uchumi wa *blue* na ni kipaumbele kama Taifa letu na ndio maana katika bajeti ya mwaka huu, Serikali ya Awamu ya Sita imeweka jumla ya kiasi cha shilingi milioni 800. Kwa kusudio la kwanza ni kuhakikisha kwamba tunafanya *stock assessment*. Ziwa Tanganyika halijawahi kufanyiwa *stock assessment* kwa mara ya kwanza sasa tunakwenda kufanya *stock assessment*, ya kujua ni kiasi gani cha Samaki migebunga na dagaa tulionao katika eneo lile. Hii itatusaidia sana kwenye mkakati wa uchumi wa *blue*, ili kuweza kuvutia uwekezaji na watu kuweza kujua kwamba akiweka fedha yake itakwenda kumlipa kwa kiasi gani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini hili la pili la ushauri la kwa nini dagaa hawa wasiitwe dagaa wa Ziwa Tanganyika? Nataka nimhakikishie yeye na Waheshimiwa Wabunge wote tumeuchukua ushauri huu. Isipokuwa kibiashara wewe unafahamu ya kwamba katika *marketing strategy* dagaa hili limetambulika kwa miaka mingi sana kama dagaa la Kigoma.

Kwa hiyo, ikiwapendeza sisi tutakaa nao tutashauriana nao badala ya kuwa dagaa la Kigoma, tutasema kwamba liitwe dagaa la Tanganyika. Kwa dhumuni jema lile la kwamba wanavuliwa kwenye Mikoa yote mitatu, Rukwa, Katavi na Kigoma kwenyewe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, na dagaa hizi ni mali sana hazijawahi kushuka bei hivi sasa inauzwa mpaka shilingi 30,000 kwa kilo na hajjawahi kushuka chini ya shilingi 20,000. Ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa sio linauzwa, inauzwa. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Kicheko*)

SPIKA: Unasahihishwa na mgogo sasa. Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza. (*Makof!*)

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Ziwa Tanganyika linatumika zaidi ya nchi moja kwa maana ya Tanzania kuna Congo, Burundi na nchi nyingine. Lakini dagaa wengi wanapatikana Ziwa Tanganyika upande wa Tanzania na sheria ambazo mlizitunga pamoja na Kanuni, *zinawa-guide* wavuvi wa Tanzania wavue usiku wakati dagaa wengi wanapatikana mchana. Kwa hiyo, ni muda muafaka sasa wa Wizara ya Uvubi hawaoni kwamba, kuendelea kutumia hizo sheria ambazo zinawakandamiza wavuvi wa Tanzania na kuwapa faida nchi nyingine waachane nazo? (*Makofii*)

SPIKA: Kwa hiyo, kule Congo na wapi wanavua mchana?

MHE. AIDA J. KHENANI: Ndio wanavua mchana.

SPIKA: Sisi tunaambiwa tuvve usiku. Mheshimiwa Naibu Waziri swali zito hilo majibu tafadhali. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumepokea malalamiko na tumepokea mapendekezo ya wavuvi wote wa Ziwa Tanganyika na hivi sasa, Wizara inafanya kazi mapendekezo haya yote yaliyotolewa na wavuvi. Lakini naomba kwa ruhusa yako kwa sekunde moja. Dagaa ni aina tofauti katika mionganii mwa aina za samaki tulizonazo, mle katika Ziwa Tanganyika tunao dagaa, tunao migebuka. Lakini Ziwa Tanganyika ni maarufu zaidi kwa samaki wa marembo wanaouzwa duniani kote na tunapata mapato makubwa sana kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa nini usiku? Tunaweka sayansi inayoelekeza tunapovua usiku dagaa tunaweka *light attraction*, ni dagaa pekeyake ndiye anayeweza kuvutwa na mwanga wa taa. Migebuka havutwi, samaki wa marembo havutwi, sangara havutwi anayevutwa ni dagaa pekeyake.

Sasa, tunafanya vile kuwavuta dagaa ambao wanakuja katika mtindo wa makundi kwa maana *sculling*, ili kuwaepusha kuchukua samaki wa aina nyingine. Sasa hawa wanaovua mchana, nina hakika siwezi kuzungumzia nchi zingine, lakini hapo nimezungumza *from scientific point of view*.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini msingi wa kwa nini tunasema usiku na dagaa asivuliwe mchana, ukimvua mchana utavua na migebuka, utavua na samaki wengine wasiohitajika. Kwa sababu, kila leseni anayopewa mvuvi anapewa kwa kusudio maalum. Lakini hiyo tumeichukua hoja hii na sisi kama wataalam tupo katika harakati za kuangalia, ili tuweze kuendana na mahitaji ya wavuvi wetu waweze kunufaika na rasilimali hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Salma Kikwete, swali la mwisho.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote naomba niipongeze Serikali na Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kutupatia vifaa boti katika Jimbo letu la Mchinga. Sambamba na kutupatia mashine katika Jimbo letu la Mchinga na sasa hivi wako kwenye mchakato wa kutupatia hiyo boti. Halikadhalika wako kwenye mchakato mwingine wa kutujengea eneo ambalo wavuvi hawa wadogo wadogo hasa katika Jimbo langu la Mchinga, watajenga mwalo ili wavuvi wote wawe na sehemu ya uhakika ya kuuzia bidhaa zao kutoka kwenye Bahari yetu ya Hindi. Swali langu ni hili lifuatalo: - (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi huu wa mwalo katika Jimbo langu la Mchinga na hasa Kata ya Mchinga? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Abdallah Ulega, umachingani huko lini unajenga mwalo huko?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa

Mama yangu Salma Rashid Kikwete, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana ni ukweli kwamba Serikali ya Awamu ya Sita ya Rais Samia Suluhu Hassan imepeleka mashine za kutosha. Lakini vile vile na Kamba ambazo zilikuwa ni maombi ya kwake yeche mwenyewe Mbunge wa Jimbo la Mchinga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, na katika hilo pia vile vile Serikali ya Awamu ya Sita imetenga jumla ya shilingi milioni 800, kwa ajili ya kujenga Mwalo na sasa hivi tupo katika hatua tayari kwa pamoja kwa kushirikiana na wananchi wa Mchinga, tumeshachagua eneo litakalokwenda kujengwa ule mwalo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini sasa tupo katika michoro na baadaye kupata *BOQ* ambapo jumla ya kiasi cha fedha kisichopungua Shilingi milioni 800 zimetengwa kufanya kazi hiyo. Ninaamini kazi hiyo itakapokamiliika ndani ya mwaka huu wa fedha itawanufaisha wavuvi wa eneo hili la Mchinga na wengine katika Pwani ya Bahari ya Hindi. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo linakwenda Wizara ya Madini. Mheshimiwa Mbunge wa Iramba Mashariki Mheshimiwa Francis Isack Mttinga.

Na. 30

**Serikali kusimamia ulipaji fidia kwa wachimbaji
wadogo wa Kata ya Tumuli**

MHE. FRANCIS I. MTINGA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itasimamia ulipaji fidia kwa Wachimbaji Wadogo wa Kata ya Tumuli?

SPIKA: Mheshimiwa Prof. Shukrani Manya nimekuona, majibu ya swali hilo tafadhali Naibu Waziri Madini.

NAIBU WAZIRI WA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kukusu usimamizi wa Serikali juu ya fidia kwa wachimbaji wadogo wa Kata ya Tumuli, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, jitihada za pamoja baina ya Wizara na ufuatilaji wa karibu sana wa Mheshimiwa Mbunge, mnamo tarehe 9 Agosti, 2021, malipo ya fidia ya shilingi 90,000,000.00 yalilipwa kwa wachimbaji wote 90 wa Kata ya Tumuli na malipo haya yalifanyika chini ya usimamizi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkalama ili kupisha uwekezaji wa Kampuni ya *PUBO Mining Limited*. Ninakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mtinga.

MHE. FRANCIS I. MTINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza niishukuru Serikali ya Mama Samia kupitia Wizara hii, baada ya kilio cha muda mrefu hatimaye wananchi wangu wa Tumuli walilipwa fedha hizo. Pamoja na shukurani hizo naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mazingira ya wafanyakazi wetu wadogo wa Tumuli, ambao walihamishwa pale katika lile eneo na kwenda kuanzisha maeneo mengine hasa kwa kupelekewa umeme na barabara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili Serikali ina mpango gani pia kwa kuwasaidia hao wachimbaji wadogo vifaa vya uchimbaji kwa mkopo nafuu haswa hao wa Tumuli, Langida na Ibaga ambao ni wachimbaji wadogo wanaokuza uchumi katika nchi yetu. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Profesa Shukrani Manya, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Isack Mttinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wachimbaji hawa wadogo wa Kata ya Tumuli wanapaswa kuingia katika vikundi, ili watakapokuwa wamekuwa katika vikundi halafu waweze kujisajili na wakishakuwa wamesajiliwa wakatambulika rasmi kama kikundi kilichosajiliwa, basi baada ya hapo taratibu za kuwawekea mazingira bora zinaweza zikaanza ikiwa ni pamoja na kuwapa leseni.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba panapokuwa na uchimbaji wenyе tija katika maeneo ya wachimbaji wadogo, tunawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Nishati. Kwamba, kama machimbo hayo yana tija basi waweze pia kupelekewa nishati ya umeme kama ambavyo tumefanya katika machimbo baadhi ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, na hili suala la vifaa kwa ajili ya wachimbaji wadogo tumekuwa siku za karibuni tukiwasiliana na mabenki yetu ya ndani, kuona kwamba yanaweza yakaanza kukopesha vifaa kuliko hata fedha zenyewe na katika suala hili pia tumefikia mahali pazuri na hivyo nimpe tu tija Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaenda tena kuwaona wachimbaji wake kama *wameji-organize* katika vikundi tutawasajili na baada ya hapo, tutawaunganisha na mabenki yetu ili kwamba waweze kusaidiwa kama ambavyo wengine pia wanasaidiwa hapa nchini. Ninakushukuru sana. (*Makofij*)

SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekamilika na maswali yetu yamekwisha yote. Nawashukuruni sana kwa ushirikiano, sasa tuendelee.

Tunao wageni kwenye Jukwaa la Spika, wageni hawa ni kutoka Tume ya Utumishi ya Bunge la Nigeria. Ni wageni wetu na wametutembelea hapa, pamoja nao yupo Naibu

Spika pale pamoja na wageni wetu wote, Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, ahsante sana kwa kuwa na wageni wetu, kuwapokea na kushinda nao kutwa nzima ya leo na kuwaelewesha mambo mbalimbali ambayo yanayohusu Bunge letu. Nakushukuru sana Naibu. (*Makofi*)

Tume hii ambayo nitawatambulisha mmoja mmoja, yenyewe ni tofauti kidogo na Tume yetu *Parliamentary Service Commission* ya Bunge letu, ambayo ya kwetu inatokana na sisi wenyewe; Mwenyekiti wake ni Spika, Makamu Mwenyekiti ni Naibu Spika na Wajumbe, ya kwetu. Hii ya Nigeria, kwanza Nigeria kuna mabunge mawili; kuna Bunge dogo na lile kubwa wanaloita *Senate*.

Kwa hiyo Tume hii ni Mabunge yote mawili, lakini wajumbe wake wote sio Wabunge, wanatoka nje ya Bunge. Wao hiyo shughuli ya kuwa Mjumbe wa Tume ni kazi ya muda wote, tofauti na ya kwetu ambayo ni kama bodi na kadhalika na tuna tofauti nyingi ambazo tumejifunza na baadhi ya mambo mazuri, tutayachukua. (*Makofi*)

Tume hii inaongozwa na *Executive Chairman of the Commission, Engineer Ahmed K. Amshi*, ndio kiongozi wa msafara mzima wa Tume hii ya kutoka kwa ndugu zetu wa Nigeria. (*Makofi*)

Mwingine ni *Member, Senate Committee on Establishment and Public Service Senator Bomai Ibrahim Mohammed*, huyu amefuatana na hii Tume lakini sio mjambe kwa sababu ye ye ni *senator kwenye Bunge lile la Senate*. (*Makofi*)

Makamishna ni pamoja na hao wanaofuata, kutoka *North Central Alhaji Auwalu Aliyu Ohindase, thank you.* (*Makofi*)

Makamishna wengine ni Mheshimiwa Muazu Ishaq, Abubakar Tutare, Babagana Modu na Bilyaminu Yusuf Shinkafi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naona Mheshimiwa Mkuchika na Waziri wa Fedha hawapigi makofi sawasawa kwa sababu wanaikumbuka *Rivers United* ilivyowachapa juzi juzi hapa. Timu ya *Rivers* kutoka Nigeria ilivyowakung'uta. (*Makof/Kicheko*)

Makamishna wengine ni Alhaji Samo Saidu Kazaure, Senator Julius A. Ucha, Chief Francis Atanomeyowvi Jp, Engineer Bassey O. Etuk, Alhaji Hakeem Akamo, Motunrayo Akintomide na pia yupo Katibu wa Kamisheni Ikharo Lucky. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge wako sasa watumishi mbalimbali wa Bunge; Director of Planning, Research and Information Technology, Omobolanle O. Lipede; Director of Public Affairs, Janet J. Mambula; Director of Administration and Employee Relations, Ahmed Bala Binta; Director of Procurement and General Service, Ahamed Malami; Director of Zonal Officers and Legislative Aid, James Ekeji; yupo Director of Finance and Accounts, Innocent O. Odo; Director of Promotion and Discipline, Ribadu Ismaila; Director of Establishment, Records and Training, Mr. Sopitan O. Olusola; Deputy Director of Appeals and Legal Service, Mr. Ajiboye O. Festus; Deputy Director of Planning Ms. Fatima B. S. Bashir; Chief Administrative Officer, Mr. Isola Olayinka; Assistant Chief Administrative Officer, Mr. Bavid Simpa, Assistant Chief Administrative Officer, Mr. Orji Chidiebere; Executive Chairman's PA Mr. Ali Garba; ni huyo Personal Assistant wa Chairman na yupo kutoka Utawala Micheal Oladimeji O. M. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo ndio timu ya wageni wetu wamekuja leo asubuhi kutoka Dar es Salaam, na wanafuatana na Balozi wa Nigeria hapa Tanzania. Mheshimiwa Balozi yupo? His Excellence, the Ambassador? Is not there, okay. Walikuwa wamefuatana naye, itakuwa ametoka kidogo.

Wamekuja leo asubuhi na leo jioni wataondoka na ndege ya saa 12.30 kurudi Dar es Salaam. Kwa hiyo

tumeshinda nao kwa kutwa nzima ya leo, tumewapokea, tumeshinda nao vizuri wageni wetu hawa, katika kuimarisha umoja wa Mabunge ya Afrika ya *Common Wealth* ambapo sisi hapa ndio Makao Makuu ya *CPA Africa*. Kwa hiyo wageni wetu karibuni sana. (*Makofii*)

Ahsante sana Naibu, mnaweza mkaendelea na programu inayofuata, ahsanteni sana. (*Makofii*)

Tangazo la kikao; Mheshimiwa Margaret Sitta, anawatangazieni Wabunge ambao ni Wanachama wa Chama cha Kibunge cha Elimu Bora kwa Wote (*Parliamentary Organization for Quality Education for All – POQEA*), kwamba kutakuwa na kikao leo tarehe 3 Novemba mara baada ya kumaliza shughuli za Bunge. Kikao hicho kinatarajiwa kufanyika kwa kifupi sana pale Ukumbi wa Msekwa. Hivyo wanachama wote ambao mngependa kujinga na chama hicho kuhudhuria katika kikao hicho muhimu sana kwa ajili ya maandalizi ya uzinduzi wa chama hicho utakaofanyika tarehe 5 Novemba. Kwa hiyo naona kuna *interest* kubwa sana katika *quality education*. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Sasa Katibu tuendelee. Katibu.

NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Kamati ya Mipango.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaingia kwenye sessionya siku tano mfululizo kuanzia leo ikiwa *day one*, ambapo tutakuwa katika utaratibu wa Kamati ya Mipango. Sasa bila kupoteza muda nimkaribishe Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchomba ili atupitishe katika hotuba yake ambapo nampa dakika 45.

Karibu hapa mbele Mheshimiwa Waziri, tafadhali, endelea sasa.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Mipango na lipokee na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango pamoja na Bajeti ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kutoa pole kwako wewe mwenyewe, Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote na ndugu jamaa na marafiki kwa kifo cha Mheshimiwa William Tate Olenasha aliyekuwa Mbunge wa Ngorongoro, CCM na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji.

(Hapa Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaombeni sana muwe utulivu, kwa sababu tutakuwa na mjadala katika siku hizi tano, ni vizuri sana kumsikiliza Mheshimiwa Waziri ili hata utakapokuwa unachangia, basi unakuwa katika *position* ambayo ni *informed*. Mheshimiwa Waziri endelea.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati kabisa, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu kwa busara, hekima, weledi na umahiri mkubwa pamoja na kuendeleza mashirikiano na nchi mbalimbali. Tunazidi kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu, ujasiri na afya njema ili aendelee kutekeleza majukumu mbalimbali ya kulihudumia Taifa kikamilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, naendelea kuwapongeza wasaidizi wake akiwemo Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori

Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye pia ni kiongozi wa shughuli za Serikali hapa Bungeni kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie fursa hii kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi, pamoja na Wenyeviti wanaokusaidia katika shughuli hapa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, nitumie fursa hii pia kuishukuru Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Bajeti chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini; Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi; pamoja na wajumbe wa kamati kwa kutoa maoni bora yaliyoboresha taarifa yetu hii tunayoisoma hapa leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutoa shukrani za dhati kwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Mipango na Fedha wakiongozwa na Katibu Mkuu - Bwana Emmanuel Mpawe Tutuba kwa ushirikiano wao katika kukamilisha taarifa hii tunayoiwasilisha hapa leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya mwongozo huu wa mpango pamoja na Bajeti ya Serikali yamezingatia vigezo muhimu na ni taarifa muhimu sana kwa kutoa taswira ya Serikali ya Awamu ya Sita ambayo imejipambanua kwajuhudi kubwa za kuboresha maisha ya Watanzania. Mapendekezo haya ya Mwongozo ni maandalizi ya mpango pamoja na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023. Mapendekezo haya yamezingatia mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mwongozo wa mwaka 2021/2022 pamoja na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano yaani 2016/2017 hadi 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya pia yameainisha masuala mbalimbali muhimu yakiwemo mapitio ya utekelezaji wa mpango pamoja na bajeti ya mwaka 2021na robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022 mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi, makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2022/2023 na maeneo ya kipaumbele katika Mpango pamoja na Bajeti kwa mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, pia yamezingatia vihatarishi vyatatu ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa Mpango na Bajeti na mikakati ya kukabiliana navyo. Maelekezo yanayotakiwa katika kuzingatia kwa Maafisa Masuuli wakati wa uandaaji wa bajeti, utekelezaji wa bajeti, ufuatiliaji pamoja na tathmini ya Mpango pamoja na Bajeti ya mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2020, uchumi ulikuwa kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na matarajio ya kukuwa kwa 5.5% katika kipindi kama hicho na ukuaji halisi wa 7% kwa mwaka 2019. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana na athari za UVIKO 19, lakini pamoja na kupungua kwa kasi ya ukuaji, Tanzania iliweza kuwa mionganini mwa nchi chache duniani zilizokuwa na ukuaji chanya wa uchumi katika mwaka 2020. Hali hii ilitokana na hatua ya Serikali kutokusitisha shughuli za biashara pamoja na uzalishaji wakati wa mlipuko wa ugonjwa UVIKO 19.

Mheshimiwa Spika, naomba taarifa yangu yote iingie katika *Hansard*. Katika mwendelezo wa ukuaji wa uchumi pamoja na maeneo mengine, shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa imara dhidi ya sarafu ya washirika wakuu wa biashara ulimwenguni katika kipindi chote cha mwaka 2020/2021. Hali hii imechangiwa na utulivu wa bei hapa nchini, utekelezaji wa sera thabiti za fedha pamoja na bajeti, usimamizi imara katika soko la kubadilisha fedha za kigeni pamoja na kuimarisha urari wa biashara na utulivu wa bei ya mafuta katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi milioni 2309.58, ikilinganishwa na wastani wa shilingi milioni 2301.30 katika

kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/2020. Badiliko hilo lilikuwa la kiasi cha 0.40% kwa mwaka ikilinganishwa na 0.36% katika mwaka uliopita. Kiwango hicho kilikuwa kidogo cha kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache duniani zilizoweza kuwa na utulivu wa kiwango cha kubadilisha fedha dhidi ya fedha za kigeni licha ya athari za UVIKO 19.

Mheshimiwa Spika, deni la Serikali lilifikia shilingi bilioni 64,497.83 Juni, 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 56,449.8 Juni, 2020, sawa na ongezeko la 14.3%. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi bilioni 45,563.5 na deni la ndani ni shilingi bilioni 18,934.3. Mwenendo huo wa deni ultokana na kupokelewa kwa mikopo yenye masharti nafuu na ya kibiasara kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo hususan ile inayochochea ukuaji wa uchumi. Pamoja na kuongezeka kwa deni la Serikali, deni hilo linaendelea kuwa himilivu katika muda mfupi, muda wa kati pamoja na muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa viashiria vyta uchumi yanapatikana katika sehemu ya kwanza, sura ya kwanza ya kitabu cha Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango pamoja na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023, sura ya pili ya kitabu cha Mapendekezo ya Mpango.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa bajeti pamoja na mpango; katika mwaka 2020/2021 Serikali imekusanya shilingi bilioni 31,280.1 sawa na asilimia 89.7 ya lengo. Kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 20,594.6 ni mapato ya ndani na shilingi bilioni 10,685.5 ni misaada na mikopo ya ndani na nje ya nchi. Aidha, Serikali ilitumia shilingi bilioni 31,280.1 kughaamia shughuli mbalimbali ambapo shilingi bilioni 20,613.0 ni matumizi ya kawaida, na shilingi bilioni 10,667.1 ni matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2020/2021 na robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022 yanapatikana katika sehemu ya kwanza, sura ya pili ya Kitabu cha Mwongozo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2020/2021 na robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022, pamoja na mafanikio na Serikali ya Awamu ya Sita ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kielelezo na shughuli nyingine katika maeneo ya kipaumbele yaliyobainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano yaani 2021/2022 -/2025/2026. Hatua iliyofikiwa pamoja na sehemu ya mafanikio imeainishwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza: Kukuza mapato. Moja ya mafanikio yaliyopatikana ni kuendelea kuimarika kwa mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri ambapo makusanyo hallisi yaliuka kwa asilimla 7.2 kati ya Aprili hadi Septemba, 2021 na kufikia shilingi bilioni 10,629.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 9,915.0 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madeni na madai, Serikali imelipa madeni yaliyohakikiwa jumla ya shilingi bilioni 516.23 na kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 111.41 ni madeni ya watumishi na shilingi bilioni 70.49 ni madeni ya wazabuni na shilingi bilioni 2.17 yakiwa madeni ya watoa huduma wadogo wadogo. Shilingi bilioni 264.23 yakiwa ni madeni ya wakandarasi na madeni mengineyo yanayotokana na hukumu za Kimahakama na fidia yakiwa yanafikia shilingi bilioni 67.93.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kero za Muungano, Serikali imetatua changamoto 11 za Muungano zikiwemo masuala yaliyokuwa yanahuisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato, ukokotoaji wa kodi kwenye huduma za simu inayofanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar na masuala ya ucheleweshwaji wa mikataba mbalimbali inayohusu miradi ya maendeleo. Yote hayo yametatuliwa yakiwemo pamoja na mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kukuza biashara na uwekezaji, moja ya mafanikio yaliyopatikana ni kurahisisha kwa upatikanaji wa vibali vya kazi kwa kuanzisha mfumo wa kielektroniki (*e-permit*) ambapo kwa sasa vibali vinapatikana kati ya siku moja hadi tatu kutoka siku 14 baada ya kuanzishwa kwa dirisha moja la kielektroniki la uwekezaji; kuanzishwa kwa Kituo cha Mawasiliano cha uwekezaji na kanzidata ya ardhi yenye ukubwa wa hekta milioni 1.6; mengine ikiwa ni kufanyika kwa Mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara, kusajili miradi 182 yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 3.5 inayotarajiwa kuanzishwa na kuzalisha ajira zaidi ya 43,782 ikilinganisha na miradi yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 647.43 ya mwaka uliopita.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kutolewa kwa leseni za *BRELLA* 6,051 ikiwa ni sambambana kuondolewa kwa vilkwazo visivyo vya kiforodha kati ya nchi ya Tanzania na nchi jirani ikiwepo Kenya kutoka 64 hadi 46 na kuridhiwa kwa mkataba wa eneo huru la kibiashara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo, mafanikio ni pamoja na kuzalishwa kwa mbegu bora tani 50,589.43 na miche 13,568,422 ya mazao mbalimbali pamoja na kupatikana kwa mbolea tani 678,017. Mafanikio mengine ni pamoja na kununuliwa kwa lita 113,066 za viwatilifu pamoja na kudhibiti visumbufu vya mlipuko. Katika mwaka wa 2021 shilingi bilioni 79.9 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022 na shilingi bilioni 76.8 zimeshatumika katika hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ya Serikali ya Awamu ya Sita katika Sekta ya Kilimo ni pamoja na kuendelea kuimariika kwa Sekta ya Kilimo ambapo mashamba yenye ukubwa wa hekta 237,941.9 yamehakikiwa na kupimwa na kupimiwa afya ya udongo. Mafanikio mengine ni ujenzi wa vihenge, ukarabati na ujenzi wa skimu za umwagiliaji, udhibiti wa nzige katika mikoa ya Kaskazini na kufungua kwa vituo vya mazao nje ikiwemo katika nchi za Kenya, Sudan Kusini, China, India, Ukraine, Saudi Arabia, Umoja wa Ulaya pamoja na nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kuimarisha uhifadhi wa chakula hapa nchini ambapo shilingi bilioni 129 zimetolewa kwa ajili ya Wakala wa Hifadhi wa Chakula (*NFRA*) na Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Mafanikio mengine ni kuimarika kwa bei ya mahindi kwa wakulima ambapo Serikali ilinunua mahindi kwa shilingi 500 kwa kilo kutoka shilingi 300 ya kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mifugo, mafanikio ni pamoja na kujengwa kwa majosho 49 katika Halmashauri 18 ambapo utekelezaji wa miradi hiyo umeshafikia wastani wa asilimia 60. Uhimilishwaji wa ng'ombe 78,575 katika mikoa 10 na kukamilika kwa ukarabati wa mabwawa matatu. Kwa upande huu wa mabwawa, kasi yake itaenda kuongezeka kufuatia utaratibu huu unaoendelea wa kupatikana mitambo ya kujenga mabwawa katika kila ukanda yaani wa pande nne wa nchi yetu utakaosaidia pia katika jukumu hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uvuvi, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni kujengwa kwa ofisi tano za vikundi vyta usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi katika Halmashauri tano; yaani Bagamoyo, Lindi Vijijini, Mkinga, Pangani pamoja na Chalinze.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kujengwa kwa maabara moja ya utafiti wa uvuvi katika kituo cha *TAFIRI* Dar es Salaam na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa Bandari ya Uvivi na ununuzi wa meli za uvuvi katika bahari kuu. Kwa upande wa uendelezaji wa viwanda, mafanikio ni pamoja na kujengwa kwa mtambo wa kuyeyusha chuma katika kiwanda cha *Kilimanjaro Machine Tools Company* ambapo ujenzi umefikia zaidi ya asilimia 80 na mafanikio mengine ni kuanza kwa uzalishaji katika kiwanda cha kuunganisha magari cha *GF Trucks Motors* katika eneo la viwanda, yaani *TAMCO* kule Kibaha.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa madini, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha pamoja (*One Stop Center*) Mirerani; kuanzishwa kwa masoko mapya matatu ya madini ya Kiteto Manyara, Mirerani

Arusha na Mangaka Mtwara. Mafanikio mengine ni pamoja na kuanzishwa kwa vituo vipyta 18 vya ununuzi wa madini; kujengwa kwa Makao Makuu ya Tume ya Madini, kununuliwa kwa mtambo mmoja wa uchorongaji kwa ajili ya Shirika la Madini la Taifa; kukusanya kwa mapato yasiyo ya kikodi kiasi cha shilingi bilioni 588.04 kwa mwaka 2020/2021 na kununuliwa kwa vifaa vya utafiti vitakavyotumika katika taasisi yetu hiyo ya madini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utali, mafaikio yaliyopatikana ni pamoja na kuanza kuimariika kwa Sekta ya Utalii ambapo watalii waliotembelea hapa nchini wamefikia 464,913 na kuanzishwa kwa mpango wa kutangaza utalii hapa nchini ambao umejulikana kwa jina la *Royal Tour* ambao umelenga kutangaza vivutio vyetu vya utalii na fursa za kiuchumi za nchi yetu katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kadhalika katika kutekeleza miradi mahsusini chini ya Kampeni ya Maendeleo na Mpambano wa Uviko 19, shilingi bilioni 90 zimeelekezwa kugharamia sekta hiyo ya utalii ambayo iliathirika na uviko 19 kwa upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mataifa mbalimbali duniani ambayo ni washirika wetu wa kibashara kuchukua hatua za kudhibiti kuenea kwa Uviko 19 ikiwemo kusitisha baadhi ya safari, ni dhahiri kwamba Sekta ya Utalii iliathiria. Fedha hizo zitatumika katika kutekeleza maeneo ambayo yatarejesha hali ya utalii na pia ikiwa katika kufidia maeneo ambayo yaliathirika zaidi hasa ya kitaasisi ikiwemo *TANAPA*, *TAWA*, *NCAA*, *TFS* pamoja na *NMT*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa reli ya kati, moja ya mafanikio ambayo yamepatikana ni ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa ambapo kipande cha Dar es Salaam – Morogoro ambayo ni kilometra 300 kimeshafikia zaidi ya asilimia 93. Kipande cha Morogoro – Makutupora – Singida chenye kilometra 422 kimeshafikia zaidi ya asilimia 70 na kuanza kwa ujenzi wa kipande cha Mwanza – Isaka chenye

kilometra 341 ambacho kinaendelea; vile vile hatua za kuanza ujenzi wa kipande cha Makutupora – Tabora na Tabora – Isaka vikiwa viko katika hatua za kutafuta Wakandarasi na vikiwa vimeshafikia hatua nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa abiria na mizigo katika maziwa makuu, tukianza na Ziwa Victoria, mafanikio yaliyopatikana ni kukamilika kwa ukarabati wa meli mbili za *New Butiama*, Hapa Kazi Tu na *New Victoria* Hapa Kazi Tu na kuendelea na ujenzi wa meli mpya, yaani MV Mwanza Hapa Kazi Tu ambao umeshafikia zaidi ya asilimia 80. Mafanikio mengine ni kukamilika kwa ujenzi wa Chelezo cha kujengea na kukarabati meli katika Bandari ya Mwanza. Kwa upande wa Ziwa Tanganyika ni kusainiwa kwa mkataba kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli ya *MT. Sangara*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ziwa Nyasa ni kukamilika kwa ujenzi wa matishali mawili yenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja na kukamilika kwa ujenzi wa meli moja mpya yaani MV. Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa anga ni kuanza kwa ujenzi wa Uwanja wa Ndege Msalato ambapo tayari kumeshasainiwa mkataba na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Mikoa ya Shinyanga, Tabora, Sumbawanga pamoja na kuanza maandalizi ya maboresho ya kiwanja cha Ndege cha Kigoma.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kuendelea kwa ujenzi wa viwanja vya ndege vya Songea ambapo tayari asilimia 95 imeshakamilika, Mtwara asilimia 61, Iringa asilimia 21.3 na kukamilisha malipo ya awamu ya mwisho ya kupokelewa kwa ndege tatu, hivyo kufanya jumla ya ndege mpya zilizonunuliwa kufikia kuwa 11.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni shirika la ndege Tanzania kupata kibali cha kwenda moja kwa moja katika nchi mbalimbali ikiwemo Falme za Kiarabu pamoja

na kwingineko ambapo tayari shilingi bilioni 596.3 zimeshatolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara na madaraja, mtandao wa barabara hapa nchini umefikia kilometa 36,361.95 ambapo barabara kuu ni kilometa 12,215.58 na barabara za mikoa ni kilometa 24,146.37 na ujenzi wa madaraja 8.647 katika barabara kuu na barabara za mikoa. Katika kipindi cha mwaka 2021, shilingi bilioni 1,552.8 tayari zimeshatumika katika robo ya kwanza ya Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ya Serikali ya Awamu ya Sita ni pamoja na kuanza ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano katika Jiji la Dodoma. Barabara hizi ni pamoja na ujenzi wa barabara za mzunguko katika Jiji la Dodoma ambapo ni barabara zenyet urefu wa kilometa 112.3. Ujenzi umeanza na unatarajiwaa kukamilika katika mwaka wa fedha unaokuja. Kazi nyiningine ni maandalizi ya upanuzi wa barabara kutoka Dodoma kwenda Singida kilometa 50, Dodoma – Iringa kilometa 50, Dodoma – Arusha kilometa 50, Dodoma – Morogoro kilometa 70 na kuendelea na ujenzi wa barabara za njia nne, Kimara hadi Kibaha ambapo ujenzi umeshafikia zaidi ya asilimia 95.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni kuendelea kwa ujenzi wa daraja kubwa likiwemo daraja la *Tanzanite* ambao umeshafikia zaidi ya asilimia 97, Kigongo – Busisi ambao umeshafikia zaidi ya asilimia 32 na Wami zaidi ya asilimia 65. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa barabara za ndani ya Jiji la Dodoma ambao ni asilimia 6.4 na wenyewe unaendelea.

Mheshimiwa Spika, tayari shilingi bilioni 228.3 zimeshatolewa katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha unaoendelea ambapo zinatumika katika ujenzi wa barabara za lami kilometa 27 lakini pia ukiwa unaendelea kwa ajili ya ujenzi wa madaraja pamoja na vivuko na barabara zenyet urefu wa kilometa 4,439.28. Katika hatua nyiningine, Serikali inatarajia kuanza ujenzi wa barabara mpya za kufungua fursa

za kiuchumi zenye urefu wa kilometra 879 katika sehemu mbalimbali hapa nchini. Hii itasaidia kufungua zaidi Taifa katika maeneo ya uzalishaji pamoja na biashara katika maeneo ya kikanda.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) na mshauri elekezi inakamilisha mchoro wa daraja la Jangwani ili kufanikisha maandalizi na majadiliano na Benki ya Dunia yatakayowezesha kumaliza tatizo la muda mrefu la mafuriko katika eneo lile la Jangwani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bandari, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na upande wa Bandari ya Dar es Salaam. Awamu ya kwanza ya utekelezaji umefikia asilimia 95 ambapo Gati Na. 1 hadi Na. 7 limeongezwa kina hadi kufikia mita 14.5 na gati maalum la kuhudumia meli za magari Roro limeshaanza kutumika. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 shilingi bilioni 124.4 zimetumika katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bandari ya Mtwara, ujenzi wa Gati Na. 1 lenye urefu wa mita 300 na sakafu ngumu, umekamilika ambapo katika mwaka wa fedha 2020/2021, shilingi bilioni 65.47 tayari zimetumika. Hii ni sambamba na Bandari ya Tanga ambapo uongezaji wa kina cha lango cha bandari kutoka mita 4 - 13 na ujenzi wa Gati Na. 2 kwenye kina kirefu umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 shilingi bilioni 20.41 zimetumika na katika robo ya kwanza tayari shilingi bilioni 11.6 zimeshatumika.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa nishati/miradi ya umeme; baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na utekelezaji wa mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere *megawatt* 2,115 ambaao umeshafikia zaidi ya asilimia 55.6 ambapo ujenzi wa handaki la kuchevushia maji umekamilika. Aidha, kazi nyingine zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa tuta kuu la bwawa, ujenzi wa njia za kupelekea maji kwenye mitambo, ujenzi wa jengo la mitambo, kingo za

bwawa, kituo cha kuongeza nguvu za umeme, swichi, *switch yard* pamoja na utengenezaji wa mitambo tisa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya umeme, baadhi ya mafanikio ni pamoja na kuendelea na usambazaji wa umeme ambapo zaidi ya vijiji 10,361 kati ya vijiji 12,317 vya Tanzania Bara, sawa na asilimia 84.12 vimeunganishiwa umeme. Mradi wa umeme wa Rusumo wa *Megawatt* 80 umefikia zaidi ya asilimia 81.2, mradi wa njia za kusafirishia umeme msongo wa *KV260* kutoka Bulyanhulu hadi Geita yenye urefu wa kilometra 55 umekamilika.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine kati ya hiyo katika mwaka wa fedha 2020/2021 imetumia jumla ya shilingi bilioni 1,067 na kati ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha unaoendelea tayari shilingi bilioni 88.1 zimeshatumika. Mafanikio mengine katika sekta hiyo ni kuendelea na ujenzi wa njia nne za kusafirishia umeme, Rufiji – Chalinze ambapo shilingi bilioni 112 zimeshatumika.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine katika sekta hiyo ni pamoja na hatua ambayo imeshafikiwa katika ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima Uganda hadi Chongoleani Tanga. Tayari katika mwaka wa fedha 2021 shilingi bilioni 262.7 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa sehemu ya hisa za Serikali sawa na asilimia 45.4 ya lengo la mtaji wa shilingi bilioni 577.7 na fedha zilizosalia zitalipwa kama ambavyo iliainishwa katika makubaliano.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, kati ya mafanikio yaliyotokea katika Awamu ya Sita ni pamoja na ukamilishwaji wa ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Rufaa 19, kuendelea na ujenzi wa hospitali 99 za Halmashauri ambazo zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji; kutolewa kwa chanjo kwa watoto 2,112,411 wenyewe umri wa chini ya miaka mitano sawa na asilimia 101 ya lengo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2020/2021 ni pamoja na shilingi bilioni 402.7 zikiwa zimeshatumika katika robo ya

kwanza na shilingi bilioni 83.2 zikiwa zimetumika. Aidha, Serikali imepata dozi 1,058,000 za chanjo ya Uviko 19 aina ya *J and J* kutoka USA, dozi 1,065,000 aina ya *Sinopharm* kutoka *Covax facility* ambapo hadi Oktoba 20, 2021 jumla ya watu 959,377 ambaao ni sawa na asilimia 90.6 walipata chanjo ya *J and J* na watu 8,591 walipata chanjo aina ya *Cinopharm*. Shilingi bilioni 234 zimetolewa kwa ajili ya kununua dawa na shilingi bilioni 26.3 kwa ajili ya vifaa tiba, shilingi bilioni 7.9 kwa ajili ya kununua mashine za kupasua ubongo bila kupasua kichwa katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hatua hizo, katika utekelezaji wa mradi mahsusini chini ya kamjeni ya maendeleo na mapambano dhini ya *UVIKO-19* sekta ya afya imetengewa Shilingi Bilioni 466.9, na tayari zimeshapelekwa kwa ajili ya kujengwa na kukarabati miundombinu ya vyumba vya wagonjwa mahututi (*ICU*) kwenye hospitali 67 hapa nchini. Kununua vifaa vya *ICU* katika hospitali 66, kujenga na kukarabati miundombinu ya kutolea huduma za dharura (*EMB*) katika hospitali 115, kununua vifaa katika miundombinu ya kutolea huduma za dharura katika hospitali 119, kununua magari 253 ya kubebea wagonjwa, 20 yenye kiwango cha huduma za juu (*advanced ambulance*) na magari 233 yenye kiwango cha huduma za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ni pamoja na kusimika mfumo wa usambazaji wa hewa-tiba (*oxygen*) kwa wagonjwa katika wodi za hospitali 82, kununua mitungi 5,782 ya hewa-tiba ya *oxygen* na vifaa wezeshi vya utoaji hewatiba katika hospitali 116 hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine yatakuwa ni pamoja na kusimika mitambo 53 ya kuzalisha hewatiba. Pia mafanikio mengine yatakuwa ni kununua vifaa wezeshi vya utoaji hewa-tiba katika hospitali 116. Sambamba na hiyo, mafanikio mengine yatakuwa ni kununua seti 2700 za vitanda vya wagonjwa pamoja na magodoro yake na makabati pamoja na meza. Mafanikio mengine katika sekta hii yatakuwa ni kununuliwa na kusimikwa mashine 85 za *X-ray*, mashine 29 za *CT scan*, mashine saba za huduma za

uchunguzi wa moyo pamoja na *MRI* Nne ambazo zitaenda kukamilisha hospitali zetu zote za Kanda kuwa na huduma hiyo ya *MRI*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine yatakuwa ni kununua mashine ya upimaji wa gesi katika damu pamoja na kukamilisha utaratibu wa usambazaji wa chanjo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu, baadhi ya mafanikio yaliyokamilika ni pamoja na ujenzi wa miunndombinu katika shule za msingi 998 na sekondari 719 kwenye Halmashauri 184. Mafanikio mengine ni ujenzi wa maktaba saba katika Mikoa ya Kigoma, Rukwa, Kagera, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa pamoja na Tabora. Mafanikio mengine pia ni ujenzi wa *VETA* katika maeneo ya Chato, Goroa upande wa Manyara, Ngorongoro, Simanjiro pamoja na Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine zinazoendelea ni katika utekelezaji wa elimu msingi bila malipo ambapo tayari fedha ambazo zinatakiwa kutumika zimeendelea kutolewa kwa kadri zinavyohitajika kwa kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuititia kampeni ya maendeleo na mapambano dhini ya *UVIKO* sekta ya elimu imetengewa bilioni 368.9, ambapo shilingi bilioni 304 zitatumika kupunguza msongamano madarasani kwenye upande wa sekondari na kwenye mabweni kwa kujenga vyumba vya madarasa 15,000 katika shule za sekondari na shule za msingi shikizi 3,000 pamoja na madawati 641,850 na kujenga mabweni 50 kwa ajili ya wanafunzi wenyе ulemavu. Shilingi bilioni 64.9 zimeelekezwa katika kukamilisha Vyuo vya Ufundis Stadi (*VETA*) sita pamoja na vyuo katika Wilaya 26 kwa upande wa Wilaya. Hii ni sambamba na uchapishaji wa vitabu vya nukta nundu 10,812 kwa ajili ya wanafunzi wenyе uhafifu wa kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maji, upatikanaji wa huduma ya maji umeimarika ambapo hadi Juni, 2021 umefikia wastani wa asilimia 72.3 vijijiini na asilimia 86 kutoka asilimia 84. Kazi hiyo imefanyika ni pamoja na ukarabati wa vituo 159 vya kufuatilia mwenendo wa maji na kukamilika kwa miradi 666 inayonufaisha wananchi zaidi ya milioni 3.8 waishio vijijiini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Shilingi Bilioni 495.3 zimetumika, na katika robo ya kwanza Shilingi Bilioni 99.8 tayari zimeshatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia inaendelea na utekelezaji wa miradi mahsusi kupitia kampeni ya maendeleo na mapambano dhidi ya UVIKO-19, ambapo Shilingi Bilioni 139.4 zinatarajia kugharamia miradi mbalimbali ya maji. Hii inajumuisha Bilioni 101.7 kwa ajili ya ukarabati, upanuzi na uongezaji wa miundombinu ya usambazaji wa maji, na Shilingi Bilioni 37.6 kwa ajili ya kununulia mitambo 25 ya kuchimba maji ili kuongeza kasi ya uchimbaji wa visima vitakavyohitajika katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Kwa maana hiyo kila Mkao utakuwa na mtambo wake wa kuchimbia maji, na kutakuwepo na seti tano za mitambo ya uchimbaji na ujenzi wa mabwawa ambayo itagawanywa katika pande nne za nchi yetu. Vilevile kutakuwepo na seti nne ambazo zitatumia kwa upande wa uchunguzi wa maji ardhini ili kuweza kupata maeneo yanayostahili kuweza kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa habari, mawasiliano na TEHAMA baadhi ya maganikio yaliyopatikana ni kukamilika kwa ujenzi wa mkongo wa taifa kwa kilometra 409 katika mgawanyo ufuatao: -

Kilometra 72 kuunganisha nchi ya Msumbiji kupitia mpaka wa Mtambaswala katika Mkao wa Mtwara na kukamilika kwa kituo cha kutoa huduma za mawasiliano kilometra 72 kuunganisha watumiaji wa mwisho (*last connectivity*) katika ofisi za Serikali, na kilometra 265 awamu ya kwanza ya Manyoni hadi Kambi ya Katoto kule Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ni kukamilika kwa ukarabati wa kilometra 105 za ujenzi wa mkongo wa Arusha-Namanga kuitia miundombinu ya TANESCO, ununuzi wa magari 47 kwa ajili ya kuhudumia shughuli za mkongo na kukamilika kwa uwekaji wa miundombinu ya anuani za makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mahakama na Utawala wa Sheria ni kuimari kwa mfumo wa utoaji wa haki na usimamizi wa sheria ambapo jumla ya mashauri 104,441 yalisikilizwa katika ngazi mbalimbali, kuteuliwa kwa Majaji wapya saba wa Mahakama ya Rufaa, Majaji 21 wa Mahakama Kuu na kuajiriwa kwa Mahakimu 245. Hii ikiwa inaenda sambamba na ujenzi wa vituo sita jumuishi vya utoaji huduma za mahakama katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro pamoja na Mwanza. Hatua nyingine zinaendelea ambazo zitahusisha kuwianisha Mahakama pamoja na maeneo mengine ya kiutendaji kazi ambayo yataboresha huduma za utoaji haki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ulinzi na usalama ni kutolewa kwa kuajiri jumla ya Askari 5400 kwa ajili ya shughuli mbalimbali pamoja na maeneo mengine na upande wa vyombo vyote ambavyo takwimu rasmi zinaonekana katika taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa utumishi wa umma, watumishi 29,900 wameajiriwa na watumishi 180,830 wamepandishwa vyeo na kulipwa stahili zao, na watumishi 8,202 wamebadilishwa kada, watumishi 30,228 wamelipwa malimbikizo ya madeni yao. Jumla ya Shilingi Bilioni 55.75 zimetumika na kupunguzwa kwa makato ya kodi ya PAYE kufikia asilimia nane kutoka asilimia tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni kulipa mafao ya Shilingi Bilioni 1,540 na pensheni ya shilingi bilioni 446.93. Aidha, Serikali inakamilisha mchakato wa kutoa hati fungani maalum zisizo taslim (*non-cash special bond*) za miaka nane hadi ishirini na tano kwa ajili ya kulipa madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii, ambapo

kiasi cha shilingi bilioni 2,176.74 kilichokuwa kimehakikiwa cha deni la 1999 kimeridhiwa kutolewa ifikapo Disemba 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kaya masikini ni kuimarika kwa maisha ya kaya masikini kuititia TASAF ambapo kaya 879,670 zitanufaika na utaratibu huo. Vilevile kwa kuwezesha wajasiriamali wadogo wadogo mpango kabambe unaendelea ambao Bunge lako Tukufu litaendelea kupata taarifa kama ambavyo zitakuwa zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sanaa na burudani, kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ambao umetengewa Shilingi Bilioni 1.5 kwa ajili ya kuzisaidia timu za Taifa. Nitumie fursa hii kuipongeza timu ya wanawake ambayo imefanya vizuri na imetutoa kimasomaso. Kwenye eneo hilli nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, ameendelea kuwapa motisha dada zetu na watoto wetu hawa pia nimshauri Mheshimiwa Bashungwa aangalie uwezekano wa kuzisaidia na *club* zetu, kwa sababu mwaka huu zimetolewa kwa aibu aibu. Japo ni aibu kubwa sana, ni aibu ndogo... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri naona muda wako! Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa ananikonyeza hapa, kwamba mbona unampa muda mwingi sana... (*Kicheko/Makofii*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu ndogo kidogo ukitolewa na timu ya Nigeria ambayo wako kwenye ramani, lakini ni aibu kubwa sana ukitolewa na Makhirikhiri wa hapa Botswana. Kwa hiyo Mheshimiwa Bashungwa aangalie na upande wa vilabu ili vilabu vyetu viweze kufanya vizuri kama ambavyo kilabu kimojawapo kimeonesha mfano mkubwa wa kucheza vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande kuimarisha Diplomasia mafanikio yaliyopatikana ni kufunguliwa kwa Ubalozi Mpya wa Tanzania kule Vienna Austria, kufunguliwa

kwa *Consul* Kuu katika Miji ya Lubumbashi katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Guangzhou nchini China pamoja na kuridhiwa kwa Mkataba wa uanzishwaji wa eneo huru. Kwa upande wa uimarishaji Makao Makuu ya Serikali hapa Dodoma hatua za kuimarissha Makao Makuu zinaendelea ambapo vibali vya ujenzi vimeshatolewa na michoro na ubunifu tayari imeshakamilika na zaidi ya shilingi bilioni 300 zimetengwa kwa ajili ya shughuli hiyo. Kuhusu maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo imetolewa katika kitabu cha mapendeleko sura ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili niweke msisitizo wa maeneo machache kwenye upande wa utekelezaji wa miradi. Msisitizo wa kwanza, Maafisa Manunuzi, Maafisa Masuuli na wasimamizi wa miradi yote hii tunayoiongelea wanatakiwa kuzingatia sheria na maelekezo katika kutekeleza miradi hii illi tuweze kupata ubora wa miradi na tuweze kupata *value for money* katika miradi yote inayotekelizwa. Kwa wote watakaohusika na ufuatiliaji wa miradi hii, kikiwemo kitengo cha *Monitoring and Evaluation, Expenditure Tracking*, Sekretarieti za Mikoa yote pamoja na wataalam wengine wote wanaohusika katika miradi wahakikishe wanagundua dosaro zote zinazojitikeza kabla dosari hizo hazijabainishwa na wakaguzi wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze wote pia ambao wanahusika na kukusanya mapato, lakini tuendelee kuweka mkazo katika ukusanyaji wa mapato. Bado kuna ulegevu kidogo kwenye ukusanyaji wa mapato katika maadhi ya maeneo. Kuna uvujaji mkubwa sana wa mapato yanayokusanya kwa upande wa maduhuli, kote kwenye Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa. Pia kumekuwa na ulegevu katika matumizi ya *EFD*. Tunashauriana sana kuhusu bei na matumizi ya risiti au tutoe risiti ama tusitoe risiti. Naelekeza tabia hiyo iachwe na tuendeleze matumizi ya *EFD* kama maelekezo na sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kuna vitendo vya rushwa, hasa katika baadhi ya ukusanyaji wa kodi kubwa ambazo zimekuwa zikijitokeza. Tunashauriana kiasi gani

kiende Serikalini na kiasi gani kije mifukoni mwetu. Vitendo vya aina hiyo navyo tuviache mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mpango naomba pia taarifa hiyo iingie yote kama ambavyo nimeanza kutoa maelezo tangu mwanzo nilipoanza kutoa taarifa hizi ambazo zinalezea na kwa upande wa takwimu hizo hizo kwa upande wa mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mwongozo Mahsusni katika utekelezaji na uandaaji wa bajeti, maelekezo mahsusni ni kutenga bajeti kwa ajili ya shughuli za ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kuandaa bajeti ambayo ni shirkishi kwa kuzingatia muundo wa mapato na matumizi wa muda wa kati na ratiba iliyobainishwa katika mwongozo. Pia kuimarisha Kamati za kibajeti ili kuweza kuhakikisha Kamati hizo zinafanya kazi kama ambavyo Sheria ya Bajeti sura namba hiyo inasema pamoja na maelekezo mengine yote ambayo tumekuwa tukiyatoa yaendelee kuzingatiwa kama yanavyotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mapendekezo ya mpango, katika mwaka 2022/2023 maeneo mahsusni ya kipaumbele yaliyobainishwa ni pamoja na kuchochea uchumi shindani na shirkishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma, kukuza biashara na uwekezaji, kuchochoa maendeleo ya watu pamoja na rasilimali watu na la mwisho ni kuendeleza rasilimali watu. Eneo hili linajumuisha *program* na mikakati inayolenga kuendeleza ujuzi pamoja na rasilimali watu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/2023 utajumuisha miradi ya kielelezo inayoendelea ambayo utekelezaji wake unatarajiwa kuwa na matokeo mapana na ya haraka katika uchumi. Miradi hiyo ni kama ambavyo nimeitaja katika taarifa yangu hii kuanzia mwanzo, ambapo nimeielezea na hatua ambazo zimeshafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uchumi shindani na shirikishi wa viwanda kwa maendeleo ya watu taifa linahitaji ushiriki wa sekta binafsi yenye uwezo wa kuchangia katika utekelezaji wa mpango. Kwa msingi huo, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa sekta binafsi kwa kuyafanyia kazi maoni na ushauri wa kukabiliana na changamoto za sekta binafsi zinazojitokeza katika utekelezaji wa mpango wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kutoa rai, kwamba wale wote ambao wako katika sekta binafsi wasitumie fursa hizi za maendeleo ambazo tunazitangaza kupandisha bei za bidhaa ambazo zingeweza kutumika na kuleta tija kubwa kama zingefuata bei ambazo ni za kawaida na ambazo ni bei za soko licha ya kutumia uhitaji mkubwa umetangazwa kufuatana na utekelezaji wa miradi mingi wakaingia vishawishi na tamaa ya kupandisha bei ili waweze kujipatia kipato kikubwa kuliko ilivyo kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina mahsusini kwenye maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2022/2023 yanayoongelea mpango wa maendeleo yapo katika kitabu cha mapendekezo ya mpango sura ya nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Mapendekezo ya mwongozo na mpango yatawezesha mafungu kuandaa mipango na bajeti kwa mwaka 2022/2023. Kutokana na mapendekezo haya Maafisa Masuuli wa Wizara, na Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2022/2023. Aidha, wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu Sheria ya Bajeti Sura Na. 439 na Kanuni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango

pamoja na Bajeti ya Serikali, na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/2023 kama nilivyowasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO MHE. DR.
MWIGULU L. N. MADELU KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO
WA MAENDELEO WA TAIFA UNAOKUSUDIWA KUTEKELEZWA
NA SERIKALI KWA MWAKA 2021/2023 PAMOJA NA
MWONGOZO WA KUANDAA MPANGO WA NA BAJETI YA
SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

- 1. Mheshimiwa Mwenyekiti**, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Mipango ili kupokea na kujadili mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/23.
- 2. Mheshimiwa Mwenyekiti**, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana ili kuwasilisha na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/23.
- 3. Mheshimiwa Mwenyekiti**, naomba kuchukua fursa hii kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, ndugu, jamaa na marafiki kwa kifo cha Mheshimiwa William Tate Olenasha aliyekuwa Mbunge wa Ngorongoro (CCM) na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Uwekezaji. Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi.
- 4. Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa moyo wa dhati, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea

kuliongoza Taifa letu kwa busara, hekima, weledi na umahiri mkubwa pamoja na kuendeleza mashirikiano na nchi mbalimbali. Tunazidi kumwombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumpa nguvu, ujasiri na afya njema ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu ya kulihudumia Taifa letu kikamilifu. Aidha, naendelea kuwapongeza wasaidizi wake wakuu, kwanza Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni kwa kuendelea kumshauri vyema Mheshimiwa Rais.

5. Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kushukuru kumpongeza Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika kwa kuendelea kuongoza bunge letu kwa weledi. Aidha, nitumile fursas hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini (CCM) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi (CCM) kwa maoni na maboresho wakati wa vikao vyatika kuboresha Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/23.

6. Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni (Mb), na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bw. Emmanuel Mpawe Tutuba kwa ushirikiano walionipa katika maandalizi ya hotuba hii, vitabu vyatika Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo pamoja na utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, minawashukuru sana Wizara, Taasisi, Idara za Serikali, Sekta Binafsi na wadau mbalimbali waliota maoni na michango yao katika kukamilisha Mapendekezo ya Mpango na Mwongozo.

7. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mapendekezo

ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/23 ni ya kwanza kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mapendekezo haya yanawasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu ili kupata maoni na ridhaa ya Waheshimiwa Wabunge.

8. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo haya ni muhimu kwa kuwa yanatoa taswira ya Serikali ya Awamu ya Sita ambayo imejjipambanua kwa juhudzi za kuboresha maisha ya Watanzania kwa kutekeleza mambo mbalimbali ikiwemo: Kuimarisha huduma za jamii hususan elimu, afya na maji kama ilivyojidhihirisha katika uzinduzi wa Kampeni ya Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 uliofanyika tarehe 10 Oktoba 2021; kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini ili kuchochea fursa za ajira; kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kimataifa; kudumisha amani na umoja wa kitaifa; na kuimarisha ulinzi na usalama katika mipaka yote ya nchi. Hivyo, mapendekezo yanayowasilishwa yameainisha masuala muhimu ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wakati wa kuandaa, kutekeleza, kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti za Mafungu yao ili kufikia malengo ya kiuchumi na kijamii yaliyobainishwa katika vipaumbele vya Taifa. Aidha, mapendekezo haya yanawasilisha vipaumbele vya Serikali katika mwaka 2022/23.

9. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/23 yamezingatia mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mwongozo wa mwaka 2021/22 pamoja na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21. Vilevile, Mapendekezo yameandalishiwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha Mwaka 2020 hadi 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); Hotuba

mbalimbali za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ikiwemo hotuba alioitoa katika Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania April 2021 na hotuba alioitoa tarehe 10 Oktoba 2021 wakati akizindua Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 chini; Sera na Mikakati mbalimbali ya Kisekta pamoja na makubaliano ya kikanda na kimataifa yaliyordhiwa na Tanzania.

10. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo haya yameainisha masuala mbalimbali, ikiwemo: mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2020/21 na robo ya kwanza ya mwaka 2021/22; mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi; makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2022/23; maeneo ya vipaumbele vya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23; vihatarishi vya ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa mpango na bajeti na mikakati ya kukabiliiana navyo; na maelekezo yanayotakiwa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatilaji na tathmini ya mpango na bajeti kwa mwaka 2022/23.

2.0MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

2.1 Mwenendo wa Viashiria vya Uchumi

11. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2020, uchumi ulikua kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 5.5 kwa kipindi hicho na ukuaji halisi wa asilimia 7.0 mwaka 2019. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kulitokana na athari za UVIKO-19. Pamoja na kupungua kwa kasi ya ukuaji, Tanzania iliweza kuwa mionganoni mwa nchi chache duniani zilizokuwa na ukuaji chanya wa uchumi katika mwaka 2020. Hali hii ilitokana na hatua ya Serikali ya kutositisha shughuli za biashara na uzalishaji wakati wa mlipuko wa UVIKO-19 (isipokuwa kwa kipindi kifupi tu cha robo ya pili ya mwaka 2020 ambapo baadhi ya shughuli zinazohusisha mikusanyiko ya watu kama shule, sanaa na burudani zilisitishwa kwa muda). Shughuli za kiuchumi zilizokuwa na ukuaji mkubwa mwaka 2020 ni pamoja na ujenzi (asilimia 9.1); habari na

mawasiliano (asilimia 8.4); na usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 8.4). Aidha, sekta ya kilimo iliendelea kuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa mwaka 2020, ikichangia asilimia 26.9, ikifuatiwa na ujenzi (asilimia 14.4), biashara (asilimia 8.7), viwanda (asilimia 8.4) na uchukuzi (asilimia 7.5). Mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 4.0 Septemba 2021, ikilinganishwa na asilimia 3.1 Septemba 2020.

12. Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya nje iliathirika moja kwa moja na athari za UVIKO-19, hususan shughuli za usafiri wa anga na utalii. Katika kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2021, urari wa malipo ya kawaida ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,414.2 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,127.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kutosha mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi. Hadi Juni 2021, kulikuwa na akiba ya fedha za kigeni ya dola za Marekani bilioni 5.2, ambayo inatosha kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 6.1. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi miezi 4.0 na zaidi ya lengo la miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

13. Mheshimiwa Mwenyekiti, viashiria vyta sekta ya benki vilikuwa na mwenendo wa kuridhisha ambapo thamani ya rasilimali za benki iliimarika kama inavyojidhahirisha katika kupungua kwa mikopo chechefu kufikia asilimia 9.30 Juni 2021 kutoka asilimia 10.84 Juni 2020; kuongezeka kwa faida kutokana na uwekezaji wa rasilimali kutoka wastani wa asilimia 2.19 mwaka 2019/20 na kufikia wastani wa asilimia 2.42 mwaka 2020/21; na kuongezeka kwa faida kutokana na uwekezaji wa mtaji kutoka wastani wa asilimia 9.88 mwaka 2019/20 na kufikia wastani wa asilimia 10.47 mwaka 2020/21. Mwenendo huu unaonesha kuendelea kuimarika kwa sekta ya benki ambapo kumekuwa na mtaji na ukwasi wa kutosha kukidhi mahitaji ya kila siku ya wengine amana na wakopajji. Kadhalika, riba za mikopo zilipungua kufikia wastani wa asilimia 16.60 kutoka wastani wa asilimia 16.80 mwaka 2020.

14. Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa imara dhidi ya sarafu za washirika wakuu wa biashara ulimwenguni katika kipindi chote cha mwaka 2020/21. Hali hii imechangiwa na: utulivu wa bei nchini; utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti; usimamizi imara katika soko la kubadilisha fedha za kigeni; kuimarika kwa urari wa biashara; na utulivu wa bei ya mafuta katika soko la dunia. Katika kipindi hicho, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,309.58, ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,301.30 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Badiliko hilo lilikuwa la kiasi cha asilimia 0.40 kwa mwaka ikilinganishwa na asilimia 0.36 katika mwaka uliopita. Kiwango hicho kilikuwa kidogo na kuifanya Tanzania kuwa mionganoni mwa nchi chache duniani zilizoweza kuwa na utulivu wa kiwango cha kubadilisha fedha dhidi ya fedha za kigeni licha ya athari za UVIKO-19.

15. Mheshimiwa Mwenyekiti, Deni la Serikali lilifikia shilingi bilioni 64,497.83 Juni 2021 ikilinganishwa na shilingi bilioni 56,449.8 Juni 2020, sawa na ongezeko la asilimia 14.3. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi bilioni 45,563.5 na deni la ndani ni shilingi bilioni 18,934.3. Mwenendo huo wa deni umetokana na kupokelewa kwa mikopo yenye masharti nafuu na ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo hususan inayochochea ukuaji wa uchumi. Pamoja na kuongezeka kwa deni la Serikali, deni hilo limeendelea kuwa himilivu katika muda mfupi, kati na mrefu.

16. Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa viashiria vya uchumi yanapatikana katika **Sehemu ya Kwanza, Sura ya Kwanza ya kitabu cha Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/23 na Sura ya Pili ya Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango**.

2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti

2.2.1 Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2020/21

17. Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka 2020/21, Serikali imekusanya shilingi bilioni 31,280.1 sawa na asilimia 89.7 ya

lengo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 20,594.6 ni mapato ya ndani na shilingi bilioni 10,685.5 ni misaada na mikopo ya ndani na nje ya nchi. Aidha, Serikali ilitumia shilingi bilioni 31,280.1 kugharamia shughuli mbalimbali, ambapo shilingi bilioni 20,613.0 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 10,667.1 ni matumizi ya maendeleo.

2.2.2 Utekelezaji wa Bajeti kwa Robo ya Kwanza ya Mwaka 2021/22 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, jumla ya shilingi bilioni 8,419.3 zilikusanywa kutoka vyanzo vyote, sawa na asilimia 93.3 ya lengo la kipindi hicho. Kati ya fedha hizo, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 5,492.1 sawa na asilimia 89.0 ya lengo la kipindi hicho. Misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 534.4 sawa na asilimia 88.6 ya lengo. Mikopo ya kibiashara kutoka katika soko la ndani ilifikia shilingi bilioni 1,220.9 sawa na asilimia 117.0 ya lengo la shilingi bilioni 1,043.2. Mikopo ya ndani ilivuka lengo katika robo husika kutokana na mwitikio mzuri wa wawekezaji, hususan katika hatifungani za muda mrefu. Hata hivyo, Serikali itahakikisha kwamba ukomo uliowekwa kwa mwaka 2021/22 unazingatiwa ili kutoathiri upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Kadhalika, mikopo ya nje ilifikia shilingi bilioni 1,171.9 sawa na asilimia 96.7 ya lengo la shilingi bilioni 1,211.6 katika kipindi hicho.

19. Mheshimiwa Mwenyekiti, ridhaa za matumizi zilizotolewa katika kipindi cha robo ya kwanza kwa mwaka 2021/22 ni shilingi bilioni 8,065.6 sawa na asilimia 89.3 ya lengo la shilingi bilioni 9,028.7. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5,517.7 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 2,547.9 ni fedha za maendeleo. Aidha, fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa zinajumuisha: shilingi bilioni 2,053.0 kwa ajili ya mishahara; shilingi bilioni 1,935.6 kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali; na shilingi bilioni 1,529.2 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo zilizotolewa zinajumuisha shilingi bilioni 2,367.2 fedha za ndani na shilingi bilioni 180.7 fedha za nje. Vilevile, kiasi cha shilingi bilioni 353.7 ni fedha za

Washirika wa Maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi.

20. Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2020/21 na robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 yanapatikana katika **Sehemu ya Kwanza, Sura ya Pili ya kitabu cha Mwongozo**.

2.3 Utekelezaji wa Baadhi ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2020/21 na Robo ya Kwanza ya Mwaka 2021/22 na Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita

21. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2020/21 na robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya kielelezo na shughuli nyingine katika maeneo ya kipaumbele yaliyobainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 - 2020/21. Hatua iliyofikiwa ambayo ni sehemu ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kama ifuatavyo:

(i) **Kukuza Mapato**: Kuendelea kuimarika kwa mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) ambapo makusanyo halisi yalikua kwa asilimia 7.2 katи ya Aprili hadi Septemba 2021 kufikia shilingi bilioni 10,629.4 ikillinganishwa na shilingi bilioni 9,915.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020;

(ii) **Kulipa madeni na madai**: Serikali imelipa madeni yaliyohakikiwa ya jumla ya shilingi bilioni 516.23. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 111.41 ni madeni ya watumishi, shilingi bilioni 70.49 ya wazabuni, shilingi bilioni 2.17 ya watoa huduma, shilingi bilioni 264.23 za wakandarasi na madeni mengineyo (madeni yanayotokana na hukumu za mahakama na fidia) yalikuwa shilingi bilioni 67.93;

(iii) **Kutatua kero za Muungano**: Serikali imetatua changamoto 11 za Muungano zikiwemo: masuala ya usimamizi wa ukusanyaji wa mapato; ukokotoaji wa kodi kwenye huduma za simu inayofanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar; na

suala la ucheleweshaji wa mikataba mbalimbali ya miradi ya maendeleo;

(iv) **Kukuza Biashara na Uwekezaji:** Kurahisisha upatikanaji wa vibali nya kazi kwa kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa e-permit ambapo kwa sasa vibali vinapatikana kati ya siku 1 hadi 3 kutoka siku 14; kuanzishwa kwa dirisha moja la kielektroiniki la uwekezaji; kuanzisha kituo cha mawasiliano cha uwekezaji na kanzidata ya ardhi yenye ukubwa wa hekta milioni 1.6; kufanyika kwa mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara; kusajili miradi 182 yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 3.5 inayotarajiwa kuzalisha ajira 43,782 ikilinganishwa na miradi yenye thamani ya dola za Marekani milioni 647.43 mwaka uliopita; kutolewa kwa leseni za BRELA 6,051; kuondolewa vikwazo visivyo nya kiforodha kati ya Tanzania na Kenya kutoka 64 hadi 46; na kuridhiwa kwa mikataba wa Eneo huru la biashara Afrika (Africa Continental Free Trade Area);

(v) **Kilimo:** Kuzalishwa kwa mbegu bora tani 50,589.43 na miche 13,568,422 ya mazao mbalimbali; kupatikana kwa mbolea tani 678,017; na kununuliwa kwa lita 113,066 za viuatilifu nya kudhibiti visumbufu nya milipuko. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 79.9 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 76.8 zimetumika.

Mafanikio ya Serikali ya awamu ya sita katika sekta ya kilimo ni pamoja na: Kuendelea kuimarika kwa sekta ya kilimo ambapo mashamba yenye ukubwa wa hekta 237,941.9 yamehakikiwa na kupimwa afya ya udongo; ujenzi wa vihenge; ukarabati na ujenzi wa skimu za umwagiliaji; kudhibiti nzige katika mikoa ya kaskazini; kufungua vituo nya mazao nje ikiwemo katika nchi za Kenya, Sudani Kusini, China, India, Ukraine, Saudi Arabia, Umoja wa Ulaya na Jumuuya ya Nchi za Afrika ya Kusini (SADC); kuimarisha hifadhi ya chakula nchini ambapo shilingi bilioni 129 zilitolewa kwa Wakala wa Uhifadhi wa Chakula (NFRA) na Bodi ya Mazao Mchanganyiko; kuimarika kwa bei za mahindi kwa wakulima ambapo Serikali ilinunua mahindi kwa shilingi 500 kwa kilo kutoka bei ya shilingi 300. Hali hiyo ilipelekea kuwa na ziada ya mahindi tani

950,000; kupatikana kwa masoko ya mbogamboga na matunda aina ya parachichi nchini Qatar; na kuanza kwa ujenzi wa kiwanda cha mbolea mkoani Dodoma kinachojengwa na kampuni ya Itracom Fertilizer Ltd kinacholenga kuimarisha upatikanaji wa mbolea nchini;

(vi) **Mifugo:** Kujengwa kwa majosho 49 katika Halmashauri 18 ambapo utekelezaji umefikia wastani wa asilimia 60; kuhimilishwa kwa ng'ombe 78,575 katika mikoa 10; na kukamilika kwa ukarabati wa mabwawa matatu (3) ya Chamakweza (Chalinze), Kimokoua (Longido) na Narakauo (Simanjiro). Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 10.5 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi milioni 186.8. Aidha, serikali ya awamu ya sita imefanikisha kuzinduliwa kwa viwanda vipyta sita vya kusindika maziwa ikiwemo Dodoma Halisi (Dodoma), Mabuki mini-dairy (Shinyanga), Misenani mlini-dairy (Mwanza) na Mbeya milk (Mbeya); kupatikana kwa masoko ya bidhaa za nyama ya mbuzi, kondoo na ng'ombe nchini Saudi Arabia pamoja na visiwa vya Comoro;

(vii) **Uvuvi:** Kujengwa kwa ofisi tano (5) za Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) katika Halmashauri tano (5) za Bagamoyo, Lindi Vijijini, Mkinga, Pangani na Chalinze; kujengwa kwa maabara moja (1) ya Utafiti ya Uvuvi katika kituo cha TAFIRI, Dar es Salaam; na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi na ununuzi wa meli za uvuvi katika bahari kuu. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 6.8 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 2.1 zimetumika. Mafanikio mengine ni kukamilika kwa kituo cha ukuzaji viumbe bahari, samaki, mwani, majongoo ya bahari, na kamba miti (kunduchi); kupatikana kwa masoko ya mabondo ya samaki nchini China; na kutenga shilingi bilioni 50 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari ya uvuvi Kilwa Masoko (Lindi);

(viii) **Uendelezaji wa Viwanda:** Kujengwa kwa mtambo wa kuyeyusha chuma (Galvanizing Plant) katika kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools Company (KMTC) ambapo ujenzi umefikia asilimia 80; na kuanza kwa uzalishaji katika Kiwanda

cha Kuunganisha Magari cha GF Trucks Motors katika eneo la Viwanda TAMCO - Kibaha ambapo jumla ya magari 245 yameunganishwa. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 46.4 zimetumika. Aidha, Serikali ya awamu ya sita imefanikisha kutolewa kwa leseni kwa kampuni 18 kupitia EPZA; kuanzishwa kwa viwanda vidogo 374; na kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa Industrial Trade and Logistics Centre - Kurasini;

(ix) **Madini:** Kukamilika kwa ujenzi wa Kituo cha Pamoja (One Stop Centre) Mirerani; kuanzishwa kwa masoko mapya matatu (3) ya madini ya Kiteto (Manyara), Mirerani (Arusha) na Mangaka (Mtwara); kuanzishwa kwa vituo vipyta 18 vya ununuzi wa madini; kujengwa kwa makao makuu ya Tume ya Madini; kununuliwa kwa mtambo mmoja (1) wa uchorongaji (Drill Rig) kwa ajili ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO); kukusanywa kwa mapato yasiyo ya kodi kiasi cha shillingi bilioni 588.04 kwa mwaka 2020/21; kununuliwa kwa vifaa vya utafiti wa jiosayansi kwa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania; na kuendelea na ujenzi wa vituo vitatu (3) vya umahiri vya Chunya, Songea na Mpanda. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 19.7 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi milioni 302.1 zimetumika;

Aidha, Serikali ya awamu ya sita imefanikisha kutolewa kwa leseni za uchimbaji madini 5,126 ikilinganishwa na 3,195 katika kipindi kama hicho mwaka uliopita; kukusanywa kwa mapato ya jumla ya shillingi milioni 336.5; ujenzi wa kiwanda cha kisasa cha kusafisha dhahabu Mwanza chenye uwezo wa kusafisha kilo 480 kwa siku; na kufutwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa wafanyabiasha watakaoleta dhahabu kwenye viwanda vya ndani;

(x) **Utalii:** Kuanza kuimarika kwa sekta ya utalii ambapo watalii waliotembelea nchini wamefikia 464,913; na kuanzishwa kwa mpango wa kutangaza utalii nchini ikiwemo kipindi cha Royal Tour kinacholenga kutangaza vivutio vya utalii na fursa za kiuchumi nchini. Kadhalika katika utekelezaji wa miradi mahususi chini ya kampeni ya maendeleo na mapambano ya UVIKO 19, **Shilingi bilioni 90.2 zimeelekezwa kugharamia**

sekta ya utalii ambayo iliathirika na UVIKO-19 baada ya mataifa mbalimbali duniani ambao ni washirika wetu kibialashara kuchukua hatua za kudhibiti kuenea kwa maambukizi ya UVIKO-19 ikiwemo kusitisha usafiri wa anga, na kuzuia watu kusafiri (wakiwemo watalii). Fedha hizo zitatumika kutekeleza yafuatayo:

Kuimarisha taasisi za sekta ya utalii zilizoathiriwa kwa kiasi kikubwa na UVIKO-19 zikiwemo TANAPA, TAWA na NCAA, TFS na NMT ikiwemo kuboresha miundombinu katika maeneo ya hifadhi na maeneo yanayozunguka hifadhi hizo kwa kukarabati barabara na kununua mitambo mitano (5) kwa ajili ya kujenga na kukarabati miundombinu hiyo katika hifadhi 13 za Taifa; Kuimarisha mifumo ya utangazaji wa fursa za utalii; Kubaini na kuwezesha ulipaji fidia kwa kodi na tozo zenye madhara makubwa kwa wafanyabiashara wa utalii kwa maeneo ya hifadhi za Taifa katika kipindi hiki cha UVIKO -19; na Kuanzisha vituo vitatu vya ukusanyaji maduhuli ambavyo vinajumuisha ujenzi wa malango ya kupokelea wageni katika maeneo yaliyopo katika hifadhi;

(xi) **Reli ya Kati:** Ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway- SGR) wa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) umefikia asilimia 93 na Morogoro – Makutupora Singida (km 422) umefikia asilimia 70; na kuanza kwa ujenzi wa kipande cha Mwanza – Isaka (km 341). Katika mwaka 2020/21, shilingi billioni 1,726.53 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi billioni 79.3 zimetumika;

(xii) **Kuboresha Usafiri wa Abiria na Mizigo katika Maziwa Makuu: Ziwa Victoria:** Kukamilika kwa ukarabati wa meli mbili (2) za New Butiama Hapa Kazi Tu na New Victoria Hapa Kazi Tu; kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza Hapa kazi Tu ambao umefikia asilimia 80.1; na kukamilika kwa ujenzi wa chelezo cha kujengea na kukarabati meli katika Bandari ya Mwanza. **Ziwa Tanganyika:** kusainiwa kwa mikataba kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli ya MT. Sangara. **Ziwa Nyasa:** kukamilika kwa ujenzi wa matishari mawili (2) yenye uwezo wa kubeba tani 1,000 kila moja; na

kukamilika kwa ujenzi wa meli moja mpya ya MV Mbeya II. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 48.5 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 4.9 zimetumika;

(xiii) **Usafiri wa anga:** Kuanza ujenzi wa uwanja wa ndege wa Msalato na kusainiwa kwa mikataba ya ujenzi wa viwanja vya ndege vya mikoa ya Shinyanga, Tabora, Sumbawanga pamoja na kuanza maandalizi ya maboresho ya kiwanja cha ndege cha Kigoma; kuendelea na ujenzi wa viwanja vya ndege vya Songea (asilimia 95), Mtwara (asilimia 61) na Iringa (asilimia 21.3); kukamilisha malipo ya awamu ya mwisho na kupokelewa kwa ndege tatu hivyo kufanya jumla ya ndege mpya zilizonunuliwa kufikia 11; Shirika la Ndege la Tanzania kupata kibali cha kwenda moja kwa moja nchi mbalimbali ikiwemo Falme za Kiarabu; na kusainiwa mkataba wa ununuzi wa ndege tano ambapo shillingi billioni 596.3 zimetolewa;

(xiv) **Barabara na Madaraja:** Mtandao wa barabara nchini umefikia kilomita 36,361.95 ambapo barabara kuu ni kilomita 12,215.58 na barabara za mikoa ni kilomita 24,146.37; na ujenzi wa madaraja 8,647 katika barabara kuu na za mikoa. Katika kipindi cha mwaka 2020/21 shilingi bilioni 1,552.8 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 295.8 zimetumika. Mafanikio mengine ya awamu ya sita ni pamoja na kuanza ujenzi wa barabara za kupunguza msongamano wa vyombo vya moto mkoani Dodoma. Barabara hizi ni pamoja na ujenzi wa barabara ya mzunguko katika jiji la Dodoma (Dodoma outer ring road) yenyewe urefu wa kilometra (112.3) ambapo ujenzi umeanza na unatarajiwa kukamilika 2023. Kazi nyingine ni maandalizi ya upanuzi wa barabara kutoka Dodoma kwenda Singida (km 50), Dodoma – Iringa (km 50), Dodoma – Arusha (km 50) na Dodoma – Morogoro (km 70); kuendelea kwa ujenzi wa barabara ya njia nane Kimara – Kibaha ambapo ujenzi umefikia takriban asilimia 95; kuendelea na ujenzi wa madaraja makubwa ya Tanzanite asilimia 97, Kigongo – Busisi asilimia 32 na Wami asilimia 65. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa barabara ya ndani ya jiji la Dodoma (Dodoma inner ring road; km 6.4) yanaendelea chini ya ufadhili wa Serikali ya Japan. Shilingi

bilioni 228.3 zilitolewa katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za mijini na vijijini ambapo kazi zilizokamilika ni ujenzi wa barabara za lami kilomita 27.1, barabara za changarawe kilomita 21.6, madaraja/Vivuko 62 na matengenezo ya barabara zenyе urefu wa kilomita 4,439.28. Vilevile, shilingi bilioni 1.5 zimetolewa kwa kila jimbo kwa ajili ya uwekaji wa lami kwenye barabara za miji.

Katika hatua nyingine, Serikali inatarajia kuanza ujenzi wa barabara mpya za kufungua fursa za kiuchumi zenyе urefu wa kilomita 879 katika sehemu mbalimbali nchini. Hii itasaidia kufungua zaidi Taifa kama kituo cha uzalishaji, biashara na usafirishaji kikanda. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Mshauri Elekezi inakamilisha mchoro (design) wa daraja la Jangwani ili kufanikisha maandalizi ya majadiliano baina ya Benki ya Dunia na Serikali ya ufadhilli wa ujenzi wa daraja hilo unaotarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka 2022/23.

(xv) **Uendelezaji wa Bandari:** Bandari ya Dar es Salaam: Awamu ya kwanza utekelezaji umefikia asilimia 95 ambapo gati Na. 1 – 7 limeongezwa kina hadi kufikia mita 14.5 na gati maalumu ya kuhudumia meli za magari (RoRo) limeanza kutumika. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 124.4 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 2.4 zimetumika; **Bandari ya Mtwara:** Ujenzi wa gati moja (1) lenye urefu wa mita 300 na sakafu ngumu umekamilika ambapo katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 65.47 zimetumika; na

Bandari ya Tanga: Uongezaji wa kina cha lango la bandari kutoka mita 4 hadi mita 13 na ujenzi wa gati mbili (2) kwenye kina kirefu umekamilika. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 20.41 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 11.6 zimetumika.

(xvi) **Nishati Miradi ya umeme:** Utekelezaji wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji - Julius Nyerere MW 2,115 umefikia asilimia 55.6, ambapo ujenzi wa handaki la kuchepushia maji umekamilika. Aidha, kazi nyingine zinazoendelea ni pamoja

na: ujenzi wa tuta kuu la bwawa; ujenzi wa njia za kupeleka maji kwenye mitambo; ujenzi wa jengo la mitambo; kingo za bwawa (Saddle Dams); kituo cha kuongeza nguvu ya umeme - Switch Yard; na utengenezaji wa mitambo tisa (9) ya kuzalisha umeme (turbines and generators) yenye uwezo wa kuzalisha MW 235 kila mmoja. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 1,171.53 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 81.4 zimetumika. Miradi mingine ni: Kuendelea na usambazaji umeme vijiji ambapo jumla ya vijiji 10,361 kati ya vijiji 12,317 vya Tanzania Bara sawa na asilimia 84.12 vimeunganishiwa umeme; mradi wa Rusumo MW 80 umefikia asilimia 81.2; Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme msongo wa KV 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita yenye urefu wa kilomita 55 umekamilika. Miradi hii katika mwaka 2020/21 imetumia jumla ya shilingi bilioni 1,067.0 na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 88.1 zimetumika.

Mafanikio mengine ni: kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Rufiji - Chalinze ambapo shilingi bilioni 112.9 zimetumika; kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya Singida - Arusha - Namanga ambapo utekelezaji umefikia asilimia 96.1; na miradi ya Ruhudji na Rumakali imepata ufadhilli kupitia Serikali ya China;

Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi: Hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Chongoleani - Tanga (Tanzania) - EACOP ni kuanza kwa taratibu za ujenzi wa mradi baada ya kukamilika kwa majadiliano na kusainiwa kwa Mkataba kati ya Nchi Hodhi na Wawekezaji (Host Government Agreement – HGA) na Mkataba wa Ubia (Shareholding Agreement – SHA). Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 262.7 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa sehemu ya hisa za Serikali, sawa na asilimia 45.4 ya lengo la mtaji wa shilingi bilioni 577.7;

Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia – Lindi: Kukamilika kwa ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha mradi katika maeneo ya Likong'o na Masasi ya Leo. Katika kipindi cha mwaka 2020/21 shilingi bilioni 2.6 zimetumika;

(xvii) **Afya:** Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi na ukarabati wa hospitali za rufaa za mikoa 19; kuendelea na ujenzi wa Hospitali 99 za Halmashauri ambazo zipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji; kutolewa chanjo kwa watoto 2,112,411 wenyewe umri wa chini ya miaka mitano, sawa na asilimia 101 ya lengo la watoto 2,091,378; upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma za afya umefikia asilimia 94; kununuliwa kwa mashine za Xray 11 za kidigitali ambazo zimesambazwa katika hospitali za mikoa 11; na kufungwa kwa mitambo 19 ya kuzalisha hewa ya Oksijeni katika hospitali za rufaa za mikoa. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 402.7 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 83.2 zimetumika. Aidha, Serikali imepata dozi 1,058,000 za chanjo ya UVIKO-19 aina ya Johnson and Johnson kutoka USA na dozi 1,065,000 aina ya Sinopharm kutoka COVAX facility ambapo hadi tarehe 20 Oktoba, 2021 jumla ya watu 959,377 ambao ni sawa na asilimia 90.6 walipata chanjo ya JJ na watu 8,591 walipata chanjo aina ya Sinopharm; shilingi bilioni 234 zilitolewa kwa ajili ya kununua dawa na shilingi bilioni 26.3 kwa ajili ya vifaa tiba; shilingi bilioni 7.9 kwa ajili ya kununua mashine ya kupasulia ubongo bila kupasua kichwa katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete; kuendelea na utekelezaji wa miradi 25 ya hospitali za rufaa za mikoa na kanda ambapo shilingi bilioni 159 zimetolewa; na kujengwa kwa vituo vya afya katika tarafa 221 ambapo shilingi billioni 37.5 zimetolewa; Kadhalika katika utekelezaji wa miradi mahususi chini ya kampeni ya maendeleo na mapambano dhidi ya UVIKO 19 katika sekta ya afya, **shilingi bilioni 466.9** zimepelekwa kwa ajili ya:

- (i) Kujenga na kukarabati miundombinu ya vyumba vya wagonjwa mahututi (ICU) katika hospitali 67;
- (ii) Kununua vifaa katika ICU za hospitali 66;
- (iii) Kujenga na kukarabati Miundombinu ya kutolea Huduma za Dharura (EMD) katika hospitali 115;
- (iv) Kununua vifaa katika miundombinu ya kutolea huduma za dharura za hospitali 119;

- (v) Kununua magari 253 ya kubeba wagonjwa (20 yenye kiwango cha huduma za juu - advanced ambulance na magari 233 yenye kiwango cha huduma ya msingi - basic ambulance);
- (vi) Kusimika mfumo wa usambazaji wa hewa tiba ya Oksijeni kwa wagonjwa katika wodi za hospitali 82;
- (vii) Kununua mitungi 5,782 ya hewa tiba ya Oksijeni na vifaa wezeshi vya utoaji hewa tiba katika hospitali 116;
- (viii) Kusimika mitambo tisa (9) ya kuzalisha hewa tiba;
- (ix) Kununua vifaa wezeshi vya utoaji (flowmeters) hewa tiba katika Hospitali 116;
- (x) Kununua seti 2,700 za vitanda vya wagonjwa vyenye godoro, kabati na meza;
- (xi) Kununua na kusimika mashine 85 za X-ray, CT-Scan 29, mashine saba (7) za huduma za uchunguzi wa moyo (Echo Cardiography) na MRI nne (4);
- (xii) Kununua mashine za upimaji gesi katika damu, vitendanishi vya upimaji wa UVIKO -19 na mashine za uchambuaji wa mazao ya damu salama;
- (xiii) Kugharamia uingizaji, utunzaji na usambazaji wa chanjo;
- (xiv) Kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu chanjo ya UVIKO;
- (xv) Kununua magari 214 kwa ajili ya huduma za chanjo katika mikoa na halmashauri na kampeni za kuhamasisha uchomaji wa chanjo;
- (xvi) Kugharamia ukarabati wa hospitali maalum ya mirembe na hospitali za rufaa za mikoa ya lindi, ligula-mtwara na kitetetabora;

(xvii) Kukarabati nyumba 116 za watoa huduma wa afya katika hospitali za rufaa za mikoa 26 na hospitali za wilaya 90 pamoja na kukarabati miundombinu kwenye hospitali sita (6) za Rufaa za Mikoa; na

(xviii) Kuwajengea uwezo watumishi wa sekta ya afya kwa kuwapatia mafunzo na kugharamia tafiti mbalimbali zinazohusu UVIKO-19.

(xviii) **Elimu:** Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu katika shule za msingi 998 na sekondari 719 kwenye Halmashauri 184; ujenzi wa maktaba saba (7) katika mikoa ya Kigoma, Rukwa, Kagera, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa na Tabora; na ujenzi wa vyuo vya VETA vya Chato, Gorowa (Manyara), Ngorongoro, Simanjiro na Karagwe. Shughuli nyingine ni kuendelea na utekelezaji wa programu ya Elimumsingi Bila Ada; na kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 415 kwa wanafunzi 149,472 wa Elimu ya Juu. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 683.0 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 152.9 zimetumika. Mafanikio mengine ni pamoja na kusainiwa kwa mkopo wa Benki ya Dunia wa shilingi bilioni 972 kwa ajili ya uboreshaji elimu kwenye vyuo vikuu 14; kuanza ujenzi wa chuo kikubwa cha ufundi Dodoma ambapo shilingi bilioni 18 zimetumika; na kutolewa kwa shilingi bilioni 40 kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika wilaya 25.

Vilevile, kipitia kampeni ya maendeleo na mapambano dhidi ya UVIKO19, sekta ya elimu imetengewa **Shilingi bilioni 368.9 ambapo:** Shilingi **bilioni 304** zitatumika kupunguza msongamano madarasani na kwenye mabweni kwa kujenga vyumba vya madarasa 15,000 katika shule za sekondari na shule za msingi shikizi pamoja na madawati 641,850; na kujenga mabweni 50 kwa ajili ya wanafunzi wenyе ulemavu; na **Shilingi bilioni 64.9** zitaelekezwa kukamilisha Vyuo vya Ufundu Stadi - VETA sita (6) vya mikoa na 26 vya Wilaya; kuchapisha vitabu vya nukta nundu 10,812 kwa ajili ya wanafunzi wasioona; na kugharamia vifaa kwa ajili ya wanafunzi 486 wenyе mahitaji maalum katika vyuo 11;

(xix) **Maji:** Upatikanaji wa huduma ya maji umeimarika ambapo hadi Juni, 2021 imefikia wastani wa asilimia 72.3 vijiji kutoka wastani wa asilimia 70.1 Juni, 2020 na mijini asilimia 86 kutoka asilimia 84. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: ukarabati wa vituo 159 vya kufuatilia mwenendo wa maji; na kukamilika kwa miradi 666 ilionufaisha wananchi 3,820,180 waishio vijiji. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 495.3 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 99.8 zimetumika; Kutolewa kwa shilingi bilioni 352 kwa miradi 328 (mijini 17 vijini 311) ambapo miradi yenye thamani shilingi bilioni 109.13 imekamilika na kunufaisha wananchi 1,975,197 vijini na 372,002 mijini; na maandalizi ya mradi wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Dodoma. Serikali pia inaendelea na utekelezaji wa miradi mahususi chini ya kampeni ya maendeleo na mapambano dhidi ya UVIKO 19 ambapo **Shilingi bilioni 139.4 zitaghamaria huduma za maji safi ikijumuisha:** Shilingi bilioni 101.7 kwa ajili ya ukarabati, upanuzi na uongezaji wa miundombinu ya usambazaji wa maji na Shilingi bilioni 37.6 kwa ajili ya kununua mitambo ambayo ni mitambo 25 ya kuchimba maji ili kuongeza kasi ya uchimbaji wa visima vinavyohitajika katika maeneo mbalimbali nchini, seti tano (5) za mitambo ya uchimbaji na ujenzi wa mabwawa ili kuongeza kasi ya ujenzi wa mabwawa katika maeneo yenye uhitaji; na seti nne (4) ya vifaa vya uchunguzi wa maji chini ya ardhi ili kupata maeneo sahihi ya kuchimba visima;

(xx) **Habari, Mawasiliano na TEHAMA:** Kukamilika kwa ujenzi wa mkongo wa taifa kwa kilomita 409 katika mgawanyo ufuatao: Kilomita 72 kuunganisha nchi ya Msumbiji kuititia mpaka wa Mtambaswala katika Mkoa wa Mtwara na kukamilika kwa kituo cha kutoa huduma za mawasiliano, Kilomita 72 Kuunganisha Watumiaji wa Mwisho (Last mile connectivity) katika Ofisi za Serikali na kilomita 265 Awamu ya kwanza Manyoni – Kambi Katoto (Chunya); Kukamilika kwa ukarabati wa kilomita 105 za ujenzi wa mkongo Arusha – Namanga kuititia miundombinu ya TANESCO; Ununuzi wa magari 47 kwa ajili ya kuhudumia shughuli za mkongo; kukamilika kwa uwekaji wa miundombinu ya anwani za makazi katika kata 18 ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza; na kubandikwa kwa vibao 78,138 vya namba za nyumba katika

Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Katika kipindi cha mwaka 2020/21 shilingi bilioni 16.0 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 8.4 zimetumika;

(xxi) **Mahakama na Utawala wa Sheria:** Kuimarisha Mifumo ya Utoaji Haki na Usimamzi wa Sheria ambapo jumla ya mashauri 104,441 yalisikilizwa katika ngazi mbalimbali za mahakama; kuteuliwa kwa Majaji wapya saba (7) wa mahakama ya rufaa, Majaji 21 wa mahakama kuu na kuajiriwa kwa mahakimu 245; ujenzi wa Vituo Sita Jumuishi vya Utoaji huduma za mahakama katika mikoa ya Arusha, Dar es salaam, Dodoma, Morogoro, na Mwanza; kukamilika kwa ujenzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Katavi na Mahakama za Wilaya za Bunda, Chemba na Bahi; kuanza ujenzi wa Mahakama za Mwanzo 18 katika maeneo mbalimbali nchini; kuendelea na ukarabatati wa Mahakama Kuu moja (1), mahakama mbili (2) za hakimu mkazi na tisa (9) za wilaya; kufungua Ofisi za Mashtaka za wilaya za Kilombero, Serengeti na Karagwe; na kufuta Mashkata 467 yasiyo na tija. Aidha, Serikali ipo katika majadiliano na Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata fedha za kuendelea kujenga na kuimarisha miundombinu ya mahakama. Kiasi kilichoombwa ni dola za Marekani milioni 75 ambazo zinatarajiwaa kupatikana katika mwaka huu wa fedha;

(xxii) **Ulinzi na Usalama:** kutolewa kwa vibali vya kuajiri jumla ya askari 5,403 kwa ajili ya Jeshi la Polisi (askari 4,103), Jeshi la Magereza (askari 700) Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (askari 250) na Idara ya Uhamiaji (askari 350); Kuendelea na ujenzi wa nyumba 119 za Maafisa na Askari wa Jeshi la Magereza zenye uwezo wa kuhudumia familia 210; kuendelea na ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika eneo la Kikombo, Jijini Dodoma.

(xxiii) **Utumishi wa umma:** Watumishi 29,900 wameajiriwa, watumishi 180,830 wamepandishwa vyeo na kulipwa stahili zao, watumishi 8,202 wamebadilishiwa kada, watumishi 30,228 wamelipwa malimbikizo ya madeni ya jumla ya shilingi bilioni 55.75 na kupunguza makato ya kodi ya PAYE kufikia asilimia 8 kutoka asilimia 9; na mifuko ya hifadhi ya jamii (PSSSF na

NSSF) kulipa mafao ya shilingi bilioni 1,540 na pensheni shilingi bilioni 446.93. Aidha, Serikali imeanza mchakato wa kutoa hatifungani maalum zisizo taslimu (non-cash special Bonds) za miaka 8 hadi 25 kwa ajili ya kulipa madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii ambapo kiasi cha shilingi bilioni 2,176.74 kilichohakikiwa cha deni la Pre-1999 kimeridhiwa kutolewa kuanzia Desemba 2021 na deni lilitlobakia linaendelea kufanyiwa uhakiki;

(xxiv) **Kaya maskini:** Kuimarisha maisha ya kaya maskini kuititia TASAF ambapo kaya 879,670 zilinuifaika kwa kupatiwa jumla ya shilingi bilioni 71.395; sambamba na utekelezaji wa miradi mahususi chini ya kampeni ya maendeleo na mapambano ya UVIKO 19 ambapo **Shilingi bilioni 5.5** zitatumika kuwezesha kaya masikini 34,375 kukidhi mahitaji ya msingi kuititia TASAF ikiwepo upatikanaji wa vifaa kinga;

(xxv) **Kuwezesha Wajasiriamali Wadogo:** Kupitia kampeni ya maendeleo na mapambano ya dhidi ya UVIKO 19, Serikali itawawezesha makundi maalum ya wajasiriamali wadogo ikijumuisha vijana, wanawake na wenyewe ulemavu kwa kuwajengea vibanda vya kufanya biashara ili kupunguza msongamano usio wa lazima ambapo shilingi bilioni 5 zitatumika;

(xxvi) **Ardhi:** Kusajiliwa kwa hati miliki 41,533 ikilinganishwa na hati miliki 34,588 katika kipindi kama hicho mwaka 2020; kushughulikiwa kwa migogoro ya ardhi 745 kwa njia za kiuatwala na mashauri 13,991 kwa kutumia mabaraza ya ardhi; kupimwa kwa viwanja 232,596 na mashamaba 353; Kutambuliwa, kupangwa na kupimwa kwa vipande 87,636 vya ardhi katika halmashauri 24; na kuandaliwa kwa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 51 vilivyopo katika mkuza wa bomba la mafuta ghafi kutoka Uganda hadi Tanga. Aidha, mashamba 11 yenye ekari 24,156 yamebadilishiwa matumizi kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwemo uwekezaji. Katika mwaka 2020/21, shilingi bilioni 5.4 zimetumika na katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22, shilingi bilioni 2.8 zimetumika;

(xxvii) **Sanaa na Burudani:** Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ambao umetengewa shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kusaidia timu za Taifa; COSOTA kutengewa bajeti ili kuiwezesha kukusanya makusanyo ya wasanii; na kufutiwa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa nyasi bandia;

(xxviii) **Ushirikiano na Washirika wa maendeleo:** Kupatikana kwa misaada na mikopo nafuu ya shilingi trilioni 1.447; kusainiwa kwa mikataba 31 na Washirika wa maendeleo yenye thamani ya shilingi trilioni 6.3;

(xxix) **Kuimarisha diplomasia:** Kufunguliwa kwa ubalozi mpya wa Tanzania Vienna - Austria; kufunguliwa kwa Konseli Kuu katika miji ya Lubumbashi katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Guangzhou nchini China; na kuridhiwa kwa Mkataba wa Uanzishwaji wa Eneo Huru la Biashara Africa (AfCFTA); na

(xxx) **Makao Makuu ya Serikali Dodoma:** Hatua za kuimarisha makao makuu ya Serikali Dodoma zinaendelea ambapo vibali vya ujenzi vimetolewa na michoro ya ubunifu kwa ajili ya kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa ofisi 22 za Wizara na Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekamilika na kiasi cha shilingi billioni 300 zimetengwa kwenye bajeti ya mwaka 2021/22 kwa ajili ya kuanza ujenzi huo.

22. Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo mwaka 2020/21 na robo ya kwanza ya mwaka 2021/22 yameainishwa katika kitabu cha Mapendekezo ya Mpango (**Sura ya Tatu**).

2.4 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti na Hatua na Kukabiliana Nazo

23. Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Mwongozo wa mwaka 2021/22 ulikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo: uwasilishaji wa mahitaji makubwa kuliko ukomo uliotolewa; kupungua kwa shughuli za kibashara na kiuchumi kutokana na athari za UVIKO -19; kutoandaliwa kwa miradi inayokidhi vigezo vya kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia

kati ya Sekta ya Umma na Binafsi; mabadiliko ya viwango vya riba katika masoko ya fedha ya kimataifa; na upungufu wa rasilimali watu hususan wahandisi wa kusimamia utekelezaji wa miradi pamoja na wataalam wa uendeshaji wa mitambo na vifaa vinavyotumia teknolojia ya kisasa.

24. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa Mpango na Bajeti, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na changamoto hizo zikiwemo: Kujenga uwezo wa Mafungu katika kuwianisha mipango na ukomo wa bajeti uliotolewa; kuendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa biashara duniani ili kutumia fursa zilizotokana na athari za UVIKO-19; kuchukua hatua za kisera na kiutawala kuimarisha sekta zilizoathirika na UVIKO-19; kuendelea kujenga uwezo wa Mafungu ili kuyawezesha kuandaa miradi inayokidhi vigezo vya kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP; kuendelea kutekeleza miradi ya maendeleo yenyewe kuchachua shughuli za kiuchumi pamoja na kujenga mazingira wezeshi ya kuvutia biashara na uwekezaji; na kuendelea kuajiri wahandisi na wataalam watakaosimamia utekelezaji na uendeshaji wa miradi.

25. Kwa kumalizia eneo hili la **Utekelezaji wa Baadhi ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2020/21 na Robo ya Kwanza ya Mwaka 2021/22 na Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita naomba nisisitize mambo matatu:-**

(i) Kwa maafisa manunuzi, Maafisa Masuuli na wasimamizi wa miradi hii, tunataka uzingatiaji wa sheria na maelekezo katika utekelezaji wa miradi hii, tunataka ubora wa miradi, tunataka **“Value for Money”** katika miradi yote.

(ii) Kwa wote wanaohusika na ufuutiliaji wa utekelezaji wa miradi kitengo cha M & E, Expenditure tracking, Sekretariat za mikoa yote tufuatilie miradi kila siku, sio kusubiri ziara za viongozi, wala sio kusubiri kazi iharibike. Wakaguzi wa ndani tubainishe dosari kila zinapojitokeza, kwa ambao hawataona dosari katika maeneo yao mpaka wakaguzi wa nje waje

wayabainishe watakuwa wamepoteza sifa za kuwa kwenye nafasi hizo.

(iii) Niwapongeze wote mnaohusika na kukusanya mapato ya Serkali. Tuendelee kuweka mkazo katika kukusanya mapato. Bado kuna ulegevu katika ukusanyaji wa mapato katika baadhi ya maeneo. Kuna UVUJAJI Mkubwa wa makusanyo ya maduhuli ya serikali katika Serikali za mitaa na ulegevu wa matumizi ya EFD (Tunashauriana bei ya risiti na isiyo na risiti). Aidha, kuna vitendo vya rushwa katika baadhi ya ukusanyaji wa kodi kutoka kwa walipa kodi wakubwa (tunashauriana kiasi gani kiende serikalini na kiasi gani kije mifukoni mwetu). Tuviache vitendo hiyyo mara moja.

3.0 MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/23

26. Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya msingi yatakayowezesha kufikia shabaha za uchumi jumla ni pamoja na: kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za maendeleo; kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili; kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya kimataifa; kuendelea kuwa na utoshelevu wa chakula nchini; na uwepo wa amani, usalama, umoja, utulivu wa ndani na nchi jirani.

27. Mheshimiwa Mwenyekiti, shabaha na malengo ya uchumi jumla yatakayozingatiwa katika muda wa kati ni pamoja na:-

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa kutoka asilimia 4.8 mwaka 2020 hadi asilimia 5.0 mwaka 2021 na kuendelea kukua hadi asilimia 5.2 mwaka 2022;

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani (ikijumuisha mapato ya Halmashauri) kufikia asilimia 16.3 ya Pato la Taifa mwaka 2022/23 na 2023/24;

- (iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 13.8 ya Pato la Taifa mwaka 2022/23 kutoka matarajio ya asilimia 12.9 mwaka 2021/22;
- (v) Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na
- (vi) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

3.1 Mfumo wa Awali wa Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2022/23

28. Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2022/23, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shillingi billioni 39,387.5, ikilinganishwa na shillingi bilioni 36,681.9 mwaka 2021/22. Kiasi kilichoongezeka ni sawa na asilimia 7.4 kutokana na mahitaji ya kugharamia miradi mbalimbali; ongezeko la mishahara ya watumishi wa umma; ajira mpya pamoja na fursa zilizopo za mapato ya ndani na nje. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani (yakijumuisha mapato ya Halmashauri) yanakadiriwa kufikia shillingi bilioni 28,567.9, sawa na asilimia 72.5 ya bajeti yote. Aidha, Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia shillingi bilioni 3,043.5, sawa na asilimia 7.7 ya bajeti yote. Serikali inatarajia kukopa shillingi bilioni 5,354.3 kutoka soko la ndani ambazo zinajumuisha shillingi bilioni 3,300.0 kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali zinazoiva na shillingi bilioni 2,054.3 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Vilevile, mikopo ya masharti ya kibiashara kutoka nje inatarajiwa kuwa shillingi bilioni 2,421.9.

29. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, Matumizi ya Serikali yanakadiriwa kufikia shillingi bilioni 39,387.5, ambapo shillingi bilioni 24,708.6 ni matumizi ya kawaida na shillingi bilioni 14,678.9 ni matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya maendeleo, shillingi bilioni 11,635.4 ni fedha za ndani na shillingi bilioni 3,043.5 ni fedha za nje.

30. Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu sera za mapato na matumizi katika muda wa kati yapo katika **Sehemu ya Kwanza, Sura ya Tatu ya Kitabu cha Mwongozo.**

3.2 Maelekezo Mahsusini ya Mwongozo

31. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23 umeainisha maelekezo mbalimbali ambayo Maafisa Masuuli watatakiwa kuyazingatia wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye Mwongozo wakati wa uandaaji, utekelezaji, na ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti. Miongoni mwa maelekezo hayo ni kama ifuatavyo:

3.2.1 Uandaaji

- (i) Kutenga bajeti kwa ajili ya shughuli za ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ);
- (ii) Kuandaa bajeti ambayo ni shirikishi kwa kuzingatia Muundo wa Mapato na Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) na ratiba iliyobainishwa kwenye Mwongozo;
- (iii) Kuimarisha Kamati za Bajeti na kuhakikisha kuwa Kamati hizo zinafanya kazi kwa mujibu wa Kifungu 18(2) cha Sheria ya Bajeti Sura 439;
- (iv) Kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea kutekelezwa inatengewa fedha kwa ajili ya kuikamilisha kabla ya kuanza miradi mipya;
- (v) Halmashauri zenye mapato yasiyolindwa ya shilingi bilioni tano au zaidi kutenga asilimia 60 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, ikijumuisha asilimia 10 kwa ajili ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu na asilimia 10 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazosimamiwa na TARURA;

(vi) Halmashauri zenye mapato yasiyolindwa chini ya shilingi bilioni tano kutenga asilimia 40 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ikijumuisha asilimia 10 kwa ajili ya Mikopo ya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu;

(vii) Kupata idhini kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Fedha kabla ya kupokea mikopo, misaada na dhamana kwa mujibu wa kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134;

(viii) Kuzingatia viwango vya ukomo wa bajeti vitakavyotolewa na Serikali;

(ix) Kutumia Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS) katika kuandaa na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kuzingatia Waraka wa Hazina Na. 5 wa mwaka 2020/21;

(x) Kuandaa na kuwasilisha mikakati ya uwekezaji ya taasisi, sera ya gawio (dividend policy) na mipango ya biashara katika Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya kupata idhini;

(xi) Kukamilisha uhuishaji wa Mipango Mikakati na wasifu wa taasisi ili iendane na vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); na

(xii) Kuandaa bajeti ya maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26).

3.2.2 Utekelezaji

(i) Kuhakikisha mapato yote katika Wizara na Taasisi za Umma yanaendelea kukusanya kupitia Mfumo wa Government e-Payment Gateway (GePG);

(ii) Kuzingatia maelekezo ya Waraka wa Hazina Na. 2 wa Mwaka 2019 unaohusu utaratibu wa kuomba, kuhamisha, kupokea, kutumia, kuhasibu na kutoa taarifa za utekelezaji

wa miradi ya D-Fund na matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Fedha Zinazopelekwa Moja kwa Moja kwenye Miradi;

(iii) Kuhakikisha ununuzi wa umma unafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 na Kanuni zake kwa kufanya ununuzi wa pamoja na kutumia Mwongozo wa Matumizi ya Force Account wa Mei 2020 ili kupata thamani halisi ya fedha;

(iv) Kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (TANePS) katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi za ujenzi;

(v) Kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Pili ya ujenzi wa Ofisi za Wizara katika Mji wa Serikali Mtumba Dodoma;

(vi) Kuzingatia Sheria ya Msajili wa Hazina, Sura 370 kwa kutenga na kuwasilisha katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi ya Taasisi na asilimia 70 ya ziada ya mapato baada ya kutoa matumizi yaliyoidhinishwa;

(vii) Kuzingatia Waraka wa Hazina Na. 7 wa Mwaka 2020/21 kuhusu utekelezaji wa miradi ya Ubia Bainya Sekta za Umma na Binafsi (PPP); na

(viii) Kuendelea kutekeleza Blueprint kwa kuboresha sheria mbalimbali ili kuweka misingi mizuri ya kusimamia mazingira bora ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini.

3.2.3 Ufuatiliaji na Tathmini

(i) Kuandaa mpango kazi na mtiririko wa fedha wa utekelezaji wa bajeti kupitia mifumo ya CBMS na PlanRep;

(ii) Kuandaa taarifa za utekelezaji kwa kuzingatia muundo ulioainishwa katika Sura ya Pili ya Sehemu ya Pili ya Mwongozo. Taarifa za utekelezaji za kila robo ya mwaka ziwasilishwe katika muda wa siku 30 baada ya kukamilika kwa

robo ya mwaka husika. Vilevile, taarifa za utekelezaji za mwaka ziwasilishwe kabla ya tarehe 15 Oktoba ya mwaka wa fedha unaofuata;

(iii) Kujenga uwezo wa watumishi katika vitengo vya ufuatiliaji na tathmini na kuandaa mpango wa kurithisha watumishi wapya maarifa ili kuwa na mfumo endelevu wa ufuatiliaji;

(iv) Kuendelea kutumia taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kuboresha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mpango na bajeti; na

(v) Kuongeza matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali ili kuongeza ufanisi ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa wataalam wa ndani kwenye eneo la usalama wa mifumo.

32. Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu maelekezo mahsusii ya Mwongozo yanapatikana katika Sehemu ya Pili, Sura ya Kwanza na Sura ya Pili ya Kitabu cha Mwongozo.

4.0 MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2022/23

33. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 ni wa pili katika utekelezaji Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2021/22 – 2025/26, wenye dhima ya “Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu”. Katika mwaka 2022/23, Maeneo mahsusii ya kipaumbele ni:

(i) **Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi.** Eneo hili linajumuisha miradi ambayo itajikita katika: kujenga jamii yenye uwezo wa kushindana kikanda na kimataifa; kuimarisha utulivu wa uchumi jumla; kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji; kuimarisha Tafiti na Maendeleo (R&D) pamoja na uhawilishaji wa teknolojia kutoka nje; na kuendeleza miundombinu na huduma katika maeneo ya reli, barabara, madaraja, usafiri wa maji, usafiri wa anga, TEHAMA, nishati, bandari na viwanja vya ndege;

- (ii) **Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma:** Eneo hili linajumuisha miradi ya viwanda inayolenga kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na madini pamoja na kuzalisha bidhaa zitakazotumia malighafi na rasilimali zinazopatikana kwa wingi nchini. Aidha, eneo hili linajumuisha miradi na programu zinazolenga kuboresha sekta ya utalii, huduma za fedha na bima;
- (iii) **Kukuza Biashara na Uwekezaji:** Eneo hili linajumuisha programu zitakazoimarisha masoko ya ndani na kutumia fursa za masoko kikanda na kimataifa. Masoko yanayolengwa ni yale yatakayotoa fursa kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini ikiwemo bidhaa na huduma zitokanazo na kilimo, viwanda na utalii. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (Blue Print);
- (iv) **Kuchochea Maendeleo ya Watu:** Eneo hili linajumuisha utekelezaji wa miradi inayolenga kuboresha maisha ya watu ikiwemo kuboresha elimu na mafunzo katika ngazi zote; afya na ustawi wa jamii; hifadhi ya jamii; sensa ya watu na makazi; huduma za maji na usafi wa mazingira hususan mradi mkubwa wa maji kutoka ziwa Victoria hadi jiji la Dodoma; mipango mijji, nyumba na maendeleo ya makazi. Aidha, eneo hili linajumuisha kuimarisha mfumo wa sheria na taasisi za utoaji haki na usimamizi wa utawala bora, ulinzi na usalama na utulivu wa ndani na nje ya nchi, mapambano dhidi ya rushwa na ujisadi ikiwemo kuimarisha utoaji haki pamoja na ukuzaji wa maadili. Vilevile, Serikali itaendelea na utekelezaji wa shughuli za kuhamishia makao makuu ya Serikali Jijini Dodoma ikiwemo awamu ya pili ya ujenzi wa ofisi na miundombini katika mji wa Serikali Mtumba; na
- (v) **Kuendeleza Rasilimali Watu:** Eneo hili linajumuisha programu na mikakati inayolenga kuendeleza ujuzi wa rasilimali watu nchini, kuanzia ngazi za elimu ya awali hadi elimu ya juu ikiwemo kuwawezesha vijana kujiajiri. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini kwa kutoa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kupitia Programu ya Uanagenzi kwa vijana, kutoa mafunzo, kurasimisha na

kutoa vyeti kwa vijana waliopata ujuzi nje ya mfumo rasmi pamoja na kutoa mafunzo ya vitendo mahali pa kazi kwa wahitimu wa elimu ya juu. Vilevile, eneo hili linajumuisha hatua za kuboresha viwango vya utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na ujuzi adimu kwa lengo la kuongeza tija na ushindani wa wananchi katika kutumia rasilimali zilizopo nchini ili kuleta maendeleo.

34. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 utajumuisha miradi ya kielelezo inayoendelea ambayo utekelezaji wake unatarajiwu kuwa na matokeo mapana na ya haraka katika uchumi. Miradi hiyo ni: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway - SGR); Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere – MW 2,115; Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (LNG) – Lindi; Mradi wa Magadi Soda Engaruka; Mradi wa Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Chuma – Liganga; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Ruhudji (MW 358) - Njombe; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Rumakali (MW 222) - Njombe; Ujenzi wa Madaraja Makubwa na Barabara za Juu za Daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza) na Daraja la Jipyä la Selander (Tanzanite - Dar es Salaam); Bandari ya Uvuvi (Kilwa) na Ununuvi wa Meli za Uvuvi; Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi; Utafutaji wa Mafuta na Gesi katika Kitalu cha Eyasi Wembere; Utafutaji wa mafuta na gesi katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini; Kanda Maalumu za Kiuchumi ikiwemo Eneo Maalumu la Kiuchumi Bagamoyo; Ujenzi wa reli ya Mtwara - Mbamba Bay na matawi yake ya Mchuchuma na Liganga kwa kiwango cha SGR; Mradi wa kutoa maji wa Ziwa Victoria hadi Dodoma; na Kuongeza Rasilimali Watu yenye Ujuzi Adimu na Maalumu (Ujuzi wa Kati na Wabobezi) kwa maendeleo ya viwanda na ustawi wa jamii ikiwemo ujenzi wa shule 26 za wasichana katika mikoa yote.

Katika Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu, Taifa linahitaji ushiriki wa sekta binafsi yenye uwezo wa kuchangia katika utekelezaji wa Mpango. Kwa msingi huo,

Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa sekta binafsi kwa kufanya kazi maoni na ushauri wa kukabiliana na changamoto za sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango na miradi ya maendeleo.

35. Mheshimiwa Mwenyekiti, Maeleo ya kina kuhusu Maeneo ya Kipaumbele kwa mwaka 2022/23 yapo katika **Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango (Sura ya Nne)**.

5.0 HITIMISHO

36. Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mwongozo na Mpango yatawezesha Mafungu kuandaa Mipango na Bajeti kwa Mwaka 2022/23. Kutokana na Mapendekezo haya, Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/23. Aidha, wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake.

37. Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maeleo hayo naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/23.

38. Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, ahsante sana kwa wasilisho zuri sana ambalo ninaamini sasa Waheshimiwa Wabunge liko ndani ya vishkwambi vyetu, vikiwemo vitabu hivi vyote viwili, ambazo ni Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2022/2023 na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023, lakini pia Hotuba ya Waziri wa Fedha

na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchomba ambaye ametoka kuiwasilisha muda si mrefu hapa mbele.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninaomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Anakuja Mwenyekiti mwenyewe. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, una nusu saa, jitahidi. Karibu. (*Makofii*)

MHE. DANIEL S. BARAN – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 113 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa hii ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/2023 unaopendekezwa ni Mpango wa Pili katika mfululizo wa utekelezaji wa Mpango wa Tatoo wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022-2025/2026) uliobeba Dhima ya "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu". Hivyo, ni wazi kwamba, mapendekezo ya mpango huu yanalenga kuweka mazingira mahsusii ya kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2022/2023 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023 yaliyowasilishwa na Serikali na kutoa ushauri wake kwenye maeneo yafuatayo; Hali ya Uchumi, Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/2021 na robo ya Kwanza ya Mwaka 2021/2022, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka

wa Fedha 2022/2023 pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yaliyowasilishwa mbele yako leo yanaonyesha nia thabiti ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuiletea maendeleo nchi yetu na kujenga uchumi shindani. Mapendekezo haya ya mpango kweli yanadhihirisha maneno ya wananchi kwamba Mama anaupiga mwingu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mapitio ya Hali ya Uchumi Jumla katika Mwaka 2021 Kamati imefanya uchambuzi wa mwenendo wa viashiria vyote vya hali ya uchumi katika mwaka 2021 ili kuangalia mafanikio na changamoto za kiuchumi zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mpango kwa mwaka 2020/21. Kwa kuzingatia uchambuzi wa Kamati kuhusu mwenendo wa viashiria vya hali ya uchumi, Kamati inapenda kutoa ushauri ufuatao: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ukuaji wa Uchumi wa Taifa. Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2021, Uchumi wa Taifa ulikua kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. sekta zilizokua kwa kasi kubwa ya ukuaji ni pamoja na habari na mawasiliano asilimia 10.7, umeme asilimia 9.6, maji safi na taka asilimia 8.7. Aldha, malazi na huduma za chakula zillikuwa kwa kasi ndogo zaidi kuliko sekta nytingine kwa asilimia 1.0.

Kushuka kwa ukuaji wa uchumi kumechangwa kwa kiasi kikubwa na kucheleva kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi pamoja na athari za UVICO-19 hasa katika shughuli za kiuchumi kama za hoteli, utalii, huduma za chakula, afya na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza vyema mapambano dhidi ya UVICO-19 kwenye uchumi wa Taifa letu pamoja na maendeleo ya watu. Juhudi alizoziweka

Mheshimiwa Rais katika upatikanaji wa Fedha za Mkopo wa Masharti nafuu wa Shilingi trillioni 1.3 kutoka *IMF* na uwekaji wa vipaumbele vya matumizi ya fedha hizo kwa kulishirikisha Bunge lako kupitia Kamati ya Bajeti ni za kupongezwa na Kamati inaamini juhudhi hizo zitasaidia kwa kiasi kikubwa kupambana na UVIKO-19 pamoja na kuboresha ustawi wa Taifa letu. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inatumia vizuri fedha hizo katika kutekeleza vipaumbele viliviyowekwa. Pia, iendelee kuziwezesha kifedha na kuweka mipango mizuri ya kukuza sekta kama za kilimo, kufufua sekta ya utalii na sekta zingine kama vile sekta ya afya, biashara na uwekezaji ambazo zimeathirika na UVIKO-19.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mfumuko wa bei mapendekezo ya mpango yanaonesha kuwa mfumuko wa bei umeendelea kuimarika na kuwa ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Aidha, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 4 mwezi Septemba 2021 ikilinganishwa na asilimia 3.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Hata hivyo mapendekezo ya mpango yaliyowasilishwa yameeleza kwamba, sababu za kupanda kwa mfumuko wa bei ni kutokana na kuongezeka kwa mzunguko wa fedha usioendana na bidhaa zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2020/2021 sababu zilizochangia kupungua kwa mfumuko wa bei nchini ni upatikanaji wa chakula cha kutosha, kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia, uwepo wa utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani na sarafu nyingine duniani, pamoja na sera madhubuti ya fedha na sera ya bajeti. Hata hivyo, shilingi trillioni 1.3 kutoka *IMF* zilizoingia katika uchumi kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO-19, katika fedha hizo zaidi ya Shilingi bilioni 500 zitapelekwa kwenye miradi ya ujenzi, ambazo zimesababisha mfumuko wa bei. Aidha, kutokana na uwepo wa taarifa ya kuwa na hali ya ukame katika msimu wa 2021/2022, pamoja na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia inaashiria kwamba, katika muda wa katika kuna hatari kubwa ya bei za bidhaa kupanda maradufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha viwanda vya ndani vya uzalishaji wa bidhaa za ujenzi kuzalisha katika uwezo wao wa juu (*Full capacity*). Kuendelea kuijengea uwezo *NFRA* kifedha, kimitaji na kimiundombinu endapo kutakua na ukame *NFRA* iwe na hifadhi ya chakula cha kutosha. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kudhibiti bei ya mafuta ya petroli katika soko la ndani na kuendelea kupambana na wahujumu uchumi wanaoficha bidhaa ili bei ipande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Deni la Serikali mapendekezo ya mpango yanaonyesha kuwa hadi Juni 2021, Deni la Serikali lilitifika Shilingi trillioni 64.498 ikiltinganishwa na Shilingi trillioni 56.45 Juni 2020, sawa na ongezeko la asilimia 14.3. Kati ya Deni hilo, kiasi cha Shilingi trillioni 45.5 ni deni la nje na Shilingi trillioni 18.9 ni deni la ndani. Sababu ya ongezeko hilo linatokana na kupokelewa kwa fedha za mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Kamati imebaini kwamba, Serikali inatarajia katika muda wa kati kuongeza kukopa mikopo yenye masharti ya kibashara kutoka asilimia 8.9 hadi asilimia 44.5. Utuftuti mkubwa wa mikopo ya kibashara na mikopo ya masharti nafuu ni muda wa kuanza kulipa (*grace period*). Mikopo ya kibashara ina muda mfupi wa mwaka mmoja hadi miwili na deni huiva ndani ya miaka mitatu wakati mikopo ya masharti nafuu ni miaka saba hadi 8 na huiva ndani ya miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tathmini hiyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo; Kwanza, fedha za mikopo yote ya kibashara zielekezwе kwenye miradi yenye sura ya kibashara na inayoweza kuzalisha mapato kwa muda mfupi. Pili, miradi yote inayotumia muda mrefu kukamilika na kuleta faida itumie mikopo yenye masharti nafuu na tatu, kukamilisha uhakiki na kulipa Madeni ya Wazabuni, Wakandarasi na Watoa huduma ili kudhibiti Deni la Serikali liendelee kuwa himilivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mwenendo wa mikopo ya sekta binafsi. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 4.3 katika mwaka 2020/2021 ikiltinganishwa

na wastani wa asilimia 8.1 katika mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, riba ya mikopo inaonekana kushuka kutoka asilimia 16.8 hadi asilimia 16.6 sawa na punguzo la asilimia 0.2. Uchambuzi wa kamati ulibaini kwamba, Benki Kuu ya Tanzania imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuongeza ukwasi kwenye mabenki ili yatoe mikopo kwa sekta binafsi. Hatua hizo ikiwa ni kupunguza riba inayotozwa kwenye mikopo ambayo mabenki yanakopa kutoka Benki Kuu kutoka asilimia 12 hadi asilimia saba, pamoja na kupunguza kiwango cha chini cha amana ambacho benki za biashara zinaweka Benki Kuu kutoka asilimia 10 hadi asilimia nane. Hatua hizo zimeweza kuongeza ukwasi kwa benki za biashara zaidi ya viwango vilivyowekwa na Benki Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa riba ya mikopo kwa sekta binafsi bado ni kubwa kinyume cha matarajio ya Benki Kuu. Riba inayotozwa kwenye mikopo ya sekta binafsi nchini imeshuka kwa asilimia 0.2 tu. Kamati inaona ukubwa wa riba ndio kikwazo kwa sekta binafsi kukopa katika mabenki ya biashara. Pamoja na uamuzi wa Serikali kutoa shilingi trilioni moja kwa benki za biashara ili zikopeshe sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya kilimo kwa riba nafuu benki zinatakiwa kushusha riba ya mikopo hiyo pamoja na kufanya marekebisho ya viwango vya riba vilivyokua vikitozwa kwenye mikopo hiyo iliyokuwa ikitolewa awali kabla ya kupokea fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kufanya yafuatayo; kwanza, kuhakikisha mikopo ya watumishi wa umma au watumishi wenyewe ajira za kudumu inatozwa riba ndani ya wigo wa tarakimu moja kwa sababu vihatarishi vya urejeshwaji wake si vikubwa. Pili, kushusha riba inayotolewa katika Hatifungani za Serikali kutoka asilimia 15 ya sasa hadi walau asilimia 10 ili kutozilazimisha benki za biashara kuwekeza kwenye Hatifungani za Serikali na badala yake zikopeshe sekta binafsi kwa riba nafuu kuliko ile inayotolewa na Serikali. Hatua hii itasaidia benki kufanya jukumu lake la msingi la kuikopesha sekta binafsi na kuchechemua uchumi. Aidha, suala hili liangaliwe sanjari na riba zinazotozwa na

kampuni za simu zinazotoa huduma za kifedha ambazo zimekuwa zikitoza riba kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na sekta ya kilimo; sekta hii inachangia shilingi triliuni 44.08 sawa na asilimia 26.9 ya Pato la Taifa la shilingi triliuni 163.88. Jambo la kusikitisha ni kwamba, sekta hii inaukuaji wa asilimia tatu hadi nne. Uchambuzi umebaini kwamba, sekta zinazokuwa kwa kasi kama vile ujenzi ni kutokana na uwekezaji wa Serikali katika sekta husika. Hivyo, ni wazi kwamba, Serikali ikifanya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo kwa kuhakikisha inaendeleza kilimo cha umwagiliaji, upatikanaji wa pembejeo za kilimo na viuatalifu kwa bei nafuu, upatikanaji wa mbegu bora za mazao na mifugo na kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo, hatua hizo zitaondoa umasikini kwa kiasi kikubwa kwa sababu, sekta hii ya kilimo inatao ajira kwa asilimia 66.3 ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeishauri Serikali kufanya yafuatayo ili iweze kuchochea ukuaji wa Sekta ya Kilimo na kuondoa umasikini: -

- i. Kuongeza Bajeti ya Wizara ya Kilimo kutoka shilingi bilioni 294.1 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hadi walau shilingi bilioni 450 kwa mwaka wa fedha 2022/2023,
- ii. Kufanya jitihada za makusudi za kuhakikisha kwamba, mbolea na pembejeo zinapatikana za kutosha, kwa muda sahihi na kwa bei nafuu,
- iii. Kuondoa kodi, ada na tozo ambazo zinasababisha kupanda kwa bei ya pembejeo, mbolea na viuatalifu,
- iv. Kuendeleza Kilimo cha umwagiliaji ili tuwe na kilimo endelevu na cha mwaka mzima,
- v. Kutenga na kulinda maeneo kwa ajili ya kilimo, ufugaji na vyanzo vya maji kwa ajili ya kilimo,

vi. Kuanzisha na kuendeleza mashamba makubwa ya mazao tunayonunua kutoka nje kama vile ngano, mafuta, sukari ya viwandani na shairi,

vii. Uwepo wa maafisa ugani wa kutosha na vitendea kazi kama pikipiki na magari.

viii. Kuwepo na ruzuku kwenye mbolea za kupandia, kukuzia mazao. Kutokana na mfumuko wa bei ya mbolea, Serikali chukue hatua kwa dharura kutoa ruzuku kwa mbolea angalau kwa bei nafuu ya mkulima isiyozidi msimu uliopita,

ix. Kuchangamkia fursa ya uwepo wa masoko makubwa ya mazao ya mbogamboga, matunda na maua (*horticulture*),

x. Serikali iboreshe kilimo cha umwagiliaji na mabwawa ya maji pamoja na uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora zinazo vumilia ukame,

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usimamizi wa sekta ndogo ya fedha, utakumbuka kwamba, mwaka 2018 Serikali ililetu Bungeni Sheria ya Sekta Ndogo ya Fedha (*The Microfinance Act Cap 407*) na ikapitishwa na Bunge na baadaye kanuni zake zikatungwa na Serikali Mwaka 2018. kifungu cha 14 cha Sheria hiyo kinaweka mazingira ya Benki Kuu kukasimu madaraka yake ya kusimamia sekta ndogo ya fedha kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, kifungu cha 54 cha sheria hiyo kinaweka masharti ya kumlinda mkopaji dhidi ya mikataba onevu na udhalimu kwa wakopaji.

Hata hivyo, pamoja na uwepo wa vifungu hivyo vyaheria, Benki Kuu haijaweza kusimamia utekelezaji wake kikamilifu na hivyo wafanyabiashara rasmi na wasio rasmi wameendelea kutoa huduma za kifedha zinazowanyonya wakulima, watumishi wa umma wakiwemo walimu na raia wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zilitakiwa kuwasaidia

wananchi zimekuwa na uelewa hafifu kuhusu matumizi ya sheria hiyo. Hivyo, Kamati inaisisitiza Serikali kuweka mikakati ya namna ya kuwabaini na kuwachukulia hatua stahiki wafanyabiashara rasmi na wasio rasmi wanaojihusisha na biashara ya sekte ndogo ya fedha kinyume na Sheria. Aidha, ni lazima kupunguza ukiritimba na mlolongo wa upatikanaji wa fedha ili kurahisha maisha ya wananchi wetu na kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa chakula tathmini ya Awali ya Hali ya Uzalishaji wa Mazao ya Chakula kwa Msimu wa 2020/2021 na Upatikanaji wa Chakula kwa mwaka 2021/2022 imeonesha kuwa hali ya uzalishaji wa chakula inatarajiwa kufikia kiasi cha tani 18.4 mwaka 2020/2021 kwa mlinganisho wa nafaka, ikilinganishwa na tani 18.1 msimu wa 2019/2020, sawa na ongezeko la asilimia 1.3. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2021/2022 yanakadiriwa kuwa kiasi cha tani 14.8 ambapo tani 9.4 ni ya mazao ya nafaka na tani 5.37 ni mazao yasiyo ya nafaka. Nchi inategemewa kuwa na ziada ya tani 3.6 za chakula ambapo tani 1.2 ni mazao ya nafaka na tani 2.4 ni mazao yasiyo nafaka. Hata hivyo, Mamlaka ya Hali ya Hewa imetabiri kuwepo kwa uhaba wa mvua kwa msimu wa mwaka 2021/2022 unaoweza kusababisha kupungua kwa uzalishaji wa chakula kwa mwaka 2022/2023 na hivyo kuleta mfumuko wa bei za vyakula nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali masuala yafuatayo: -

i. Kuendelea kuiwezesha *NFRA* kifedha ili iwe na uwezo wa kununua ziada ya chakula, ili kuleta uhimilivu wa bei inapotokea njaa na kuuza nje ya nchi tunapokuwa tumejitosheleza.

ii. Kuendelea kujenga vihenge na maghala ya kuhifadhia nafaka kwa *NFRA* hasa kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa chakula nchini kuliko ilivyo hivi sasa, ambapo *NFRA* wana uwezo wa kuhifadhi tani 501,000 tu. Kwa hali hii ina maana kwamba, hata Serikali ikiendelea kuipa

NFRA fedha za ununuzi wa nafaka, uwezo wake wa kuhifadhi ni asilimia 36 ya ziada ya nafaka inayozalishwa katika msimu wa mwaka 2020/21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2020/2021 na Robo ya Kwanza kwa Mwaka 2021/2022. Kamati ilipata fursa ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2020/2021 na Robo ya Kwanza ya Mwaka 2021/2022 ambapo masuala yafuatayo yamebainika:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya fedha za Maendeleo kwa mwaka 2020/2021 ulikuwa ni kwa asilimia 83.5. Aidha, kwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022 fedha za maendeleo zilizotolewa ni asilimia 17.3 ya bajeti kwa ajili ya kugharamila miradi ya maendeleo. Utoaji huu wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo hauridhishi ikizingatiwa kwamba utekelezaji wa miradi hiyo ndio utachochea ukuaji wa uchumi, maendeleo ya watu na viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2020/2021 na Mwaka 2021/2022 kama ilivyotajwa katika jedwali kwenye taarifa yetu kubwa, Kamati inapenda kusisitiza Serikali kutoa fedha za matumizi ya maendeleo kwa wakati kama zilivyoindhinishwa na Bunge ili mipango tunayojiwekea kila mwaka itekelezwe kama ilinavyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Sekta zilizopewa Kipaumbele kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/2021 na Robo ya kwanza ya mwaka 2021/2022. Sekta ya Miundombinu; Barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi kwenye utekelezaji wa miradi ya barabara 38 yenye jumla ya kilomita 8,575.29 zilizoko kwenye hatua mbalimbali na kubaini mambo yafuatayo; moja, Kuna barabara ambazo zina zaidi ya 10 ziko katika hatua

za upembuzi yakinifu na uchambuzi wa kina na hazijaanza kujengwa. Pili, kuna baadhi ya barabara zimejengwa kilomita chache na ujenzi haujaendelea kwa miaka mingi. Aidha, barabara mpya zinaendelea kuibuliwa ilihali barabara za zamani hazijakamilika ujenzi wake na kuna ongezeko la malipo ya riba kwa Serikali linalotokana na kutolipa wakandarasi kwa wakati kwa kigezo cha uhakiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi Kamati inashauri Serikali kufanya mambo yafuatayo;

Kwanza ni kukamilisha ujenzi wa barabara zilizokwisha ainishwa kwenye mpango, pili ni kuharakisha malipo ya wakandarasi pindi hati za malipo zinapowasilishwa. Aidha, endapo inabidi Serikali ifanye uhakiki usizidi siku 20 za kazi. Hatua hizi mbili zitasaidia kupunguza hasara inayotokana na riba na kuleta maendeleo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu reli. Hivi sasa nchi yetu ina njia kuu tatu za reli; Reli ya Kati yenye urefu wa kilometa 1,254 pamoja na matawi yake, Reli ya TAZARA inayounganisha nchi mbili Tanzania na Zambia yenye urefu wa kilometa 1,860 na reli ya kisasa inayojengwa kwa kiwango cha kimataifa (*SGR*). Pamoja na uwezo wa reli hizo mzigo unaoondoshwa kwa reli katika Bandari ya Dar es Salaam ni asilimia 2 tu ya shehena yote ya mizigo inayopita bandari ya Dar es Salaam, hivyo kamati inaona kwamba, bado kuna fursa kubwa katika kutumia miundombinu hii ya reli. Kamati inaushauri ufuatao kwa Serikali: -

i. Kukamilisha mapema iwezekanavyo upatikanaji wa fedha na mkandarasi wa ujenzi wa vipande vya Makutupora – Tabora kilometra 368 na Tabora – Isaka kilometra 165 ili Reli ya Kati kwa kiwango cha *SGR* ianzе kufanya kazi. Ikiachwa hivihivi manufaa ya reli hiyo hayataonekana.

ii. Kukamilisha mapema iwezekanavyo upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa reli za Tabora – Kigoma kilometra 411, Keza - Ruvubu kilometra 36, Uvinza – Musongati kilometra 210 na Kaliua – Mpanda – Karema

kilometra 321 kwa kiwango cha *Standard Gauge* kwa sababu, huku ndiko hasa kuna shehena kubwa ya mzigo ambayo inaweza kuleta manufaa makubwa kwa taifa letu.

iii. Kuharakisha mapitio ya Sheria ya *TAZARA* ili kutoa fursa kwa Tanzania kuwekeza kwenye reli hiyo ili iwe na manufaa kwa upande wa Tanzania. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuingia ubia na kampuni kubwa ili kupata vichwa na mabehewa na Serikali iwe inakodisha njia ya reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usafiri wa Anga. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imeshatumia Shilingi billioni 557.8 katika kuimarisha usafiri wa anga na Shirika la ndege la *ATCL*. Kamati ilipata fursa ya Kukutana na Mkurugenzi Mkuu wa *ATCL* na kubaini changamoto ambazo zinakwamisha shirika hilo kusimama imara na kupunguza hasara. Kwanza kutokana na athari za ugonjwa wa UVIKO-19, shirika liliathirika lakini hakukuwa na mpango wowote wa Serikali kulinusuru shirika hilo kama ambavyo mashirika mengine ya ndege duniani yamefanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Ndege za Serikali aliendelea kutoza gharama ya pango kwa ndege zote hata zile ambazo zimepaki kwa kiasi cha dola milioni 1.5 kwa mwezi. Aidha, Wakala wa Ndege inaitaka *ATCL* kuweka amana ya matengenezo ya ndege ya jumla ya Shilingi billioni 1.2 kila mwezi ilhali matengenezo ya ndege yanafanywa na *ATCL* wenyewe na si wakala wa ndege za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kufanya yafuatayo ili kuimarisha usafiri wa anga na shirika la ndege la *ATCL*: -

i. Serikali kulipa madeni yaliyokuwa ya Shirika la Ndege la *ATCL* kabla ya kufufuliwa ili kusafisha vitabu vyta ya Shirika.

ii. Serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama za kukodi ndege ili shirika liweze kukua na kuijendesha kwa faida. Hatua hii iende sambamba na

uwezekano wa kusamehe ada ya pango la ndege walau kwa miaka miwili katika kipindi ambapo kulikuwa na athari za *UVICO-19* kwa maana ya mwaka 2019/2020 na 2020/2021.

iii. Serikali kukamilisha haraka ujenzi wa viwanja vya ndege vya mikoa ili kuongeza mtandao na idadi ya miruko ya ndege za *ATCL* ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na bandari. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Bandari ambapo ni dira pana ya maendeleo ya bandari zote nchini. Mpango huu umezaaa miradi mingi kama vile mradi wa *DMGP* ambao una lengo la kuongeza uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam kuhudumia shehena ya mizigo kwa kufanya uboreshaji wa miundombinu ya bandari ya Dar es Salaam ambapo itaweba kusafirisha mizigo kuanzia tani milioni 16 hadi tani milioni 25 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaushauri ufuatao kwa Serikali kuhusu Mamlaka ya Bandari: -

i. Serikali kuhamisha makusanyo ya *warfage* kutoka mfuko mkuu wa Serikali na kuyapeleka kwenye akaunti ya *TPA* iliyoko Benki kuu ili kuhakikisha kwamba, *TPA* inakuwa na ukwasi wa kutosha muda wote tofauti na ilivyo hivi sasa.

ii. Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Bandari ukatekelezwe katika Bandari zote nchini na sio Dar es Salaam peke yake ili kutanua uwezo wa *TPA* kuhudumia shehena kubwa zaidi.

iii. Kamati imeielekeza Serikali kuititia upya Masharti ya Mkataba wa *TICTS* pamoja na *TPA* ili kuangalia kama bado tunahitaji kampuni hiyo hasa kwa kuzingatia kwamba, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika Bandari ya Dar es salaam.

iv. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutoa eneo lilitokuwa la mradi wa Kurasini *Logistic Centre* kwa mamlaka ya *TPA* ili litumike kama *Container Deport* ya *TPA*

kuliko ilivyo sasa hivi ambapo sasa imebaki tu kuwa maegesho ya Malori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Mazingira. Moja ya jambo ambalo halipewi kipaumbele ambalo lina gharama kubwa ni utunzaji wa mazingira. Sote tunakubaliana kwamba, tukiacha mazingira yakaharibika kwa namna yoyote ile madhara yake ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2022/2023 ujielekeze kwanza katika kufanya mabadiliko kwenye sheria ya mazingira sura 272 ili kutanzua vikwazo vyote vya kisheria vinavyosababisha mfuko wa mazingira usipate fedha kutoka "*Global Green Fund*". Pili ni kuanzisha programu maalumu za upandaji miti katika mashule, vyuo, Vijiji, Mitaa kata na Tarafa ili kuanzisha misitu mipya nchini. Tatu kulinda vyanzo vyote vya maji na mito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Ardhi, moja ya changamoto kubwa nchini ni mipango ya matumizi bora ya ardhi na upatikanaji wa hati miliki. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba hati miliki za maeneo yaliyopimwa zitolewe ndani ya siku saba pindi ambapo mhusika anakuwa amekamilisha taratibu zote za umiliki. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhuisha na kutengeneza mipango mipya ya matumizi ya ardhi kwa kuangalia shughuli za kiuchumi, kijamii na kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa Wa Mwaka 2022/2023. Kamati ya Bajeti imepitia na kuchambua ugharamiaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2022/2023, ambapo Jumla ya shilingi trillioni 14.7 zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kulipa madeni ya wakandarasi wa ndani. Kamati ilibaini kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kufikia malengo ya utekelezaji wa Bajeti ya maendeleo kwa asilimia 85 hadi 90. Vilevile kamati ilibaini ongezeko la Bajeti ya maendeleo imeongezeka toka shilingi trillioni 13.7 hadi shilingi trillioni 14.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatifungani za halmashauri, Kamati ilibaini kwamba Serikali imepanga kutumia vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia mpango kama vile hatifungani za halmashauri, kamati ilibaini kwamba vyanzo hivyo vilikuwa kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa lakini hawakuweza kuvitumia. Mfano hatifungani za halmashauri Serikali ilikuwa imepiga hatua hadi kuwapeleka baadhi ya Wakurugenzi wa Majji ya Tanga, Dar es Salaam na Arusha nchini Afrika Kusini ili wakajifunze namna ya kutumia chanzo hicho hata hivyo hakuna kilichofanyika. Kamati inaitaka Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 kutumia Hatifungani ya Miundombinu "*Infrastructure Bond*" kujenga Reli na Halmshauri zianze kutumia *Municipal Bond* kujenga miradi ya kibiashara kuliko kutegemea fedha kutoka mfuko mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tathmini na Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mpango kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Kamati inaitaka Serikali katika mwaka ujao wa fedha 2022/2023 kuleta Bungeni Sera na Muswada wa Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji (*M&E*). Jambo Hili limekuwa likisemwa miaka yote lakini Serikali haikuchukua hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati Kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Mwaka (2022/2023) Pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23 katika kuboresha mapendekezo ya Mpango wa Mwaka 2022/2023 na ili kufanikisha azma ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati cha juu ifikapo 2025, na sio wa kipato cha kati cha chini, Kamati imependa kuwasilisha uchambuzi na mapendekezo yake katika maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi wa shabaha, vihatarishi na maeneo ya Vipaumbele katika mpango wa mwaka 2022/2023 na kubaini kwamba kuna uwezekano mkubwa wa Serikali kufikia shabaha zake kama zinavyoonekana kwenye Mpango. Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya vipaumbele vichache kwa kila sekta

ambavyo vinaweza kuleta matokeo ya haraka ama kumaliza changamoto zinazokabili Taifa na kuvitekeleza kwa mwaka mmoja ili kuchochaea uchumi na kuleta maendeleo ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhakiki na ulipaji wa Madeni ya Wakandarasi na Wazabuni, kuanzia 2015/2016 hadi 2020/2021, jumla ya madeni ya shilingi trilioni 3.8 yaliwasilishwa kwa ajili ya uhakiki na yalihakikiwa. Kati ya kiasi hicho, madeni ya shilingi trilioni 2.6 yalikidhi vigezo na shilingi trilioni 1.1 hayakukidhi vigezo. Aidha, katika kipindi hicho, madeni yenye jumla ya shilingi trilioni 2.1 yalilipwa na hivyo kuwepo na baka ya shilingi bilioni 506.8 ambayo hayajalipwa hadi kufikia Juni 30, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya uchambuzi wa madeni ya wakandarasi na wazabuni na kubaini kwamba wapo wadai ambao hawana taarifa kuwa madeni yao yamehakikiwa na hayajakubalika kulipwa hakuna vigezo vilivyobainishwa nani aanze kulipwa wa kwanza, nani afuate na nani awe wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kwanza, kuhakikisha msamiati wa uhakiki unaondoka kwenye taarifa zinazowasilishwa Bungeni kwa sababu inaonekana kama kichaka cha kukwepa kulipa madeni ya wazabuni. Aidha, uhakiki ufanyike kabla ya mpewa huduma hajapokea *certificate* na kuipeleka hazina kwa ajili ya malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ununuzi wa Dawa na Upatikanaji wa Dawa nchini Kamati imefanya utafiti na kubaini kwamba kumekuwa na changamoto za upatikanaji wa Dawa katika Hospitali za Umma na vituo vya kutolea huduma za afya katika maeneo yafuatayo: -

(i) Uagizwaji wa dawa na vifaa tiba unatumia kati ya miezi miwili hadi mitatu hivyo kama fedha za ununuzi wa Dawa zinatolewa mwezi wa 8 dawa zitafika kati ya mwezi wa 10 hadi wa 11;

(ii) *MSD* kupewa fedha za ununuzi wa madawa kwa mfumo wa mahitaji na sio kwa *MSD* kuwa na dawa kusubiria mahitaji;

(iii) Katika mwaka 2019/2020 *MSD* hawakupewa fedha kabisa za ununuzi wa dawa kwa sababu kulikuwa na viashiria vya wizi;

(iv) *MSD* haina mtaji wa kutosha na mtaji uliopo unapungua kila kukicha kwa sababu inautumia katika kuondosha mizigo ya dawa zilizoko bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kuachana mara moja na utaratibu wa kuwahukumu wananchi kwa matendo ya watendaji wake kwa sababu tabia hii imeonekana katika maeneo mengi. Kuna halmashauri hazipatifu fedha za maendeleo kwa sababu kuna ubadhilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu *MSD* Kamati ina ushauri ufuatao: -

(i) Serikali itoe kiasi cha Shilingi bilioni 150 kama mtaji kwa kiasi cha shilingi bilioni 363.9 za mtaji wa ununuzi wa madawa kwa kufanya hivyo *MSD* itaweza kuagiza dawa na pindi mahitaji yanapojoitokeza dawa zisubiriwe. Mtaji huo utoke kwenye mkopo ambao Serikali huchukua Benki Kuu kila mwaka kwa mujibu wa kifungu cha 34 cha Sheria ya Benki kuu Sura namba 197;

(ii) Aidha Serikali inashauriwa kuangalia uwezekano wa kutoa fedha za miezi miwili kwa *MSD* au mitatu mwanzo wa mwaka ili *MSD* iwe na mtaji wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe ila naomba taarifa yetu iingie kwenye kumbukumbu rasmi za *Hansard* hapa kuna madini ya kutosha kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb),

kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu na kwa maelekezo yako ambayo umekuwa ukitoa mara kwa mara kwa Kamati hii. Maelekezo ambayo umekuwa ukitupatia mara kwa mara yamekuwa kwa kiasi kikubwa yakiboresha utendaji kazi wa Kamati hii na ushauri unaoutoa kwa Serikali. Kwa hilo tunapenda kukushukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru Mhe. Dkt. Tulia Ackson, Mb, Naibu Spika kwa miongozo ambayo kwa pamoja mmekuwa mkitupatia. Vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Mwihambi na timu yake kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, kipekee napenda kumshukuru, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb, Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Mb, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru Katibu Mkuu Fedha na Manaibu Katibu Wakuu wa Wizara na wataalamu wote ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mapendekezo ya Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wa Kamati hii ya Bajeti kwa umakini mkubwa katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali. Naomba majina yao yote yaingie katika kumbukumbu rasmi za Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa naomba kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Mathew Kileo, Makatibu wa Kamati Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala, Maombi Kakoozi na Wilfred Akasi pamoja na Msaidizi wa Kamati Grace Mwenye kwa miongozo yao na ushauri wa kiutalaam hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU
MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA
WA MWAKA 2022/23 PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA
MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA
BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/23 – KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 113 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 unaopendekezwa ni Mpango wa Pili katika mfululizo wa utekelezaji wa Mpango wa Tatoo wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) uliobeba Dhima ya “*Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu*”. Hivyo, ni wazi kwamba Mapendekezo ya Mpango huu yanalenga kuweka mazingira mahsus ya kufikia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, hasa ukizingatia imebakia miaka mitatu (3) ya kukamilisha na kufikia malengo yaliyobainishwa katika Dira hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23 yaliyowasilishwa na Serikali na kutoa ushauri wake kwenye maeneo yafuatayo; Hali ya Uchumi, Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21 na Robo ya Kwanza ya Mwaka 2021/22, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/23 pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23.

Mheshimiwa Spika, Mapendekazo yaliyowasilishwa mbele yako leo yanaonyesha nia thabiti ya **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuiletea maendeleo nchi yetu na kujenga uchumi shindani. Mapendekazo haya ya mpango kweli yanadhihirisha maneno ya wananchi kwamba Mama anaupiga mwingu.

2.0. MAPITIO YA HALI YA UCHUMI JUMLA KATIKA MWAKA 2021

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa mwenendo wa viashiria vyote vya hali ya uchumi katika mwaka 2021 ili kuangalia mafanikio na changamoto za kiuchumi zilizojitekeza katika utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2020/21. Baadhi ya viashiria vilivyo fanyiwa mapitio ni Ukuaji wa Uchumi, Mfumuko wa Bei, Deni la Serikali, Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi, Mwenendo wa thamani ya Shilingi, Usimamizi wa Sekta Ndogo ya Fedha pamoja na Upatikanaji wa Chakula.

Jedwali Na. 1: Viashiria vya Hali ya Uchumi katika Mwaka 2019/20 – 2020/21 (bilioni)

Nr.	Kiashiria	Malengo ya Mpango wa Maka Mtano (2021/2022 – 2025/2026)	Hali ya Utekelezaji	
			2019/20	2020/21
1.	Ukuaji wa Uchumi	100	7.0	4.8
2.	Mfumukwa bei	5	3.1	4.0
3.	Deni la Serikali	-	56,449.8	64,497.83
4.	Mwenendo wa Thamani ya Shilingi dhidi ya USD	2,185.62	2,301.30	2,309.58
5.	Vivango vya riba kwa sekta binafsi	-	16.8	16.6
6.	Hali ya Umakini	22%	26.4%	26.4%
7.	Ukuaji wa Sekta ya Kilimo	5	4.4%	4.9%

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia uchambuzi wa Kamati kuhusu mwenendo wa viashiria vya hali ya uchumi, Kamati inapenda kutoa ushauri ufuatao: -

2.1. Ukuaji wa Uchumi wa Taifa

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2021 (Januari hadi Juni 2021), Uchumi wa Taifa ulikuwa kwa asilimia 4.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2020. Sekta zilizokua kwa kasi kubwa ya ukuaji ni pamoja na: habari na mawasiliano

(asilimia 10.7); umeme (asilimia 9.6); na maji safi na taka (asilimia 8.7). Aidha, malazi na huduma za chakula ziliikuwa kwa kasi ndogo zaidi kuliko sekta nyingine kwa asilimia 1.0. Kushuka kwa ukuaji wa uchumi kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na kuchelewa kwa utekelezaji wa baadhi ya miradi pamoja na athari za UVIKO-19 hasa katika shughuli za kiuchumi za hoteli, utalii, huduma za chakula, afya na biashara.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza vyema mapambano dhidi ya athari za UVIKO-19 kwenye uchumi wa Taifa letu pamoja na maendeleo ya watu. Juhudi alizoziweka Mheshimiwa Rais katika upatikanaji wa **Fedha za Mkopo wa Masharti nafuu Shilingi Trilioni 1.3 kutoka IMF** na uwekaji wa vipaumbele vyta matumizi ya fedha hizo kwa kulishirikisha Bunge lako Mheshimiwa Spika kuititia Kamati ya Bajeti, ni za kupongezwa na Kamati inaamini juhudhi hizo zitasaidia kwa kiasi kikubwa kupambana na UVIKO-19 pamoja na kuboresha ustawi wa Taifa letu. Aidha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inatumia vizuri fedha hizo katika kutekeleza vipaumbele viliviyowekwa. Pia, iendelee kuziwezesha kifedha na kuweka mipango mizuri ya kukuza sekta ya kilimo, kufufa sekta ya utalii na sekta zingine kama vile sekta ya Afya, biashara na uwekezaji ambazo zimeathirika na UVIKO-19.

2.2. Mfumuko wa Bei

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango yanaonyesha kuwa Mfumuko wa Bei umeendelea kuimarika na kuwa ndani ya lengo la **asilimia 3** hadi **5**. Aidha, mfumuko wa bei ulifika wastani wa **asilimia 4.0** mwezi Septemba 2021 ikillinganishwa na **asilimia 3.1** katika kipindi kama hicho mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2020/21 sababu zilizochangia kupungua kwa mfumuko wa bei nchini ni upatikanaji wa chakula cha kutosha, kushuka kwa bei ya mafuta kwenye soko la dunia, uwepo wa utulivu wa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani na sarafu nyingine duniani, pamoja na sera madhubuti ya fedha na

sera ya bajeti. Hata hivyo, **Shilingi Triliioni 1.3** kutoka IMF zilizoingia katika uchumi kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO-19, kati ya fedha hizo zaidi ya **Shilingi Bilioni 500** zimepelekwa kwenye miradi ya ujenzi, ambapo zimesababisha mfumuko wa bei kwa vifaa vya ujenzi. Aidha, kutokana na uwepo wa taarifa ya kuwa na hali ya ukame katika msimu wa 2021/22, pamoja na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia, inaashiria kwamba katika muda wa kati kuna hatari kubwa ya bei za bidhaa kupanda maradufu.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha Viwanda vya ndani vya uzalishaji wa bidhaa za ujenzi, kuzalisha katika uwezo wao wa juu "*Full capacity*"; Kuendelea kuijengea uwezo NFRA kifedha, kimitaji na kimiundombinu endapo kutakua na ukame NFRA iwe na hifadhi ya chakula cha kutosha; aidha, Kamati inaishauri Serikali kusimamia kwa makini sekta ya fedha katika kipindi hiki ambapo kunatarajija ongezeko katika mfumukowa bei, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kudhibiti bei ya mafuta ya petroli katika soko la ndani; na kuendelea kupambana na wahujumu uchumi wanaoficha bidhaa ili bei ipande.

2.3. Deni la Serikali

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango yanaonyesha kuwa hadi Juni 2021, Deni la Serikali liliflikia **Shilingi Triliioni 64.498** ikilinganishwa na **Shilingi Triliioni 56.45** Juni 2020, sawa na **ongezeko la asilimia 14.3**. Kati ya Deni hilo, kiasi cha Shilingi Triliioni **45.564** ni deni la Nje na **Shilingi Triliioni 18.934** ni deni la ndani. Sababu ya ongezeko hilo linatokana na kupokelewa kwa fedha za mikopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Kamati imebaini kwamba Serikali inatarajia katika muda wa kati kuongeza kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara kutoka **asilimia 8.9** hadi **asilimia 44.5**. Utuftuti mkubwa wa mikopo ya kibiashara na mikopo ya masharti nafuu ni muda wa kuanza kulipa "*grace period*" na kiwango cha riba cha mikopo ya kibiashara ni kikubwa. Mikopo ya kibiashara ina muda mfupi wa mwaka **1** hadi **2** na deni huiva ndani ya miaka **3**. Wakati mikopo ya masharti nafuu ni miaka **7** hadi **8** na huiva ndani ya miaka **10**.

Mheshimiwa Spika, baada ya tathmini hiyo, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo; Kwanza, fedha za mikopo yote ya kibashara zielekezwe kwenye miradi yenye sura ya kibashara na inayoweza kuzalisha mapato kwa muda mfupi. Pili, Miradi yote inayotumia muda mrefu kukamilika na kuleta faida itumie mikopo yenye masharti nafuu. Tatu, kukamilisha uhakiki na kulipa Madeni ya Wazabuni, Wakandarasi na Watoa huduma ili kudhibiti Deni la Serikali liendelee kuwa himilivu.

2.4. Mwenendo wa Thamani ya Shilingi

Mheshimiwa Spika, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani na sarafu nyingine za Washirika wakuu wa biashara ulimwenguni katika mwaka 2020/21 imeendelea kuimarika. Katika kipindi hicho, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa **Shilingi 2,309.58** ikilinganishwa na **Shilingi 2,301.30** katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Hali hii imechangiwa na utulivu wa bei nchini, utekelezaji wa sera thabiti za fedha na bajeti, usimamizi imara katika kuhakikisha uwazi na utaratibu mzuri katika soko la kubadilisha fedha za kigeni na utulivu wa bei ya mafuta katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuendelea kuimarika kwa thamani ya shilingi ya Tanzania, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inapunguza uagizaji wa huduma na bidhaa kutoka nje ya nchi ambazo zinaweza kuzalishwa nchini na kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma ambazo zitaongeza mauzo nje ya nchi kama vile ngano, shayiri, mafuta ya kula, sukari ya viwandani, chuma, huduma za kitaalmu na usafiri wa anga.

2.5. Mwenendo wa Mikopo ya Sekta Binafsi

Mheshimiwa Spika, Mikopo kwa Sekta Binafsi ilikua kwa wastani wa **asilimia 4.3** katika mwaka 2020/21, ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 8.1** katika mwaka wa fedha 2019/20. Aidha, riba ya mikopo inaonekana kushuka kutoka **asilimia 16.8** hadi **asilimia 16.6** sawa na punguzo la **asilimia 0.2**. Uchambuzi wa kamati ulibaini kwamba Benki Kuu ya Tanzania imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuongeza ukwasi

kwenye mabenki ili yatoe mikopo kwa Sekta Binafsi. Hatua hizo ikiwa ni pamoja na Kupunguza riba inayotozwa kwenye mikopo ambayo mabenki yanakopa kutoka Benki Kuu kutoka asilimia **12** hadi asilimia **7**, pamoja na kupunguza kiwango cha chini cha amana (SMR) ambacho Benki za biashara zinaweka Benki Kuu kutoka **asilimia 10** hadi **asilimia 8**.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uamuzi wa Serikali kutoa shilingi **Triliioni 1** kwa Mabenki ya biashara ili yakopeshe sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya kilimo kwa riba nafuu mabenki yanatakiwa kushusha riba ya mikopo hiyo pamoja na kufanya marekebisho ya viwango vya riba vilivyokua vikitozwa kwenye mikopo iliyokua ikitolewa awali (restructuring of existing portfolio) kabla ya kupokea fedha hizo. Hatua hizo zimeweza kuongeza ukwasi kwa benki za biashara zaidi ya viwango vilivyowekwa na Benki Kuu. Ingawa riba ya mikopo kwa sekta binafsi bado ni kubwa kinyume cha matarajio ya Benki Kuu. Riba inayotozwa kwenye mikopo ya sekta binafsi nchini imeshuka kwa **asilimia 0.2** tu. Kamati inaona ukubwa wa riba ndio kikwazo kwa sekta binafsi kukopa katika mabenki ya biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kufanya yafuatayo; Kwanza, kuhakikisha mikopo ya watumishi wa umma au watumishi wenyewe ajira za kudumu inatozwa riba ndani ya wigo wa tarakimu moja kwa sababu vihatarishi vya urejeshwaji wake sio vikubwa. Pili, kushusha riba inayotolewa katika Hatifungani za Serikali kutoka **asilimia 15** ya sasa hadi walau **asilimia 10** ili kutozilazimisha benki za biashara kuwekeza kwenye Hatifungani za Serikali na badala yake zikopeshe sekta binafsi kwa riba nafuu kuliko ile inayotolewa na Serikali. Hatua hii itasaidia mabenki kufanya jukumu lake la msingi la kuikopesha sekta binafsi na kuchechemua uchumi. Aidha, suala hili liangaliwe sanjari na riba zinazotozwa na Makampuni ya simu yanayotoa huduma za kifedha ambayo nayo yamekuwa yakitoza riba kubwa.

2.6. Sekta ya Kilimo

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo inachangia **Shilingi Triliioni 44.08** sawa na **asilimia 26.9** ya Pato la Taifa la **Shilingi Triliioni**

163.88. Jambo la kusikitisha ni kwamba sekta hii inaukuaji wa **asilimia 3** hadi **4**. Uchambuzi umebaini kwamba sekta zinazokuwa kwa kasi kama vile ujenzi (**asilimia 14.4**) ni kutokana na uwekezaji wa Serikali katika sekta husika. Hivyo, ni wazi kwamba Serikali ikifanya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo kwa kuhakikisha inaendeleza kilimo cha umwagiliaji, upatikanaji wa pembejeo za kilimo na viuatilifu kwa bei nafuu, upatikanaji wa mbegu bora za mazao na mifugo na kuimarisha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya uwekezaji kwenye sekta ya kilimo. Hatua hizo zitaondoa umasikini kwa kiasi kikubwa kwa sababu sekta ya kilimo inatoa ajira kwa **asilimia 66.3** ya watanzania.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeishauri Serikali kufanya yafuatayo ili iweze kuchochea ukuaji wa Sekta ya Kilimo na kuondoa umasikini: -

- i. Kuongeza Bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo kutoka **shilingi bilioni 294.1** kwa mwaka wa fedha 2021/22 hadi walau **shilingi bilioni 450** kwa mwaka wa fedha 2022/23;
- ii. Kufanya jitihada za makusudi za kuhakikisha kwamba mbolea na pembejeo zinapatikana za kutosha, kwa muda sahihi na kwa bei nafuu;
- iii. Kuondoa kodi, ada na tozo ambazo zinasababisha kupanda kwa bei ya pembejeo, mbolea na viuatalifu;
- iv. Kuendeleza Kilimo cha umwagiliaji ili tuwe na kilimo endelevu na cha mwaka mzima;
- v. Kutenga na kulinda maeneo kwa ajili ya Kilimo, ufugaji na vyanzo vya maji kwa ajili ya kilimo;
- vi. Kuanzisha na kuendeleza mashamba makubwa ya mazao tunayonunua kutoka nje kama vile ngano, mafuta, sukari ya viwandani na shairi.
- vii. Uwepo wa maafisa ugani wa kutosha na vitendea kazi kama vile pikipiki na magari; na

viii. Kuwepo na ruzuku kwenye mbolea za kupandia, kukuzia mazao. Kutokana na mfumuko wa bei ya mbolea, Serikali ichukue hatua kwa dharura kutoa ruzuku kwa mbolea angalau kwa bei nafuu ya mkulima isiyozidi msimu uliopita.

ix. Kuchangamkia fursa ya uwepo wa masoko makubwa ya mazao ya mbogamboga, matunda na maua (horticulture).

x. Serikali iboreshe kilimo cha umwagiliaji na mabwawa ya maji pamoja na uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora zinazo vumilia ukame.

2.7. Usimamizi wa Sekta Ndogo ya Fedha

Mheshimiwa Spika, Utakumbuka kwamba mwaka 2018 Serikali ililetu Bungeni Sheria ya Sekta Ndogo ya Fedha *"The Microfinance Act Cap 407"* na ikapitishwa na Bunge na baadae kanuni zake zikatungwa na Serikali Mwaka 2018. kifungu cha 14 cha Sheria hiyo kinaweka mazingira ya Benki Kuu kucasimu (delegate) madaraka yake ya kusimamia Sekta ndogo ya fedha kwa Mamlaka za Serikali za Mtaa. Aidha, kifungu cha 54 cha sheria hiyo kinaweka masharti ya kumlinda mkopaji dhidi ya mikataba onevu na udhalimu kwa wakopaji. Hata hivyo, pamoja na uwepo wa vifungu hivyo vyta sheria, Benki Kuu hajjaweza kusimamia utekelezaji wake kikamilifu na hivyo wafanyabiashara rasmi na wasio rasmi wameendelea kutoa huduma za kifedha zinazowanyonya wakulima, watumishi wa umma wakiwemo walimu na raia wengine.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zilitakiwa kuwasaidia wananchi zimekuwa na uelewa hafifu kuhusu matumizi ya sheria hiyo. Hivyo, Kamati inaisisitiza Serikali kuweka mikakati ya namna ya kuwabaini na kuwachukulia hatua stahiki wafanyabiashara rasmi na wasio rasmi wanaojihusisha na biashara ya sekta ndogo ya fedha kinyume na Sheria. Aidha, ni lazima kupunguza ukiritimba na mlolongo wa upatikanaji wa fedha ili kurahisha maisha ya wananchi wetu katika kuendesha maisha yao.

2.8. Tathmini ya Upatikanaji wa Chakula

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya Awali ya hali ya uzalishaji wa Mazao ya Chakula Msimu wa 2020/21 na Upatikanaji wa Chakula kwa Mwaka 2021/22 imeonesha kuwa, hali ya uzalishaji wa chakula inatarajiwaa kufikia kiasi cha **tani 18,425,250** mwaka 2020/21 kwa mlinganisho wa nafaka, ikilinganishwa na **tani 18,196,733** msimu wa 2019/20 sawa na ongezeko la **asilimia 1.3**. Mahitaji ya chakula kwa mwaka 2021/22 yanakadiriwa kuwa kiasi cha **tani 14,796,751** ambapo **tani 9,417,888** ni mazao ya nafaka na **tani 5,378,864** ni mazao yasiyo nafaka. Nchi inategemewa kuwa na ziada ya **tani 3,628,499** za chakula ambapo **tani 1,222,103** ni mazao ya nafaka na **tani 2,406,396** ni mazao yasiyo nafaka. Hata hivyo, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetabiri kuwepo kwa uhaba wa mvua kwa msimu wa mwaka 2021/22 unaoweza kusababisha kupungua kwa uzalishaji wa chakula kwa mwaka 2022/23 na hivyo kusababisha mfumuko wa bei za vyakula nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali masuala yafuatayo: -

- i. Kuendelea kuiwezesha kifedha NFRA iwe na uwezo wa kununua ziada ya chakula ili kuleta uhimilivu wa bei inapotokea njaa na kuuza nje ya nchi tunapokuwa tumejitosheleza;
- ii. Kuendelea kujenga vihenge na maghala ya kuhifadhia nafaka kwa NFRA hasa kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa chakula nchini kuliko ilivyo hivi sasa, ambapo NFRA wana uwezo wa kuhifadhi tani 501,000 tu. Kwa hali hii ina maana kwamba hata Serikali ikiendelea kuipa NFRA fedha za ununuzi wa nafaka, uwezo wake wa kuhifadhi ni **asilimia 36** ya ziada ya nafaka iliyozalishwa katika msimu wa mwaka 2020/21; na
- iii. Kuiwezesha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kimtaji ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kununua mazao na kuyauza kibiashara pale ambapo uwezo wa NFRA kuhifadhi mazao unapokuwa mdogo.

3.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2020/21 NA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2021/22

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21 na Robo ya Kwanza ya Mwaka 2021/22. Tathmini inaonyesha kuwa Serikali imeweza kusimamia na kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kiwango kinachoridhisha hasa ile miradi mikubwa ya kielelezo ya kuwezesha uchumi kukua kwa kasi (flagship project), miradi ya kuendeleza viwanda na sekta muhimu kiuchumi ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi pamoja na baadhi ya maeneo ya kuboresha maendeleo ya watu.

3.1. Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo za Mwaka 2020/21 na Robo ya kwanza ya Mwaka 2021/22

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya fedha za Maendeleo kwa mwaka 2020/21 ulikuwa ni kwa **asilimia 83.5**. Aidha, kwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22 fedha za maendeleo zilizotolewa ni **asilimia 17.3** tu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Utoaji huu wa fedha za kugharamia miradi ya maendeleo hauridhishi ikizingatiwa kwamba utekelezaji wa miradi hii ndio utachochea ukuaji wa uchumi, maendeleo ya watu na viwanda.

Jedwali Na. 2: Utekelezaji wa Bajeti ya Mipango ya Maendeleo ya Taifa Mwaka 2020/21 na Robo ya Kwanza 2021/22 (bilioni)

Na.	Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21	Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22
Bajeti ya Mpango wa Maendeleo iliyotengwa	12,779.3	13,678.9
Asilimia (%) ya Bajeti ya Serikali	37	37.3
Fedha za Matumizi zilizotolewa	10,667.1	2,367.2 (Robo ya Kwanza)
Asilimia (%) ya utekelezaji wa Bajeti ya Mpango	83.5	17.3

Chanzo: Taarifa ya Serikali ya Mapendekezo ya Mpango 2022/23

Mheshimiwa Spika, Baada ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2020/21 na Mwaka 2021/22 kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 2 hapo juu, Kamati inapenda kusitiza Serikali kutoa fedha za matumizi ya maendeleo kwa wakati kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili Mipango tunayojojiwekea kila mwaka itekelezwe kama ilivyokusudiwa.

3.2. Utekelezaji wa Sekta zilizopewa Kipaumbele kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/21 na Robo ya kwanza ya mwaka 2021/22.

3.2.1 Sekta ya Miundombinu

a) Barabara

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi kwenye utekelezaji wa miradi ya barabara 38 yenye jumla ya **Kilomita 8,575.29** zillizoko kwenye hatua mbalimbali na kubaini mambo yafuatayo: moja, Kuna barabara ambazo zina miaka zaidi ya 10 ziko katika hatua ya upembuzi yakinifu, na uchambuzi wa kina na hazijaanza kujengwa. Pili, Kuna baadhi ya barabara zimejengwa kilomita chache na ujenzi haujaendelea kwa miaka mingi. Aidha, Barabara mpya zinaendelea kuibuliwa ilihali barabara za zamani hazijakamilika ujenzi wake na kuna ongezeko la malipo ya riba kwa Serikali linalotokana na kutolipa wakandarasi kwa wakati kwa kigezo cha uhakiki.

Mheshimiwa Spika, Baada ya uchambuzi Kamati inashauri Serikali kufanya masuala yafuatayo: Kwanza ni kukamilisha ujenzi wa barabara zilizokwisha ainishwa kwenye mpango. Pili ni kuharakisha malipo ya wakandarasi pindi hati za malipo (certificates) zinapowasilishwa. Aidha, endapo itabidi Serikali ifanye uhakiki usizidi siku 20 za kazi. Hatua hizi mbili zitasaidia kupunguza hasara inayotokana na riba na kuleta maendeleo yaliyokusudiwa.

b) Reli

Mheshimiwa Spika, Hivi sasa nchi yetu ina njia kuu tatu za Reli, Reli ya Kati yenye urefu wa **km 1,254** pamoja na matawi yake, Reli ya TAZARA inayounganisha nchi mbili Tanzania na

Zambia wenyе urefu wa **km 1,860**. Na reli ya kisasa inayojengwa kwa kiwango cha kimataifa (SGR). Pamoja na uwepo wa reli hizo mzigo unaoondoshwa kwa reli katika Bandari ya Dar es Salaam ni asilimia **2** tu ya shehena yote ya mizigo inayopitia bandari ya Dar es Salaam, hivyo kamati inaona kwamba bado kuna fursa kubwa katika kutumia miundombinu hii ya reli. Kamati inaushauri ufuatao kwa Serikali: -

- i. Kukamilisha mapema iwezekanavyo upatikanaji wa fedha na Mkandarasi wa ujenzi wa vipande vyta Makutupora (Singida) – Tabora (**km 368**) na Tabora – Isaka (**km 165**) ili Reli ya kati kwa kiwango cha SGR ianze kufanya kazi ikiachwa ilivyo hivi sasa manufaa ya reli hiyo hayataonekana;
- ii. Kukamilisha mapema iwezekanavyo upembuzi yakinifu na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa njia za reli ya Tabora – Kigoma (**km 411**), Keza - Ruvubu (**km 36**), Uvinza – Musongati (**km 210**) na Kaliua – Mpanda – Karema (**km 321**) kwa kiwango cha Standard Gauge kwa sababu huku ndiko hasa kuna shehena kubwa ya mzigo ambayo inaweza kuleta manufaa kwa Taifa; na
- iii. Kuharakisha mapitio ya Sheria ya TAZARA ili kutoa fursa kwa Tanzania kuwekeza kwenye Reli hiyo ili iwe na manufaa kwa upande wa Tanzania. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuingia ubia na makampuni makubwa ili kupata vichwa na mabehewa na Serikali iwe inakodisha njia ya Reli.

c) Usafiri wa Anga

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/22 Serikali imekwishatumia **Shilingi billioni 557.8** katika kuimarisha usafiri wa anga na Shirika la ndege ATCL. Kamati ilipata fursa ya Kukutana na Mkurugenzi Mkuu wa ATCL na kubaini changamoto ambazo zinakwamisha shirika hilo kusimama imara na kupunguza hasara. Kwanza kutokana na athari za Ugonjwa wa Uviko-19 shirika liliathirika lakini hakukuwa na mpango wowote wa Serikali kulinusuru shirika hilo kama yalivyo mashirika mengine

ya ndege duniani badala yake Wakala wa Ndege za Serikali (Tanzania Government Flight Agency-TGFA) aliendelea kutoza gharama ya pango kwa ndege zote hata zile zilizopaki kwa kiasi cha dola za kimarekani **1.5 milion** kwa mwezi. Aidha, TGFA inaitaka ATCL kuweka amana ya matengenezo ya ndege yenye jumla ya **Shilingi Bilioni 1.2** kila mwezi wakati matengenezo ya ndege yanafanywa na ATCL wenyewe na si wakala wa ndege za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kwamba Mkataba wa ukodishaji wa ndege kati ya TGFA na ATCL unaitaka ATCL kuanza kulipa gharama za kukodi ndege mara tu baada ya kukabidhiwa ndege hata kama ndege hizo hazijaanza kufanya safari zake. Aidha, kamati ilibaini kwamba kasi ya kukamilisha viwanja vyta mikoa ni ndogo kuliko kasi ya kununua ndege. Vilevile kamati ilibaini kwamba **asilimia 86.4** ya madeni yote ya ATCL mdai ni Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali katika mwaka wa fedha 2022/23 kufanya yafuatayo ili kuimarisha usafiri wa anga na shirika la ndege la ATCL: -

- i. Serikali kulipa madeni yaliyokuwa ya Shirika la Ndege la ATCL kabla ya kufufuliwa ili kusafisha vitabu vyta ya Shirika;
- ii. Serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama za kukodi ndege ili shirika liweze kukua na kujidhesha kwa faida. Hatta hii iende sambamba na uwezekano wa kusamehe ada ya pango la ndege walau kwa miaka miwili kipindi ambapo athari za UVICO-19 ziliikuwa kubwa kati ya mwaka 2019/20 na 2020/21; na
- iii. Serikali kukamilisha haraka ujenzi wa viwanja vyta mikoa ili kuongeza mtandao na idadi ya miruko ya ndege za ATCL ndani ya nchi.

d) Bandari

Mheshimiwa Spika. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Bandari ambao ni Dira pana ya maendeleo ya Bandari zote nchini.

Mpango huu umezaaa miradi mingi kama vile mradi wa DMGP-Dar es Salaam Marine time Gateway Project ambaao una lengo la kuongeza uwezo wa Bandari ya DSM kuhudumia shehena ya mizigo kwa kufanya Uboreshaji wa Miundombinu ya Bandari ya DSM tani milioni 16 hadi tani milioni 25 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaushauri ufuatao kwa Serikali na Mamlaka ya Bandari: -

- i. Serikali kuhamisha makusanyo ya warfage kutoka mfuko mkuu wa Serikali na kuyapeleka kwenye akaunti ya TPA iliyoko Benki kuu ili kuhakikisha TPA inakuwa na ukwasi wa kutosha muda wote tofauti na ilivyo hivi sasa;
- ii. Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Bandari ukatekelezwe katika Bandari zote nchini na sio Dar es Salaam peke yake ili kutanua uwezo wa TPA kuhudumia shehena kubwa zaidi;
- iii. Mamlaka ya Bandari iboreshe mifumo ya Tehama kupitia mradi wa DMGP ikiwa ni pamoja na kufunga kifaa cha EDI-Electronic Data Interchange ili kurahisisha upakuaji na upakiaji wa makasha;
- iv. Kamati imeielekeza Serikali kupitia upya Masharti ya Mkataba wa TICTS pamoja na TPA ili kuangalia kama bado tunahitaji kampuni hiyo na hasa kwa uwekezaji uliofanyika katika bandari ya Dar es salaam umeiwezesha mamlaka hiyo kuhudumia gati zote; na
- v. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutoa eneo lililokuwa la mradi wa Kurasini *Logistic centre* kwa mamlaka ya TPA ili litumike kama *container deport* ya TPA kuliko ilivyo hivi sasa ambapo linatumika kama eneo la maegesho ya Malori.

3.2.2 Uendelezaji wa Viwanda na Ushiriki wa Sekta Binafsi
Mheshimiwa Spika. Sekta binafsi ni injini ya kuchochaea ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Hata hivyo sekta binafsi

nchini bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazohusu maeneo yafuatayo: -

- i) Wingi wa mamlaka za udhibiti zinazosimamia shughuli za sekta binafsi;
- ii) Ugumu katika upatikanaji wa mikopo na uwepo wa riba za juu na ucheleweshaji wa utolewaji wa maamuzi;
- iii) Wingi wa leseni, tozo na ada kwenye biashara moja; na
- iv) Ukiritimba katika kupata vibali vya kazi na ujenzi;

Mheshimiwa Spika, Kamati iliamini kwamba utekelezaji wa *Blueprint* ungekuwa mwarobaini wa changamoto hizi. Hata hivyo utekelezaji wake umekuwa wa kusuasua hivyo kutoleta matokeo tarajiwa. Hivyo Kamati inaielekeza Serikali katika mwaka wa fedha 2022/23 kuanza kwa kuunganisha Taasisi zinazofanya kazi zinazofanana kama vile; Weight and Measures (WMA) na TBS, TIC pamoja na EPZA, ili kurahisisha ufanyaji wa biashara na uwekezaji nchini. Aidha, kamati inaitaka Serikali kuwasilisha Bungeni mapema iwezekanavyo Muswada wa Sheria ya uwezeshaji wa Biashara (Business facilitation Act) ili kuweka mazingira rafiki na wezeshi ya ufanyaji biashara nchini.

3.2.3 Sekta ya Ardh na Mazingira

a) Utunzaji wa Mazingira na uvunaji wa Rasilimali.

Mheshimiwa Spika, Moja ya jambo ambalo halipewi kipaumbele ila lina gharama kubwa kuliko gharama zote ni utunzaji wa mazingira. Sote tutakubaliana kwamba tukiacha mazingira yakaharibika kwa namna yoyote ile madhara yafuatayo yatajitokeza na baadhi yamekwisha anza kuonekana. Kwanza umasikini utaongezeka kwa kiasi kikubwa, Pili Taifa litakumbwa na baa la njaa, tatu Uzalishaji wa Viwandani utakuwa wa gharama kubwa na ikiwezekana kufungwa kabisa kwa baadhi ya Viwanda, nne majanga ya asili kama vile mafuriko, vimbunga, ukame na kuongezeka kwa joto yatakuwa ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2022/23 ujielekeze kwanza katika kufanya mabadiliko kwenye sheria ya Mazingira sura namba 272 ili kutanzua vikwazo vyote vya kisheria vinavyosababisha mfuko wa mazingira usipate fedha kutoka "*Global Green Fund*". Pili ni kuanzisha programu maalumu za upandaji miti katika mashule, vyuo, Vijiiji, Mitaa kata na Tarafa ili kuanzisha misitu mipya nchini. Tatu kulinda vyanzo vyote vya maji na mito "catchment areas" na rasilimali zote zivunwe kiundelevu "*Sustainable utilization resource*"

Mheshimiwa Spika, Hivi karibuni sote tumeshuhudia Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan akihudhuria Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira ulioandaliwa na Umoja wa Mataifa huko Glasgow nchini Uingereza. Hii inayonyesha dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais katika kupambana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya Tabia nchi eckokwako Mhehimiwa Rais. Kamati inaamini sasa Serikali italicchukua suala la mazingira kwa uzito wake unaostahili.

b) Sekta ya Ardhi

Mheshimiwa Spika, Moja ya changamoto kubwa nchini ni mipango ya matumizi bora ya ardhi na upatikanaji wa hati miliki. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba hati miliki za maeneo yaliyopimwa zitolewe ndani ya siku saba pindi ambapo muhusika anakuwa amekamilisha taratibu zote za umiliki. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhuisha na kutengeneza mipango mipya ya matumizi ya ardhi kwa kuangalia shughuli za kiuchumi, kijamii na kimazingira.

3.2.4 Sekta za Jamii

a) Sekta ya Maji

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2020/21 Wizara ya Maji iliidhinishiwa Kutumia fedha za maendeleo jumla ya **shilingi Bilioni 705.009**. Hadi kufikia tarehe 31 Juni, 2021 wizara ya maji ilipokea na Kutumia jumla ya **Shilingi Bilioni 495.3** sawa na **asilimia 70.3**. kutofikiwa kwa lengo kumechangiwa na Fedha kutoka mfuko mkuu wa Serikali zilizotolewa kwa **asilimia 43.6** tu ya lengo. Rejea Jedwali na 3.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka miwili mfululizo fedha kutoka Serikali kuu zinatolewa chini ya **asilimia 43.6**. Kamati inaitaka Serikali katika mwaka wa fedha unaondelea kuhakikisha inatoa kwa **asilimia 100** fedha zote kutoka mfuko mkuu wa Serikali na kukamilisha miradi yote ya maji inayoendelea ili wananchi wapate maji. Vilevile Kamati inaitaka Serikali kueleza kwa Kina maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa miji 28 kwa gharama ya mkopo wa Dola za Marekani Milioni 500 kutoka India. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuandaa utaratibu utakaojulikana na Halmashauri zote nchini wa matumizi ya Mitambo 25 ilionunuliwa na Serikali kwaajili ya uchimbaji wa Visima kwa sababu kusipokuwa na utaratibu wa wazi mitambo hiyo inaweza kutumika vibaya.

Jedwali Na. 3: Mwenendo wa Bajeti ya Wizara ya Maji.

NA	MATUMIZI		BAJETI KWA MWAKA 2020/21	KILICHO PO KELEWA HADIJUNI, 2021	%
1.	KAWAIDA	Mengineyo (Oc)	11,171,714,000.00	11,393,533,787.33	101.9
		Mishahara (Pe)	17,103,431,000.00	15,774,999,625.67	92.2
			28,275,145,000.00	27,168,533,413.00	96.1
		Mfu ko-Majilii	175,912,837,000.00	159,128,222,635.50	90.4
		Mfu ko-Serikali	173,536,163,000.00	75,701,530,887.62	43.6
		NDANI	349,449,000,000.00	234,829,753,523.12	67.2
		NJE	355,559,930,000.00	260,465,559,981.00	73.3
2.	MAENDELEO		705,008,930,000.00	495,279,667,789.68	70.3
3.	JUMLA (1+2)		733,284,075,000.00	522,448,201,202.68	71.2

Chanzo: Wizara ya Maji

b) Sekta ya Afya

Mheshimiwa Spika. Kabla ya Serikali kuwasilisha Taarifa ya Mapendekezo ya Mpango Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya afya kwa mwaka 2020/21 na kubaini changamoto zifuatazo: -

- Kuwepo upungufu wa asilimia asilimia 53 ya mahitaji kwa watumishi wa Sekta ya Afya katika vituo vya kutolea huduma za Afya,
- Uwepo wa uhaba wa Dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya;
- Wigo mdogo wa wanufaika wa Bima ya Afya nchini, Hadi kufikia Juni 2020, jumla ya wanufaika wa bima za afya nchini walikuwa **asilimia 12** tu ya watanzania wote **Milioni 52**; na

iv. Uwepo wa mifumo mingi ya kielektroniki katika Sekta ya Afya isiyosomana na baadhi ya vituo vyta afya kutotumia mifumo iliyopo.

Mheshimiwa spika, Kamati inashauri masuala yafuayo kwa Serikali kuhusiana na Wizara ya Afya: -

- i. Uendelezaji wa miundombinu ya afya uende sambamba na upatikanaji wa wataalamu wa afya ili pindi miundombinu inapokamilika iweze kutoa huduma kama ilivyo kushindwa;
- ii. kuhakikisha kuwa mifumo inayotumika katika vituo vyote vyta kutolea huduma za afya inaweza kubadilishana taarifa; na
- iii. Kukamilisha haraka iwezekanvyo muswada wa Sheria ya Bima kwa wote na kuuwasilisha Bungeni katika Mkutano wa 6 wa mwezi Januari mwaka 2022 ili upitishwe na kuwa sheria kwa lengo la kutanzua tatizo la Bima nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kwamba endapo masuala hayo yatafanyiwa kazi ni wazi kwamba kutakuwa na mabadiliko makubwa katika sekta ya Afya.

4.0. UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2022/23

Mheshimiwa Spika Kamati ya Bajeti imepitia na kuchambua ugharamiaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2022/23. Jumla ya **Shilingi Trilioni 14.7** zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo pamoja na kulipa madeni ya wakandarasi wa ndani. Kamati ilibaini kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kufikia malengo ya utekelezaji wa Bajeti ya maendeleo kwa **asilimia 85-90**; vilevile kamati ilibaini ongezeko la Bajeti ya maendeleo imeongezeka kwa **Shilingi trilioni 1** toka **shilingi Trilioni13.7** hadi **Shilingi Trilioni 14.7** licha ya mafanikio ya juhudini hizi za Serikali kukusanya mapato na kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato. Kamati ilibaini kwamba mwenendo wa mapato unaonyesha kuwa nchi haijawahi kuvuka asilimia 90 ya fedha

za maendeleo kwa kipindi cha miaka 3. Hivyo kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba inakusanya mapato yake kwa ufanisi na kila anayestahili kulipa kodi anafanya hivyo, pia kuongeza wigo wa walipa kodi.

Jedwali Na. 4: Mwenendo wa Mapato na Matumizi ya Maendeleo

Sn	Chanzo	2019/21	2020/21	2021/22	2022/23
1.	Fedha za Ndani	9,737.7	10,043.2	10,723.0	11,635.4
2.	Fedha za Nje	2,510.9	2,736.0	2,955.9,	3,043.5
3.	Jumla	12,248.6	12,779.2	13,678.9	14,678.9
4.	Utekelezaji	8,365.1	10,667.1	10,191.6 (Matarajio)	
5	Asilimia ya Lengo	68.3	83.4	74.5 (Matarajio)	

Chanzo: Taarifa za Mapendekezo ya Mpango 2019-2021

4.1. Mikopo kutoka Export Credit Agency – (ECA)

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba Serikali imepanga kutumia mikopo kutoka Export Credit Agency – ECA kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Moja ya sharti la chanzo hiki cha mikopo ni ununuzi wa huduma na bidhaa lazima ufanyike kutoka nchi ambayo mkopo huo umepatikana. Kamati inaitaka Serikali kila inapochukua mkopo katika chanzo hiki makubaliano yawe ni **asilimia 50** au zaidi ya Huduma na bidhaa zinunuliwe ndani ya nchi. Lengo ni kuhakikisha kwamba fedha hizo zibaki kuendeleza uchumi wetu isipokuwa kwa huduma na bidhaa ambazo hazipatikani ndani ya nchi.

4.2. Hati fungani za Halmashauri

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kwamba Serikali imepanga kutumia vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia mpango kama vile hatifungani za Halmashauri, Hatifungani za Miundombinu (Infrastructure Bonds), Dhamana za Muda wa Kati (Medium Term Notes), Hatifungani ya Bluu (Blue Bonds), Hatifungani za Makampuni (Corporate Bonds), (Micro-saving bond) na (Lease Financing), hatifungani za mazingira; pamoja na matumizi ya taasisi za fedha kupata mitaji ya muda mrefu ya kugharamia miradi ya maendeleo hususan kupitia

syndication; bima na ugharamiaji hatarishi (risk financing) na hatifungani za kiislam (Sukuk).

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba vyanzo hivi vilikuwa kwenye Mpango wa pili wa maendeleo na Serikali haikuweza kuvitumia. Mfano hati fungani za Halmashauri Serikali ilikuwa imepiga hatua hadi kuwapeleka baadhi ya Wakurugenzi wa Majji ya Tanga, Dar es salaam na Arusha nchini Afrika Kusini ili wakajifunze namna ya kutumia chanzo hicho hata hivyo hakuna kiirofanyika. Kamati inaitaka Serikali katika mwaka wa fedha 2022/23 kutumia Hatifungani ya Miundombinu "*Infrastructure Bond*" kujenga Reli na Halmshauri zianze kutumia *Municipal Bond* kujenga miradi ya kibiashara kuliko kutegemea fedha kutoka mfuko mkuu wa Serikali.

4.3. Mapato ya Kodi, yasiyo ya Kodi na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/23 Serikali imekusudia kukusanya jumla ya **Shilingi Trilioni 28.6** Kutoka vyanzo vyote vya ndani. Kati ya mapato hayo mapato ya kodi yanatarajiwa kuongezeka kutoka **Shilingi Trilioni 22.5** Hadi **Shilingi Trilioni 24.2** sawa na ongezeko la **asilimia 7.9** Mapato ya Halmashauri yataongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 863,858** Hadi **shilingi billioni 937,051** sawa na ongezeko la **asilimia 8.5**. Aidha mapato yasiyo ya Kodi yanatarajiwa kuongezeka kutoka shilingi **billioni 3,049,774**. Mwaka 2021/22 hadi **shilingi billioni 3,393,050**, mwaka 2022/23. Sawa na ongezeko la **asilimia 11.3**. Hii inaonyesha kwamba Serikali ina nia ya kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato na kusimamia vyanzo vilivyopo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa rai kwa Serikali kwamba ongezeko hili lisitokane na ongezeko la ada na tozo ambazo zinaweza kuwa kikwazo kwa wananchi na kuleta athari katika jamii na uchumi kwa ujumla.

Jedwali Na. 5: Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato ya Serikali

Na	Chanzo	2021/22	2022/23	Asilimia ya Ongezeko
1.	Mapato ya Kodi	22,471,103	24,237,760	7.9
2.	Mapato yasiyo ya Kodi	3,049,774	3,393,050	11.3
3.	Mapato ya Halmashauri	863,858	937,051	8.5
5	JUMLA	26,384,735	28,567,861	8.3

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

5.0. TATHMINI NA UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2022/23

Mheshimiwa Spika. Mapendekezo ya Mpango na majukumu ya kila mdau yamebainishwa katika ufanyaji wa Tathmini na Ufuatiliaji, ambapo, Wizara ya Fedha na Mipango itaandaa Mpango Kazi wa Kitifa wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa miradi ya Kielelezo na ile ya Kimkakati kwa kuzingatia Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Tatoo wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika. Kamati inaitaka Serikali katika mwaka ujao wa fedha 2022/23 kutengeneza sera na kuleta Bungeni Muswada wa Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji (M&E). Jambo Hili limekuwa likisemwa miaka yote na Serikali haichukui hatua. Hivi sasa Serikali inafanya tathmini na ufuatiliaji bila kuwa Sera na sheria ya tathmini na ufuatiliaji na badala yake inatumia mlolongo wa sheria nyingi na muongozo wa uandaaji wa Bajeti kama maelekezo ya namna ya kufanya tathmini na ufuatiliaji. Mwenendo wa viongozi wakubwa na wakimbiza mwenye kugundua changamoto za utekelezaji wa miradi ya Serikali wakati viongozi wote wa maeneo husika wa Serikali wapo lifike mwisho. Aidha, Kamati inashauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha katika kutekeleza ufuatiliaji na Tathimini (M&E) kwani fedha nyingi zinazopotea katika miradi kwa kutofanya ufuatiliaji na tathmini. Bajeti hii ijumuishe mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini kwa maafisa masuuli na maafisa miradi Serikalini ili kuondoa uhaba wa wataalamu wa masuala ya Ufuatiliaji na Tathimini.

6.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MWAKA (2022/23) PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2022/23

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imepitia na kuchambua Mapendekezo ya Mpango wa Mwaka 2022/23 amba ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wenyewe Dhima ya *"Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."* Aidha, Kamati ilipata fursa ya kujadiliana na Serikali juu ya Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2022/23. Maeneo yaliyochambuliwa kwa kina ni msingi wa mpango, matarajio ya ukuaji wa uchumi, viashiria vya sekta mbalimbali na matarajio, miradi ya kimkakati, ugharamiaji wa Mpango, tathmini na ufuutiliaji wa Mpango pamoja na vihatarishi vinavyoweza kusababisha malengo ya Mpango yasifikiwe. Aidha, Kamati ilifanya ulinganifu wa matarajio na hali ilivyo sasa ili kuona endapo malengo tulijojiwekea yanaweza kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mapendekezo ya Mpango wa Mwaka 2022/23 ili kufanikisha azma ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati cha juu ifikapo 2025, na sio wa kipato cha kati cha chini, Kamati imependza kuwasilisha uchambuzi na mapendekezo yake katika maeneo yafuatayo: -

6.1. Maeneo ya Kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2022/23

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa shabaha, vihatarishi na maeneo ya Vipaumbele katika mpango wa mwaka 2022/23 na kubaini kwamba kuna uwezekano mkubwa wa Serikali kufikia shabaha zake kama zinavyoonekana kwenye Jedwali Na 6.

Jedwali Na. 6: Shabaha za Utekelezaji wa Mpango

Na.	Kiashiria	Lengo
1.	Pato Halisi la Taifa	5.2
2	mfumuko wa bei	3.0 hadi 5.0
3	mapato ya ndani kwa Pato la Taifa	15.9
4	Mapato ya Kodi kwa Pato la taifa	13.9
5	nakisi ya bajeti	3.0
6	akiba ya fedha za kigeni	Miezi 4

Chanzo: Mwongozo wa Uaandaji wa Bajeti kwa Mwaka 2022/23

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia maeneo ya kipaumbele Kamati imebaini yafuatayo: -

- i. Vipaumbele vimekuwa vingi sana, hivyo kufanya mgawanyo wa rasilimali unapelekwa katika maeneo mengi, mwisho wa siku vipaumbele vinavyotekelzwa ni vichache sana na vinatekelezwa kwa asilimia 70 hadi 80;
- ii. Kuna baadhi ya vipaumbele vipo katika kila Mpango na hakuna utekelezaji mfano ujenzi wa mabwawa ya Kidunda na Farkwa;
- iii. Bado suala la upatikanaji wa pembejeo na viuatilifu kwa bei nafuu halijapewa kipaumbele wala uzito na Serikali; na Upatikanaji wa Dawa bado ni changamoto.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya vipaumbele vichache kwa kila sekta ambavyo vinaweza kuleta matokeo ya haraka ama kumaliza changamoto zinazokabili Taifa na kuvitekeleza kwa mwaka mmoja ili kuchochaea uchumi na kuleta maendeleo ya watu kwa haraka.

6.2. Uhakiki na ulipaji wa Madeni ya Wakandarasi na Wazabuni

Mheshimiwa Spika, kuanzia 2015/16 hadi 2020/21, jumla ya madeni ya **shilingi 3,827,149,336,832.89** yaliwasilishwa kwa ajili ya uhakiki na yalihakikiwa. Kati ya kiasi hicho, madeni ya **shilingi 2,657,449,500,425.41** yalikidhi vigezo na **shilingi**

1,169,699,836,407.48 hayakukidhi vigezo. Aidha, katika kipindi hicho, madeni yenyе jumla ya **shilingi 2,150,566,068,791.91** yalilipwa na hivyo kuwepo na bakaa ya madeni ya **shilingi 506,883,431,633.50** ambayo hayajalipwa hadi Juni 30, 2021.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa madeni ya wakandarasi na wazabuni na kubaini mambo yafuatayo; wadai wengi hawana taarifa ya kwamba madeni yao yamehakikiwa na hayajakubalika kulipwa; Hakuna vigezo vilivybainishwa kuhusu nani alipwe wa kwanza, nani afuate na nani awe wa mwisho; Kuna changamoto ya uhakiki wa madeni kwa sababu endapo kuna Mhasibu wa Fungu, Taasisi au Wakala na kuna mkaguzi wa ndani inawezekana vipi deni lipite maeneo hayo yote na liende kuonekana halikidhi vigezo Wizara ya fedha na Mipango ilhali wakati huo Serikali imekwisha pokea huduma au bidhaa?

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kwanza, kuhakikisha msamiati wa uhakiki unaondoka kwenye taarifa zinazowasilishwa Bungeni kwa sababu inaonekana kama kimekuwa kichaka cha kukwepa kulipa madeni ya wadai. Aidha, uhakiki ufanyike kabla ya mpewa huduma hajapokea certificate na kuipeleka hazina kwa ajili ya malipo na sio Wizara ya fedha kuanza kuhakiki, jukumu hilo lifanywe na mkaguzi wa nje aliyeko kwenye mafungu. Aidha, makubaliano ya Mawaziri wa Fedha wa Afrika mashariki kwamba deni likishahakikiwa na zkipita siku 90 hayajalipwa yahamishiwe kwenye deni la Serikali na yaweyanalipwa kwanza kabla ya matumizi yote.

6.3. Ununuzi wa Dawa na Upatikanaji wa Dawa nchini

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya utafiti na kubaini ni kwanini kumekuwa na changamoto za upatikanaji wa Dawa katika Hospitali za Umma na vituo vya kutolea huduma na kubaini mambo yafuatayo: -

- i. Uagizwaji wa dawa na vifaa tiba unatumia kati ya miezi miwili hadi mitatu hivyo kama fedha za ununuzi wa Dawa zinatolewa mwezi wa 8 dawa zitafika kati ya mwezi wa 10 hadi wa 11;

- ii. MSD kupewa fedha za ununuzi wa dawa kwa mfumo wa mahitaji na sio kwa MSD kuwa na dawa kusubiria mahitaji;
- iii. Katika mwaka 2019/20 MSD hawakupewa fedha zozote za ununuzi wa dawa kwa sababu ya viashiria vya wizi;
- iv. MSD haina mtaji wa kutosha na mtaji uliopo unapungua kila kukicha kwa sababu inautumia katika kuondosha mizigo ya dawa msonge bandarini.
- v. Kufufua viwanda vya uzalishaji wa madawa mfano TPI.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuachana mara moja na utaratibu wa kuwahukumu wananchi kwa matendo ya watendaji wake kwa sababu tabia hii imeonekana maeneo mengi. Kuna Halmashauri hazipati fedha za maendeleo kwa sababu kuna ubadhili. Kuhusu MSD Kamati inaelekeza yafuatayo: -

- (i) Serikali itoe kiasi cha **Shilingi bilioni 150 kati ya mahitaji ya mtaji ya shilingi bilioni 363.93** kwa MSD ili iweze kununua madawa kwa wakati. Hatua hiyo itaiwezesha MSD kuagiza dawa kwa wakati na pindi mahitaji yanapojitokeza isichukuwe muda mrefu kupata dawa. Kamati inaishauri Serikali mtaji huu utoke kwenye mkopo amba Serikali huchukua Benki Kuu kila mwaka kwa mujibu wa kifungu cha 34 cha Sheria ya Benki kuu Sura namba 197;
- (ii) Aidha Serikali inashauriwa kuangalia uwezekano wa kutoa fedha za miezi miwili hadi mitatu mwanzo wa mwaka ili MSD iwe na mtaji wa kutosha muda wote.

Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Bunge, Kamati ya Bajeti itafuatilia utekelezaji wa masuala haya kila robo mwaka ili kuondoa changamoto ya upatikanaji wa Dawa nchini.

6.4. Kuhuisha Mpango wa Kupambana na Athari za Kijamii na Kiuchumi kutohana na Athari na Uviko-19 (Tanzania COVID-19 Social Economic Response and Recovery Plan) na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/23

Mheshimiwa Spika utakumbuka kwamba mara baada ya Serikali Kupokea fedha za IMF ulilazimika kuita Kamati yako ili ije kujadili matumizi yake. Maagizo yetu kwa Serikali ni kuhakikisha kwamba Mpango wa Kupambana na Athari za Kijamii na Kiuchumi kutohana na Athari na Uviko-19 unahuishwa sanjari na mpango wa mwaka 2022/23 ili fedha zitakapopatikana za kutekeleza mpango huo tusilazimike kuanza kujadili shughuli na miradi mipya na badala yake zielekezwe kwenye miradi moja kwa moja ya mwaka 2022/23 na isilazimike hata kuleta "Supplementary Budget" Bungeni.

6.5. Daraja Jipya la Selander kuwa Toll Bridge

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kutembelea na kukagua ujenzi wa Daraja jipya la Tanzanite na kutaarifiwa kwamba Hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa daraja jipya (km 1.03) na barabara unganishi zenye urefu wa km 5.2 ambapo ujenzi umefikia **asilimia 87.3**. Katika kipindi cha mwaka 2020/21, **Shilingi Bilioni 58.8** zimetumika". Kamati inaitaka Serikali pindi Daraja hili litakapokamiliika na kwa sababu limejengwa kwa mkopo kama lilitivo Daraja la Kigamboni liwe ni daraja la kulipia yaani "Toll bridge" Kamati inaona kwa kuwa kuna njia mbadala ambayo endapo mtu hataki kulipia daraja anaweza kupita ni vyema ushauri huo ukazingatiwa.

6.6. Utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati

Mheshimiwa Spika, Kamati katika uchambuzi wake imebaini kwamba maelezo ya Hatua za Utekelezaji wa Miradi ya kimkakati yamekuwa yale yale kila mwaka bila kuwa na maendeleo ya aina yoyote. Miradi iliyochambuliwa ni Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (Liquefied Natural Gas - LNG) – Lindi; Mradi wa Mkulazi II – Mbigiri Estate; Mradi Na. 4191; Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kiwango cha Kimataifa Standard Gauge Railway ya Mtwara – Mbamba Bay na

matawi ya Mchuchuma na Liganga; Mradi wa Makaa ya Mawe – Mchuchuma na Mradi wa Chuma -Liganga; Mradi wa Commuter Train Dar es salaam. Kamati inaitaka Serikali miradi hii kuanza kutekelezwa kwa mwaka wa fedha unaokuja kwa sababu miradi hii haitegemei Bajeti ya Serikali na kama haitekelezeki ni bora ikaondolewa kwenye miradi ya kimkakati jambo ambalo litakuwa si la busara kwa sababu miradi hii ina manufaa makubwa kwa Taifa.

7.0. MAONI YA UJUMLA

7.1. Uanzishwaji wa Mfuko wa Dharura

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 35 cha Sheria ya Bajeti kinataka Serikali kuanzisha Mfuko wa Dharura yaani “*contingency fund*”. Pamoja na uwepo wa takwa hilo kisheria, bado Serikali hajaanzisha Mfuko huo na badala yake imekuwa ikitenga fedha za dharura kupitia **Fungu 21 - Hazina**. Uwepo wa Mfuko huu ungeisaidla sana Serikali inapotokea majanga kama vile liliivyo gonywa la UVIKO-19. Kamati inaitaka Serikali katika mwaka wa fedha 2022/23 kuanzisha mfuko huu ili utusaidie tunapopatwa na majanga na kuondokana na utaratibu wa kuweka fedha za dharura katika fungu 21.

7.2. Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya jitihada kubwa sana kuboresha huduma za Afya nchini jambo ambalo ni la kupongeza sana. Hata hivyo, changamoto kubwa iliyoko mbele yetu ni namna gani wananchi wanapata huduma hizo kwa bei nafuu, kwa ubora na kwa haraka. Suluhisho la jambo hili ni kuwa na Sheria ya Bima kwa wote “*Universal Coverage Health Insurance*”. Ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuleta Muswada wa Sheria hiyo mbele ya Bunge lako tukufu ili iende sambamba na utekelezaji wa Mpango huu wa Tatu kwa sababu hivi sasa ni **asilimia 20** tu ya watanzania wako kwenye Mifuko ya Bima.

7.3. Uzingatiaji wa Takwimu za Umaskini katika kugawanya rasilimali za Serikali.

Mheshimiwa Spika. Viashiria vyta kupima hali ya umaskini nchini hupatikana kwa kutumia taarifa za Utafiti wa Mapato

na Matumizi ya Kaya Binafsi (Household Budget Survey - HBS). Utafiti huu hufanyika kila baada ya miaka mitano. Utafiti wa HBS 2017-18 umeonesha kuwa asilimia 26.4 ya watu wa Tanzania Bara wana umaskini wa mahitaji ya msingi kama vile chakula, mavazi, malazi, maji, umeme, usafirishaji, mawasiliano, afya, elimu na huduma nyingine za kijamii. Kamati inashauri Serikali kwamba ugawaji wa rasilimali uzingatie hali ya umaskini na mahitaji ya eneo husika. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kumekuwa na kasumba ya kugawa rasilimali kwa usawa wa kiwango bila kuangalia hali ya umaskini wa mahitaji ya msingi. Mfano, umaskini mkubwa wa mahitaji ya msingi ni **asilimia 31.3** na maeneo ya mijini ni **asilimia 15.8**. Vile vile, **asilimia 8.0** ya watu Tanzania Bara wanaishi umaskini uliokithiri. Umaskini huu ni mkubwa vijiji (asilimia 9.7) kuliko ilivyo maeneo ya mijini (**asilimia 4.4**).

7.4. Kuchangamsha Soko la Hisa (DSE)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya mapendekezo ya Mpango inaonyesha jinsi soko la hisa la Dar es Salaam (DSE) linavyofanya kazi kwa ufanisi. Katika taarifa hiyo mauzo ya hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka kwa asilimia 21.13 na kufikia shilingi triliuni 2.35 katika kipindi kilichoishia Agosti 2021 ikilinganishwa na mauzo ya shilingi triliuni 1.94 yaliyorekodiwa katika kipindi kilichoishia Agosti 2020. Vile vile Mauzo ya hatifungani za Kampuni (*corporate bonds*) zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam yaliongezeka na kufikia **Shilingi Bilioni 1.98**, sawa na ongezeko la **asilimia 51.15** katika kipindi kilichoishia Agosti 2021 ikilinganishwa na **Shilingi Bilioni 1.31** katika kipindi kilichoishia Agosti 2020.

Mheshimiwa Spika. Pamoja na jitihada hizi za Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo ili kuchangamsha soko la hisa la Tanzania: -

- i. Kuhakikisha elimu ya ununuzi na uuzaji wa hisa na masoko ya hisa na mitaji inafundishwa kuanzia elimu ya msingi mpaka vyuo vikuu;

- ii. Serikali kuanzisha utaratibu wa kutafuta mitaji katika soko lake la hisa la ndani ili kugharamia miradi ya maendeleo yenye sura ya kibashara; na
- iii. Kufungua soko la hisa kwa kufanya “Full liberalization of The Capital market” ili kuwe na washiriki wengi kuliko hivi sasa ambapo kuna vikwazo;

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini hayo yakifanyika tunaweza kuchangamsha soko la hisa kuliko ilivyo hivi sasa.

7.5. Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa njia ya ubia (PPP)

Mheshimiwa Spika, Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ni njia mbadala wa kufadhili miradi ya maendeleo ambayo inazalisha faida ili Serikali ijikite kwenye maeneo mengine ambayo hayavutii Sekta Binafsi. Miradi ya PPP iliyobainishwa katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2022/23 ni ile ile ambayo imekuwa ikianishwa kila mwaka na hakuna utekelezaji wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, kamati imebaini kwamba umeongezeka mradi mmoja wa Kusimika Boya la Kuegeshea meli za mafuta katika Bandari za Dar es Salaam na Tanga jambo ambalo kamati inaona si sawa kutekelezwa kwa PPP kwa sababu ni kutoa *monopoly* kwa mbia ambaye pamoja na kumiliki boyo hiyo atafanya biashara hiyo ya gesi na Mafuta na kamati inashauri Badala yake apewe TPA kwa sababu ni mradi ambao una faida ndani ya muda mfupi. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kufanya tathmini na kubainisha sababu za Msingi zinazosababisha kukwama kwa utekelezaji wa Miradi kwa njia ya PPP ili Taifa linufaike na njia hii ya utekelezaji wa miradi ambayo inamanufaa makubwa kwa Taifa. Aidha, ikiwezekana tubadili namna tunavyotekeliza miradi ya PPP.

7.6. Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya masikini wa TASAF umeweza kuongeza uhakiki wa kaya kutoka **kaya 991,020** na kufikia kaya **1,013,635** kutoka vijiji **10,293** kwenye maeneo **187** ya

utekelezaji. Pia katika Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 zimetengwa Shilingi Bilioni 5.5 kwa ajili ya kuwezesha kaya masikini **34,641** kukidhi mahitaji ya msingi kuititia TASAF. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo hata hivyo, Kamati ina maoni kwamba mradi huu wa kunusuru kaya masikini unahitaji kuwa endelevu. Hivi sasa mpango huu unatekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Duniani lazima Serikali ianze kufikiria kuweka kwenye mipango yake mradi huu ili pindi fedha za mkopo zitakakapokuwa zimefikia ukomo iwe rahisi kwa Serikali kuuundeleza la sivyo wananchi watarudi kwenye wimbi la umasikini. Vilevile Kamati inashauri ufuatiliaji na tathimini wa kina ufanyike kwa kila hatua ya utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini. *Results Based monitoring* ifanyike ili kulinganisha malengo ya mpango na uhalisia wa matokeo yake. Hatua hii itasaidia uboreshaji wa ufanisi na ukaguzi wa mpango katika kutekeleza malengo yake.

7.7. Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, moja ya jambo ambalo Kamati imebaini ni kutawanyika kwa juhudini ya kuwawezesha wananchi kiuchumi katika Sheria mbalimbali, Taaaisi na Idara na Wakala wa Serikali. Aidha kamati ilibaini kwamba pamoja na Waziri Mkuu Mheshimiwa Majaliwa Kassimu Majaliwa kuagiza kuunganishwa kwa mifuko yote ya Serikali hakuna Taarifa rasmi yoyote iliyokwisha wasilishwa kuhusu utekelezaji wa jambo hilo. Kamati inaitaka Serikali kwanza kutekeleza mara moja agizo la kuunganisha mifuko na pili kufanya tathmini ya uwezo wa kifedha wa mifuko urejeshwaji wa mikopo na ufanisi wake. Aidha, kamati inaitaka Serikali kuititia upya sheria ya uwezeshaji wananchi kiuchumi na kuhakikisha kwamba juhudini zote za uwezeshaji zilizotawanyika katika sheria mbalimbali zinakuwa chini ya sheria moja na isimamiwe na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

7.8. Mapitio ya Viwago vya Fedha vinatolewa kuititia Mfuko wa Jimbo

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Jimbo umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Na 16

ya Mwaka 2009. Kifungu cha 5 cha sheria hiyo kinaweka vigezo vitakavyotumika katika kugawa mapato ya mfuko huo. Hata hivyo kamati imebaini kwamba kifungu hicho hakikuweka kigezo cha kulinda thamani ya Shilingi na hivyo viwango vilivyorejewa mwaka 2015 havijawahi kurejewa tena kwa kipindi cha miaka 6. Ni wazi kwamba thamani ya shilingi ya mwaka 2015 na uwezo wake wa kununua bidhaa na huduma si sawa na ilivyo hivi sasa hasa ukizingatia karibia kila mwaka thamani ya shilingi inashuka kwa asilimia 3 sawa na kasi ya mfumuko wa bei. Hii inamaanisha kwamba thamani ya shilingi hupungua sanjari na mfumuko wa bei ambao kwa kipindi cha miaka 6 umekuwa kwa wastani wa asilimia 3, hii inamaanisha uwezo wa kununua bidhaa na huduma unashuka kwa asilimia takribani 18 kwa miaka 6. Kamati inaitaka Serikali kufanya mapitio ya viwango vyta mfuko wa jimbo na kuvihiusha na hali ya uchumi ya sasa. Aldha, Serikali iliete mabadiliko bungeni ya kifungu cha 5 cha sheria hiyo ili liwekwe sharti la kurejea viwango vyta mfuko huo walau kila baada ya miaka miwili.

7.9. Tatizo la ajira na Upangaji wa Wafanyabiashara wadogo maarufu kama Wamachinga

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na uamuzi wa Serikali wa kuwaondoa wafanyabiashara wadogo (wamachinga) katika maeneo yasiyo rasmi na baadhi yao kupelekwa kwenye maeneo yaliyotengwa kwa shughuli hizo kwenye Halmashauri za Majiji, Manispaa na Wilaya. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba kumekuwa na ongezeko kubwa la nguvu kazi lisiloendana na uwezo wa uchumi kuajiri. Hivyo ni wazi kwamba lazima vijana watajitafutia namna ya kupata Kipato. Pia, ni jukumu la Serikali kuhakikisha vijana hao ambao wamelazimika kuwa wamachinga, wapate fursa na maeneo sahihi ya kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, Hivyo, Kamati inaushauri ufuatao kwa Serikali:-

- i. Serikali kuptitia Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ihakikishe inatenga maeneo rasmi kwa ajili ya wamachinga na maeneo hayo yawe ni yale yanayovutia

ufanyaji biashara kwa kuwekewa miundombinu ya msingi na yawe karibu na maeneo yaliyozoleka;

- ii. Kuhakikisha maandalizi ya maeneo rasmi ya biashara ya wamachinga pamoja na ujenzi wa miundombinu ya msingi yanafanyika katika mwaka huu wa fedha 2021/22 na kukamilika katika mwaka ujao wa fedha 2022/23 ili kuwawezesha wafanyabiashara hao waendelee kujitafutia kipato na kutunza familia zao;
- iii. Lazima Serikali ifanye tathmini ya soko la ajira nchini ili kuja na mipango ya kuchochea ajira hasa kwa vijana; na
- iv. Lazima sasa suala la kurasimisha sekta isiyo rasmi liwe endelevu ili kuondokana na suala la kuhamisha wafanyabiashara wadogo kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini yasipofanyiwa kazi mapendekezo haya tunaandaa mgogoro mkubwa kati ya Serikali na wananchi hasa hawa wafanyabiashara wadogo ambao wengi ni vijana.

8.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb), kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako na kwa maelekezo yako ambayo umekuwa ukitoa mara kwa mara kwa Kamati hii. Maelekezo ambayo umekuwa ukitupatia mara kwa mara yamekuwa kwa kiasi kikubwa yakiboresha utendaji kazi wa Kamati na ushauri tunaoutoa kwa Serikali. Kwa hilo tunapenda kukushukuru sana. Pia napenda kumshukuru Mhe. Tulia Ackson, Mb, Naibu Spika kwa miongozo ambayo kwa pamoja mmekuwa mkitupatia. Vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Bi. Nenelwa Mwihambi na timu yake kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, kipekee napenda kumshukuru, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb, Waziri wa Fedha na Mipango na Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni, Mb, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati. Nawashukuru Katibu Mkuu Fedha na Manaibu Katibu Wakuu

wa Wizara na wataalamu wote ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili Mapendekezo ya Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Mathew Kileo, Makatibu wa Kamati Emmanuel Rhobi, Lilian Masabala, Maombi Kakozi na Wilfred Akasi pamoja na Msaidizi wa Kamati Grace Mwenye kwa miongozo yao na ushauri wa kiutalaam hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshuru Mhe. Omari M. Kigua M/Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1. Mhe. Sillo Daniel Baran, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb	M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Shally Josephha Raymond, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Subira Khamis Mgusu, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Halima James Mdee, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Dkt Charles Kimei, Mb	Mjumbe
23. Mhe. Mariam Kisangi, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja.

Sillo Daniel Baran (Mb)

MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI
3 Novemba, 2021

MHE. OMAR M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono nakushukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa kutupitisha katika hotuba na kwa niaba ya Kamati ya Bajeti tunawashukuruni sana Kamati ya Bajeti kwa muda ambao mmeutumia kuchambua na kutapatia maoni yenu ambayo yatakuwa ni mwongozo mmojawapo katika kujadili.

Waheshimiwa Wabunge Bunge hili la awamu hii linaongozwa hasa na Kifungu cha 113 cha Kanuni zetu za Bunge za Kudumu ambazo nitazisoma kidogo si mahali pote 113(1) inasema kwa mujibu wa Ibara 63(3)(c) ya Katiba Serikali itawasilisha Bungeni mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa muda mrefu ambao utajadiliwa mapema iwezekanavyo katika Mkutano wowote wa Bunge. Hayo ni maneno ya katiba.

(2) Bila kuathiri masharti ya fasili ya kwanza Bunge katika mkutano wake wa mwezi Oktoba au Novemba ambao ndiyo mkutano huu kila mwaka isipokuwa kwa mkutano wa kwanza wa Bunge jipya kama ule wa mwaka jana wakati kama huu kwa siku zisizopungua tano litakaa kama kamati ya mipango kwa ajili ya kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika Mwaka wa Fedha unaofuata.

Katika mkutano huo Bunge pamoja na mambo mengine litafanya shughuli zifuatazo:

(a) Kupokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu mwongozo wa kuandaa mpango wa bajeti ya Serikali ambao mwongozo huo tayari mnao kwenye vishkwambi.

(b) Kupokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya mapato ya Serikali kwa mwaka unaokuja.

(c) Kupokea, kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa Mpango wa Serikali na vipaumbele vya mpango huo. Kabla mapendekezo ya mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kuwasilishwa Bungeni, mapendekezo hayo yatajadiliwa na Kamati ya Bajeti. Jambo ambalo limetekelizwa tayari.

Mjadala kuhusu mapendekezo ya mpango nao umeelekezwa na Kanuni utatanguliwa na maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti iliyochambua mapendekezo hayo na maoni ya kambi kama ingekuwepo mjadala huo utaendelea kwa siku tano na utahitimishwa na Serikali kwa kutoa maelezo mafupi kwamba imepokea maoni na ushauri wa Bunge.

Mwisho mjadala wa mapendekezo ya Mpango wa Taifa kanuni zinaendelea kusitiza utahusu mambo ya jumla na Wabunge watachangia na kuishauri Serikali kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa sera za kiuchumi, za kifedha, za kodi na vipaumbele katika mpango wa bajeti ya Serikali. Hayo ndiyo maelekezo ya kanuni kwa hiyo hatukutarajii ukisimama sasa unapuyanga tu kisukuma Sukuma, kinyamwezi kinyamwezi tunatarajia utaenda kufuatana na kanuni zilivyoweka mambo yake sawasawa. (*Makofii*)

Kwa jinsi hiyo kwa vile ni muhimu sasa kupitia *documents* hizi ambazo tumezipata pamoja na hotuba hii ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kwa niaba ya Kamati ya Bajeti, ningelishauri kwamba basi kwa hatua hii tuende tukapitie *document* zetu, na kesho asubuhi tunapokutana saa nane mchana kesho tuko tayari na uchangiaji ukianza na Serikali nayo inakuwa iko tayari kwa ajili ya kupokea maoni yetu. (*Makofii*)

Ningeomba upande wa Serikali pia kama Waziri anakuwa hayupo basi Naibu awepo au Naibu hayupo Waziri akawepo au wote wawili ili tusikilize kwa pamoja inawezekana Mbunge anachangia kwenye sekta ambayo ndiyo sekta yako kwa maoni ya mwakani mipango iweje ili tuweze kwenda pamoja katika siku hizi za kujadili Mpango.

Kwa kuwa mmenikubalia hilo basi sasa niseme moja kwa moja kwamba Bunge linarejea.

(Bunge Lili'rejea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaweza tukakaa, Waheshimiwa Wabunge kama nilivyoongea dakika chache hapo nyuma kwa kweli tumepata *documentzote* sasa kutoka Serikalini na tumepata ya kamati kwa hiyo, tuna kazi ya kutosha ya kupitia ili kuanzia kesho tuweze kuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kuchangia tukiongozwa na wenzetu wa wale wa Kamati ya Bajeti amba walikuwa na muda wa kutosha zaidi na ningeliwashauri nyote tuwe tayari kuchangia kwa dakika kumi kumi ukiweza hata tano ili umuachie na mwingine wale amba wanapenda kusema mwisho niwahakikishie hawatapata nafasi maana wako watu lazima asikilize wenzake mia moja ndiyo apate wazo. Kwa sababu muda ndiyo huu kwa hiyo ni vizuri kama una cha kuchangia ukawa katika wale watakaopeleka jina mapema kusudi upate nafasi ya kuweza kuchangia.

Kwa vile sasa shughuli zetu zimekamilika nadhani leo kuna mechii kubwa ya Namungo siyo wale amba mpila unaanza tu watu wanaanza kupigwa *red card* ili timu ishinde maana ligi ya mwaka huu ina mambo kwa kweli Waziri wa Uwekezaji, Waziri wa Fedha wote hawa daa! Tuna kazi mwaka huu. *(Makof)*

Basi Waheshimiwa Wabunge niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa nane kamili mchana.

*(Saa 11.15 Jioni Bunge Lili'ahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 4 Novemba, 2021 Saa Nane Mchana)*